

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Thelathini na Saba - Tarehe 1 Agosti, 2003**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika(Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza, redio ilitangaza kwa makosa kwamba Wabunge wote wanakwenda Rufiji kuhudhuria Sherehe ya Ufunguzi wa Daraja. Sio kweli, Bunge linaendelea kama kawaida siku ya leo. Wapo Wabunge wachache walioruhusiwa kwenda, lakini watakwenda kutuwakilisha katika sherehe hiyo, lakini sio Wabunge wote.

Kikao cha 37 cha Mkutano wa Bajeti kinaanza.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2001/2002 (*The Annual Report and Accounts of the National Social Security Fund for the Year 2001/2002*).

Hotuba ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MHE. HAROUD SAID MASOUD (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo katika mwaka uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 359

**Ofisi kwa Ajili ya Madiwani**

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI (k.n.y. MHE. GEORGE F. MLAWA aliuliza:-**

Kwa kuwa Madiwani ni wawakilishi muhimu sana wa wananchi katika Halmashauri zao za Wilaya na Miji; na kwa kuwa Madiwani kama ilivyo kwa Maafisa Watendaji wa Kata wanatakiwa nao wawe na Ofisi rasmi kwa ajili ya kusikiliza shida za wananchi wao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa pale palipo na Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata vile vile panakuwepo na Ofisi rasmi ya Mheshimiwa Diwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Mlawa, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Madiwani ni wawakilishi muhimu sana wa wananchi na kuwa wanastahili kuwa na Ofisi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao chini ya uwakilishi. Ofisi hizi zitawezesha wananchi kukutana na mwakilishi wao kwa urahisi zaidi. Serikali ilikwishakutoa maelekezo kwa Halmashauri zote ya kuzitaka kujenga Ofisi za Maafisa Watendaji wa Kata kwa kila Kata. Ofisi hizo zinapaswa kuwa na vyumba vya Maafisa wote wa Halmashauri walioko kwenye ngazi ya Kata, Diwani, Vyumba vya Mikutano ya Kamati ya Maendeleo ya Kata na vyumba vya huduma nyinginezo zinazoambatana na Ofisi hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi kama hizo za Kata zinapaswa kujengwa katika kila Kijiji na Mtaa na kisha kupeperushwa bendera ya Halmashauri na ya Serikali Kuu ili kuonyesha alama ya kuwepo kwa utawala wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelekezo hayo, baadhi ya Halmashauri zilikwisha kuikamilisha ujenzi wa Ofisi za Kata ambazo zina vyumba vya Ofisi ya Diwani, Afisa Mtendaji wa Kata na Watendaji wengine.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote tusaidiane kutoa msukumo kwa kushirikiana na Halmashauri na wananchi ili kuhakikisha Ofisi hizo zinajengwa kwa maendeleo na manufaa ya wananchi.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Madiwani hawapati mshahara wanapata posho, isingekuwa vizuri wapewe mshahara ili nao waweze wakapewa viinua mgongo baadaye?

**SPIKA:** Suala la msingi linahusu Ofisi sio mshahara.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru umenipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Maafisa Watendaji hawa wa Kata wataanza kuhudumiwa mishahara na vitu vingine na Serikali Kuu.

Je, hawa Waheshimiwa Madiwani kwa nini pia na wao shughuli zao, posho zao na kadhalika zisishughulikiwe na Serikali Kuu?

**SPIKA:** Bado! Bado nawarejesha kwenye Kanuni. Swali la nyongeza lazima litokane na swali la msingi. Kwa hiyo, hili nalo ni swali jipya.

Na. 360

**Watu Wanaozoa Takataka Mijini Bila Vifaa vya Kinga**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa Afya ya Mtanzania ni raslimali muhimu sana kwa uhai wa Taifa letu:-

(a) Je, Serikali inayo taarifa kwamba kuna wazoji taka katika maeneo ya Miji, Majiji hasa Dar es Salaam ambao wanafanya kazi hiyo bila vifaa vya kinga kwa afya zao?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kitendo cha kuachia wazoa taka kufanya kazi yao wangali mikono mitupu bila hata viatu kwenye maeneo niliyoyataja ni kitendo cha kuhatarisha afya zao?

(c) Je, Serikali iko tayari kuliahidi Bunge hili kwamba wafanyakazi hao watapatiwa vitendea kazi vitakavyohakikisha usalama wa afya zao haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya kulinda afya ya jamii kazini Na. 6 ya mwaka 1982 (*The Occupational Health Services and Safety No. 6 of 1982*) wahudumu wote wanaofanya kazi ya kuzoa taka Mijini wanatakiwa wawe na vifaa vya kinga ya afya kama ifuatavyo:-

Kuvali viatu (*gum boots*) na *gloves* wakiwa kazini, vifaa vya kufunika kinywa (*mouth masks*), vifaa vya kufunika pua (*nose masks*), wavae sare za kazi, wapatiwe elimu juu ya umuhimu wa kuvali na wazingatieve usafi binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tulizonazo ni kwamba Makampuni mengi kaitika Jiji la Dar es Salaam yametekeleza suala la kulinda afya ya jamii kwa watumishi wanaofanya kazi ya kuzoa taka kama sheria inavyoagiza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ziko taarifa kwamba baadhi ya watumishi hao kwa sababu ya hali ya hewa ya joto katika Jiji la Dar es Salaam hawavai *gum boots* na *gloves* kwa sababu wanapovaa inasemekana wanapata madhara ya ngozi (*rashes*) na hivyo wanaamua wenyewe kufanya kazi hiyo bila kutumia vifaa hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi tunalikubali wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba kama wako watumishi wanaofanya kazi ya kuzoa taka bila tahadhari ni kitendo cha kuhatarisha afya zao.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza hapa juu suala hili ni la kisheria na linatakiwa kuzingatiwa na bado linazingatiwa ukiondoa baadhi yao ambao hawatumii vifaa hivi kwa sababu nilizozieleza. Hivyo basi naomba nichukue nafasi hii kuziagiza Halmashauri zote kwa mara nyiningine tena kuzingatia sheria hii ili tulinde afya za wananchi. Aidha, natoa wito kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na watumishi wanaohusika kila watakapoona vitendo ya aina hii basi watoe taarifa haraka Serikalini.

Mheshimiwa mwisho, Serikali itaendelea kuwahimiza wahusika wote kuhakikisha watumishi wao wanatumia vifaa vya kinga ya afya na kuendelea kutoa elimu juu ya suala hili. Kwa watumishi wanaopata madhara kwa kutumia vifaa hivyo Halmashauri zinaagizwa kutowaajiri kazini ili kunusuru afya zao.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala la kuzoa taka kwamba linahatarisha maisha ya wananchi wanaozoa. Lakini kwa Mji wa Dodoma kuna mifereji ya kuitisha maji ya mvua, kwa sasa mifereji hiyo inatumika kama mifereji ya kuitisha majitaka kutoka majumbani na maji yamezagaa Mjini Dodoma kuhatarisha maisha ya wananchi.

Je, Waziri anatamka nini juu ya mifereji hii na wale wanaowajibika watachukuliwa hatua gani kuhakikisha kwamba mifereji ya majitaka itumike na inasafishwa? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala hili nadhani pande zote mbili tutabidi tubebeashane lawama kama mifereji hii ilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maji ya mvua lakini wananchi wameamua vile vile kutumia mifereji hiyo kama mifereji ya maji ya majitaka basi tutachukua hatua zinazostahili baada ya kuzungumza ma wahusika wa Manispaa wa Dodoma.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongenza.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi ameeleza kwamba yapo Makampuni ambayo hayawapi vifaa wafanyakazi wanaozoa takataka. Je, ni hatua zipi za kisheria zimechukuliwa dhidi ya watu hawa ili kuwasaidia wanyonge hawa wanaohangaika kutafuta riziki kidogo? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu nilisema kuwa kwa sehemu kubwa kabisa Makampuni mengi yamezingatia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *impliedly* ni kwamba yako baadhi ambayo inawezekana hayatekelezi jambo hili vizuri na ndiyo maana katika ufanuzi nimekiri kwamba tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba sasa hatua zinazostahili zinachukuliwa maadamu tumeshapata maelekezo haya mazuri kupitia hili swali.

Na. 361

#### **Gari la Kituo cha Polisi cha Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa gari la Kituo cha Polisi Mpwapwa ni bovu; na kwa kuwa gari hilo limepelekwa Dodoma Mjini kwa ajili ya matengenezo na sasa ni muda mrefu umepita bila kurudishwa kituoni:-

(a) Je, ni lini gari hilo litatengenezwa na kurudishwa kituoni?

(b) Kwa kuwa gari hilo ni bovu sana na haliwezi kwenda vijiji vya mbali; je, Serikali ina mpango gani wa kukipatia kituo hicho gari jipya ili liweze kutoa huduma ya kupambana na uhalifu katika Wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa gari lenye namba za usajili *STJ 562 Land Rover 110 Pick up* la Kituo cha Polisi Mpwapwa lilikuwa bovu na lililetwa Dodoma kwa ajili ya matengenezo. Napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa gari hilo sasa limekwisha tengenezwa na hivi sasa limerudishwa Mpwapwa na linaendelea na utoaji wa huduma katika kituo hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ili Kituo cha Polisi cha Mpwapwa kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kinahitaji gari jipya. Hali hiyo sio tu kwa Wilaya ya Mpwapwa tu bali ni takribani kwa Wilaya nyingi na vituo vingi hapa nchini.

Hata hivyo, kadri Bajeti ya Jeshi la Polisi itakavyokuwa bora zaidi, magari mapya yatanunuliwa kwa ajili ya Vituo vya Polisi mbalimbali hapa nchini ikiwa ni pamoja na Kituo cha Polisi Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa George Lubeleje, kwa kufuatilia kwa makini suala la vitendea kazi vya Jeshi la Polisi katika jimbo lake. (*Makofî*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza napenda nimpungeze sana *RPC* wa Dodoma kwa jinsi anavyojitahidi kufanya kazi zake vizuri na kuendelea kulikarabati gari hili ili liweze kufanya kazi. Sasa kwa kuwa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 55 hadi shilingi bilioni 70. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kumwongeza fedha *RPC* wa Dodoma ili gari hili liendelee kutengenezwa kwa sababu kama nilivyo sema ni bovu?

Swali la pili, pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba akinunua magari mapya atapeleka gari jipya Mpwapwa. Je, sasa ni magari haya yatanunuliwa lini kwa sababu Bajeti tumeshapitisha ili yapelekwe katika Vituo vya Polisi vyote nchini? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, pongezi za *RPC* nazipokea kwa niaba yake na tutamfikishia.

Kuhusu kuongeza Bajeti kwa *RPC* wa Dodoma kwa ajili ya mafuta na matengenezo ya magari na suala la kununua magari mapya kwa ajili ya Polisi, napenda nirudie maeleo niliyoyatoa juzi hapa hapa katika Bunge hili kwamba ni kweli Bajeti ya Jeshi la Polisi imeongezeka kwa viwango ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja. Katika ongezeko hilo Bajeti kwa ajili ya maendeleo ni shilingi bilioni 5.3 sasa hizo fedha zikishaanza kwenda katika yale maeneo tuliyoyataja kwenye Bajeti yetu ya kipaumbele ambayo tulisema kwanza inakwenda kwenye mawasiliano, majambazi sasa hivi yana vyombo vya mawasiliano vya hali ya juu, Jeshi la Polisi lina upungufu wa vyombo vya mawasiliano.

Kwa hiyo, Bajeti hii sehemu kubwa itakwenda kuimarisha vyombo vya mawasiliano. Kipaumbele kingine ni nyumba za askari halafu magari. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba hatutakuwa na fedha za kutosha kununua magari kwa kila Wilaya. Narudia kusema kwamba hayo magari machache tutakayoweza kuyanunua tutaanza kuyapeleka katika zile Wilaya ambazo hazina kabisa magari ya Polisi kwanza. Sasa baada ya hapo ndipo tutaangalia na Wilaya zingine zingine pamoja na Wilaya ya Mpwapwa. (*Makofî*)

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa nusu ya Wilaya ya Mpwapwa ni milima na matengenezo aliyoyazungumza Mheshimiwa Naibu Waziri yamefanya au yamewezesha gari lile kusafiri au kufanya kazi kwenye tambarare tu. Je, nataka kujua ni lini ataleta fedha za matengenezo mazuri zaidi za kuweza kufanya gari lile lifike hata milimani ambako kuna uhalifu mkubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba gari hilo limeshafanyiwa matengenezo mazuri ya hali ya juu pamoja na kuwekewa matairai mapya ili gari lipande milima vizuri zaidi na kwamba kama katika kipindi hiki inatokea dosari nyininge kwamba gari hili pengine halikutengenezwa sawa sawa linashindwa kupanda milima ya Mpwapwa tupewe taarifa tunaahidi kuendelea kulitengeneza ili liwe imara liweze kuhudumia Wilaya ya Mpwapwa kwa ukamilifu.

Na. 362

#### **Sheria ya Kinga kwa Wabunge**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa kazi ya Mbunge ni pamoja na kuhudhuria Mikutano ya Bunge na Kamati zake, lakini sehemu kubwa ya kazi ziko kwenye Majimbo yao ya Uchaguzi:-

- (a) Je, kuna sheria ngapi zinazompa Kinga Mbunge nje ya eneo la Bunge?
- (b) Je, kwa nini Wabunge wamenyimwa kinga kama ile wanayoipata wakati wakiwa kwenye Shughuli za Bunge?
- (c) Je, sheria hizo hazipingani?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya kinga kwa Wabunge, kama ilivyo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Majaji na Mahakimu, imejengeka katika msingi wa kuwalinda wasishtakiwe pale wanaposema au kufanya jambo lolote linalohusu shughuli mbalimbali za jamii Bungeni. Kinga hii inalenga katika kulinda haki yao ya msingi Bungeni ya kutoa mawazo yao kwa uhuru na kujadili hoja mbalimbali kwa nia ya kukosoa au kutoa maoni. Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Mbunge hawezi kufunguliwa kesi ya madai au ya jinai kwa kauli yake au jambo alilolifanya Bungeni.

Baada ya kutoa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Hakuna sheria yoyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayompa kinga Mbunge nje ya eneo la Bunge.
- (b) Kutokana na dhana yenyewe ya kinga, wigo kwa Wabunge umelenga katika kuwalinda wakati wa kutekeleza majukumu yao wakiwa ndani ya Bunge. Wanapokuwa nje ya Bunge, ikiwa ni pamoja na kwenye Majimbo Wabunge, wanapaswa kutii sheria za nchi kwa kuwa wao wako sawa na watu wote mbele ya sheria kwa mujibu wa ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- (c) Kwa kuwa hakuna sheria yoyote inayoweka kinga kwa Wabunge nje ya maeneo ya Bunge, Sheria iliopo haipingani na sheria nyingine yoyote.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba Mbunge anatakiwa aheshimu sheria na taratibu nyingine anapokuwa nje ya Bunge. Je, anapokuwa ndani ya Bunge hastahiki kuheshimu Sheria na Katiba ya nchi?

Swali la pili, kwa kuwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Zanzibar ni sehemu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano; na kwa kuwa katika Sheria ya Kinga ya Baraza la Wawakilishi inawapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kinga nje ya Baraza la Wawakilishi na ndani ya Baraza la Wawakilishi; na kwa kuwa Mbunge wakati wake mwangi si tu ndani ya Bunge ni pamoja na nje ya Bunge haoni kuna umuhimu wa Wabunge nao kupata kinga kama ile wanayapata Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi? (*Makofî*)

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu suala la Wabunge kutoheshimu sheria ndani ya Bunge. Katiba inawapa uhuru wa kuweza kujadili mambo mbalimbali ndani ya Bunge, kuweza kuuliza maswali ndani ya Bunge, lakini iwapo Mbunge atakwenda kinyume na taratibu za Bunge basi inabidi achukuliwe hatua. Akimdhalilisha Spika, Mbunge yeoyote, akitoa maneno ya kashfa, akatoa *allegations* ambazo haziendani na taratibu za Bunge basi Mbunge yule atachukuliwa hatua zinazostahili. (*Makofî*)

Swali la pili, hapa tunazungumzia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ile ni Katiba ya Serikali ya Mapinduzi. Kwa hiyo, naomba unipe muda niweze kuwasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Serikali ya Zanzibar kuona ni vipi Katiba hizi mbili zinaweza kuwiana kwa suala hilo. (*Makofii*)

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kwa sasa ndani ya Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988 inampa Mbunge haki kwamba anapokuwa katika Jimbo lake mtu yeoyote asizue Mikutano ya Mbunge. Je, kwa kuwa hiyo ipo si ingesomwa tena na kutazama namna ya kuiboresha hii kuongeza vifungu vingine hasa tukizingatia wakati huu mgumu wa Vyama vya Siasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria Na. 3 ya Mwaka 1988 inayohusu Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa ikisomwa kwa pamoja inampatia Mheshimiwa Mbunge haki ya kufanya Mikutano katika jimbo lake la Uchaguzi. Lakini haki hiyo lazima pia isomwe na sheria nyingine, Sheria ya Polisi ambayo sasa inaweka utaratibu wa namna ya kufanya Mikutano yake.

Mheshimiwa Spika, lakini niongeze tu kusema kwamba sasa hivi Serikali inaifanyia mapitio hii Sheria ya Haki na Kinga za Bunge ili tuone namna ya kuiboresha ili iende na wakati tulionao. (*Makofii*)

Na. 363

#### **Vikundi Vya Sanaa vya Uigizaji**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa vikundi vya sanaa vya Uigizaji katika *Television* hasa vya Kitanzania huifunza jamii yetu maadili ya Kitanzania na kuburudisha; na kwa kuwa vikundi hivyo hufanya maigizo yake kwa lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka kwa Watanzania wengi na mfano mzuri ni Kikundi cha Sanaa cha *Chemchem Art Group* maarufu kwa jina la Kidedea ambacho kinarusha maigizo yake kwenye kituo cha *ITV* tangu mwaka 2000:-

(a) Je, haki ya Hati miliki na malipo kutoka *ITV* kwa igizo lao la Jirekebishe na Kizazaar linaloendelea kurushwa na *ITV* ikoje na Mikataba wao wa *ITV* ukoje, ulianza lini na umetekelvezwa vipi; na je, kuna malalamiko ya aina yoyote?

(b) Je, ni haki kwa Kikundi cha Kitanzania kuzuiwa kutumia mivao ya kidini pale inapolazimu kutoa ujumbe uliokusudiwa kwa jamii?

(c) Je, mkanda wa igizo la Jirekebishe utaruhusiwa kuanza kuuzwa lini na utakuwa na miliki ya nani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mikataba inayohusu wasanii ikiwa ni pamoja na malipo ya usanii ni kati ya vikundi vya usanii wenyewe na vyombo vya urushaji husika na wala haishirikishi Serikali. Kwa misingi hii, aina, chanzo na utekelezaji wa igizo la Jirekebishe na Kizaaza havijulikani rasmi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mahusiano ya mikataba ni wa pande mbili zinazohusika na hapa ni *ITV* na vikundi husika. Serikali haiwajibiki wala kuhusika katika Mikataba hiyo. Kwa hiyo, haipaswi kujua au kushughulika na Mikataba husika.

Kuhusu malalamiko ya kikundi cha Sanaa cha *Chemchem Art Group*, Wizara haijapokea malalamiko rasmi. Hata hivyo, Chama cha Haki Miliki Tanzania (*COSOTA*) ambacho kinasaidiwa kwa muda na Serikali, kimefanya mawasiliano na *ITV* na *Chemchem Art Group* kwa lengo la kuona ni jinsi gani *COSOTA* inaweza kusaidia katika suala hili.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya kutumia mivao ya kidini wakati wa kutoa ujumbe kwa jamii, hili linategemea mambo mawili. Kwanza ni mdhamini anayetoa ujumbe anataka nini. Mdhamin ana haki ya kuamua mtoaji ujumbe avae nini. Pili, ni jinsi gani walengwa wataupokea ujumbe husika.

Hata hivyo, ni vema kutambua kuwa ipo hatari ya kwamba unapotumia mavazi ambayo yanawakilisha imani fulani katika kutoa ujumbe inaweza kuchukuliwa kama wenyi imani hiyo ndivyo walivyo kama inavyoonyesha kwenye ujumbe. Ujumbe ukiwa unaelezea mambo maovu wenyi imani wanaweza kuchukia na kuleta mfarakano. Hivyo, suala la kutumia mivao ya kidini kwa kutoa ujumbe linahitaji uangalifu na makini.

(c) Suala la mkanda wa igizo la Jirekebishe kwamba utaanza kuuzwa lini ni kati ya *ITV* na vikundi husika vya uigizaji. Mikataba kati yao ndio inaweza kuweka siku ya kuanza kuuza mkanda huo. Serikali hahisiki kabisa na wala hajibiki na maamuzi ya namna hii.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa *ITV* ni mali ya Mtanzania mzalendo na kikundi cha *Chemchem Art Group* (Kidedea) pia ni cha Watanzania, lakini mmiliki wa *ITV* anajaribu kuwasumbua na kuwashangaisha wenzake, Watanzania hawa na kukumbatia vipindi vya nje kama vile *Passions* pamoja na *Isidingo* ambavyo havieleweki kwa Watanzania. Je, Serikali inaweza kumuelimisha mmiliki wa *ITV* ili awe na uzalendo zaidi na kuwajali Watanzania wenzake kuliko kuwajali watu wa nje? (*Makofî*)

(b) Kwa kuwa mmiliki wa *ITV* anajaribu kuwadhulumu maskini wanaohangaika kutafuta riziki zao wakati yeze ana fedha nyinyi za kutosha kuliko hao wahangaikaji. Je, Serikali haioni kuwa endapo *Chemchem Art Group* watakuwa wamepeleka suala hili mahakamani bado haki haitawenza kutendeka na je, Serikali inaondoaje mashaka kuhusu suala hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tumekwishesiliana na *ITV* na tulifanya kikao tarehe 2 Oktoba, 2002. Kitu cha kwanza ni kwamba, walisikitishwa sana na hali iliyojitokeza ya wao kutolewana katika mkataba wao wa malipo na kikundi cha Chemchem. Pia, walisikitika kufikishana hapo kikundi cha Watanzania wenzao na wazalendo kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Walichokifanya ni kwamba, wamepeleka ule mkataba kwa Wakili ili waweze kuupitia tena kipengele hadi kipengele kuona ni wapi ambapo hawakuelewana.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tulijaribu kuwaonyesha kuwa kuna umuhimu wa kuvipa upendeleo maalum vikundi vya Watanzania kwa sababu vinatengenezwa kwa Kiswahili na Watanzania wengi wanaelewa Kiswahili na tukatoa mfano wa kikundi kilichokuwa kinaigiza kutoka Kenya cha Masakuu ambacho kilikuwa kinapendwa na Watanzania wengi sana na walikubaliana na sisi japo hawajibiki kufuata tunayowaambia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa tena nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuwa, haki ni lazima itatendeka. Jukumu la *COSOTA* ni kulinda na kukuza hakimiliki, kukadiria, kukusanya na kugawa mrahaba. Kwa hiyo, tutakapoenda mahakamani ambapo ndio tumewashauri waende huko, Serikali itasimama kumtetea mwenye kikundi kwa sababu ndio wajibu wetu. (*Makofî*)

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa katika swali la nyongeza Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba mwenye *ITV* ana hela nyinyi na anawadhlumu, lakini hakufafanua anawadhlumu vipi na kwa kuwa kipindi hiki cha

Maswali na Majibu Bungeni, kinasikika nchi nzima. Je, si vizuri kusahihisha kwamba hawadhulumu, isipokuwa kuna utaratibu ambao ilibidi uangaliwe? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo halielekezwi kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nadhani hakuna mwenye kuweza kulijibu.

Na. 364

### **Kuhusu Mashirika yanayoagiza Chakula**

#### **MHE. MARIAM SALUM MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshachukua tahadhari ya kutosha Wananchi wake hawaathiriki na njaa ya chakula:-

(a) Je, mpaka sasa ni Mashirika mangapi yaliyoruhusiwa kuagiza chakula na kiasi gani mpaka sasa kimeagizwa?

(b) Je, udhibiti wa bei hasa kwa walaji utakuwaje au utakuwa wa soko huru?

#### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki; Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu wa chakula unaoikabili nchi yetu, Serikali imefanya mazungumzo na Makampuni 13 ili yaagize chakula kutoka nje. Makampuni hayo yameahidi kuagiza mahindi tani 210,000, mchele tani 165,000 na ngano tani 278,100. Kati ya Januari na Julai, 2003 Makampuni hayo yaliomba na kupewa vibali vya kuagiza tani 41,000 za mahindi, tani 23,268 za mchele na tani 278,100 za ngano.

(b) Mheshimiwa Spika, bei za kuuzia vyakula hapa nchini hutegemea nguvu ya soko. Serikali haiwapangii bei wafanyabiashara kwa kuwa hatua hiyo inakiuka sera ya soko huru tuliyojiwekea. Hata hivyo, Serikali imetoa vivutio kwa wafanyabiashara ili waagize chakula kingi na kukiiza kwa bei nafuu.

Aidha, Serikali inafuutilia bei na hali ya upatikanaji wa chakula nchi nzima ili kuhakikisha chakula cha kutosha kinapatikana kwenye maeneo yenye upungufu kwa wakati na kwa bei nafuu. Bei za vyakula zitakapopanda sana, Serikali itaruhusu mahindi ya SGR kuuzwa kwenye soko.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, sasa hivi Makampuni mengi yameshaagiza chakula kutoka nje na kwa kuwa inavyoonekana sasa hivi ni kwamba, Vijiji vingi viko katika hali mbaya ya chakula; je, ni lini chakula hiki kitaanza kugawiwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Kampuni moja imeshaingiza mahindi tani 750 na ilipeleka chakula hicho Mikoa ya Lindi na Mtwara na vyakula vingine vingi vitaanza kuingia mwezi huu wa nane ulioanza leo. Kwa hiyo, tunaomba subira. Lakini vile vile, hapo katikati tulipata msaada wa mchele kutoka Japan tani 20,000 na zimeshatawanywa nchini kote. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu ya nyongeza kwa swalii la Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, alikuwa anazungumzia ugawaji wa chakula kwa watu walioathirika na njaa. Sasa, kama tulivyosema wakati tunajibu hoja za hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumetuma wataalam katika Mikoa yote kwenda tathmini.

Nafurahi kusema tathmini hiyo imekamilika na katika muda mfupi ujao Serikali itatangaza utaratibu wa kuwasaidia chakula wale wote ambao wamethibitishwa hawana uwezo kabisa na wameathirika na njaa katika nchi nzima ya Tanzania. Tathmini hiyo itatangazwa muda mfupi ujao. (*Makofsi*)

Na. 365

### **Mpira wa Pete kwa Wanaume**

#### **MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika majukumu makubwa ya Idara ya Michezo ni kusimamia ushiriki usiobagua jinsia na haki katika michezo, kama michezo ya jadi, mazoezi ya viungo kwa rika tofauti Vijana na Wazee:

- (a) Je, kuondoa tofauti hizo, mpira wa pete (*netball*) ya Wanaume utanza lini?
- (b) Je, kama utaanzishwa itaanzia ngazi gani?

#### **NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Nungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Chama cha Kusimamia Mchezo wa Netibali nchini (*CHANETA*) kimekwishatoa taarifa na kutangaza kwa wadau wote wa michezo huu kwamba Wanaume wanaweza kushiriki mchezo wa *netball*.

Mheshimiwa Spika, tangu Chama hiki kutoa taarifa hiyo miaka mitatu iliyopita ni timu chache za Wanaume zilizojitekeza. Timu ya JKT Mgulani ya Wanaume ndiyo iliyojisajili kwa Chama hicho na ilikwishapangiwa michezo ya majoribio wakati wa kuandaa Timu ya Taifa ya *Netball* ya Wanawake. Namwomba Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, ambaye michezo imo ndani ya damu yake, awahamasishé Viongozi wa Chama cha *Netball Zanzibar (CHANEZA)* ili kwa pamoja tufanikishe kuanzishwa kwa mashindano haya. (*Makofsi*)

(b) Endapo timu nyingi za Wanaume zitajitokeza kushiriki mchezo huu zitaanzia ngazi ya daraja la pili ili zile zitakazofanya vizuri ziweze kupanda daraja la kwanza.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Je, kuna utaratibu gani ambao Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo pamoja na Wizara ya Elimu na Utamaduni watatumia ili kuhakikisha kuwa huu michezo unaenea katika Shule za Msingi?

(b) Kuna sababu gani za kisayansi na za Kitanzania ambazo zimefanya michezo mingi hivi sasa ihamie Jeshini kuliko uraiani? (*Makofsi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kufanya juhudhi ya kueneza mchezo huu katika Shule zetu za Msingi, sisi ni wasimamizi wa sera, tunaendelea kushauriana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, ambao ndio wamiliki wa Shule za Msingi pamoja na wale wenye Shule binafsi

kuhakikisha kwamba siyo *netball* tu, lakini michezo mingine yote inatiliwa nguvu katika umri huo mchanga maana samaki hukunjwa akingali mbichi.

Kuhusu michezo kushamiri sana katika Majeshi yetu kuliko uraiani, siri kubwa ni nidhamu ambayo imo katika Majeshi yetu. Wana nidhamu katika usimamizi na wana nidhamu katika utawala wa michezo, lakini na wanamichezo wenyewe wana nidhamu ya kujituma tofauti na huko uraiani ambapo nidhamu imeelekezwa zaidi katika ubinafsi kuliko kusimamia michezo yenyewe. (*Makofsi/Kicheko*)

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Viongozi na Wanachama wa michezo mbalimbali ni lazima wajenge nidhamu kama anavyosema Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa suala la michezo duniani halipelekwi Mahakamani na kwa kuwa timu za Taifa zinashiriki mashindano ya Bara la Afrika; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atalielea nini Bunge hili na atachukua hatua gani kwa *FAT* kuhusu timu ya Mlandege kukosa kushiriki mashindano ya Kablu Bingwa Barani Afrika?

(b) Kwa nini *FAT* ilipeleka jina la Simba tu ilhali taratibu za *CAF* ni lazima ziwe timu tatu ikiwemo Mlandege ambayo ilikuwa ni namba mbili? (*Makofsi*)

**SPIKA:** Ni swali jipya, lakini pengine Mheshimiwa Naibu Waziri anayo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukiria kwamba dalili ya mvua ni mawingu. (*Kicheko*)

(a) Mheshimiwa Spika, suala la watu kwenda mahakamani ni haki ya msingi ya Kikatiba. Suala la michezo kutokupelekwa mahakamani haswa huo mpira wa miguu ni kanuni walizojivekea watu wa *FIFA*. Lakini kwa suala la Mlandege kutokwenda kuwakilisha nchi maadam walikuwa washindi kwamba Serikali inachukua hatua gani, kwa kweli Serikali kama msimamizi ilihakikisha kwamba *FAT* inajadili jambo hili kwa mujibu wa kanuni zao na *FAT* walichukua hatua. Hatua ambayo aliyechukuliwa alikwenda mahakamani na mahakama kumrejesha kwamba alifukuzwa au alisimamishwa uongozi kwa njia isiyostahiki.

Sasa, suala linapokuwa mahakamani si Bunge wala si Serikali inayoweza kuingiza mkono wake kwa mujibu wa Utawala wa Sheria.

(b) Kuhusu kuichukulia *FAT* hatua juu ya tatizo hili, nataka kusema kwamba *FAT* ni Chama huru kama vilivyo vilabu vyetu kwa mujibu wa sheria na ndio maana vimesajiliwa, wana taratibu zao.

Waheshimiwa Wabunge, ningombaa suala hili la Mlandege na JKT Ruvu, ambalo muda wake sasa umepita, kwa maana kwamba hakuna njia nyininge ya kuzishirikisha mle, tumwachie msajili wetu, tuiacie Wizara kwa ujumla iendelee kuwasiliana na *FAT* kujaribu kuhakikisha kwamba udhaifu wa aina hii haujitekezi tena badala ya kushughulikia jambo ambalo kwa kweli limekwishapita. (*Makofsi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuongezea majibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Said Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akitoa jibu la swali la msingi, alipokuwa akitofautisha kushamiri kwa michezo Jeshini na Uraiani, alisema tatizo kubwa ni nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunalo tatizo la nidhamu katika *FAT*. Kwa bahati mbaya zaidi ni kwamba baadhi ya Viongozi wasiokuwa na nidhamu katika *FAT* wanalelewa vile vile na baadhi ya Viongozi wa michezo kutoka Zanzibar.

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge ukatusaidie hasa kwa Makamu Mwenyekiti wa ZFA, Zanzibar aache kushabikia Viongozi wabovu katika FAT. (*Kicheko/Makof*)

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibiwa swali langu namba 366 naomba kufanya marekebisho madogo sana ya kimsingi.

Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Ussi Yahaya Haji siyo Ussi Yahya Haji. Baada ya marekebisho hayo naomba swali langu namba 366 lijibiwe. (*Kicheko*)

Na. 366

### **Kuanzishwa Vijiji kwa ajili ya Wazee**

**MHE. USSI YAHAYA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi inayoendelea na ina sera nzuri ya kuwahudumia Wananchi wake wakiwemo Wazee wasiojiweza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Vijiji Maalum kwenye kila Mkao (Tanzania Bara) kwa ajili ya wale Wazee wasiojiweza ili Serikali iweze kuwapatia huduma muhimu kwa urahisi kama vile matibabu, chakula, mavazi, malazi na kadhalika kama wanavyofanya wenzenzu kwenye nchi zilizoendelea?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, napenda kutoa maelezo yafuatayo: -

Serikali inatambua kwamba katika jamii yapo makundi ya watu amba o uwezo wao wa kujikimu umepungua au haupo kabisa. Kutokana na uelewa huo, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Na. 3 (Matunzo kwa watu wenye Ulemavu/Wasiojiweza) ya mwaka 1982 inayotoa nafasi kwa watu wasio na uwezo wa kujikimu kutunzwa na jamii.

Kutokana na maelekezo haya ya sheria hii, Serikali inaendesha makazi 17 ya watu wasio na uwezo na Wazee wakati Wakala wa Hiari zinaendesha makazi 24. Makazi haya yapo katika Mikoa ya Tanzania Bara (isipokuwa Iringa) na yanatoa huduma za msingi kama vile malazi, mavazi, chakula na matibabu. Makazi haya yanahudumia wastani wa watu 4000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, makazi haya yapo wazi kwa Wazee wote amba o hawana uwezo wa kujikimu na hawana ndugu au Taasisi ya kuwatunza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa huduma kwa Wazee wasio na uwezo, napenda kukiri kwamba matunzo yanayotolewa na Taasisi siyo nzuri na mara nyingi yanadhuru nafsi ya mhudumiwa. Matunzo ya kitaasisi hudumaza upeo wa mtu kutenda, huendekeza upweke, hupunguza uhuru binafsi na huweka mipaka ambayo haipo katika maisha ya kawa idha katika jamii.

Kutokana na madhara haya, Wizara yangu kupitia Sera ya Taifa ya Wazee iliyopitishwa mwezi Septemba, 2002 imemelekeza kwamba matunzo kwenye makazi litakuwa kimbilio la mwisho baada ya kushindikana njia mbadala za matunzo. Matunzo timilifu yanapasa kutolewa kwenye jamii na familia ambazo ndizo zenye jukumu la msingi la kutoa matunzo kwa Wazee.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuanzisha Vijiji maalum katika kila Mkao wa Tanzania Bara kwa ajili ya kuwatunza Wazee wasiojiweza kama inavyofanyika katika nchi zilizoendelea. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Wakala za Hiari inaendesha makazi 41 Tanzania Bara ambayo

yanatoa matunzo kwa Wazee wasio na uwezo wa kujikimu na hawana ndugu wa kuwatunza. Pia, makazi hayo yanatoa matunzo kwa Wazee ambao kuishi kwao kwenye familia ni mzigo kwa familia hiyo au ni hatari kwa usalama wa Wazee wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maisha kwenye familia na jamii ni bora kuliko kwenye Taasisi, kumpelekea Mzee kwenye makazi litakuwa kimbilio la mwisho baada ya njia mbadala za matunzo kushindikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ussi ameridhika, lakini sikusikia vizuri masahihisho ya jina lako uliyoyafanya, naomba urudie.

**MHE. USSI YAHAYA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima mimi naitwa Ussi Yahaya Haji, siitwi Ussi Yahya Haji. (*Makofî*)

**SPIKA:** Sasa nimeelewa, ahsante.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba wapo Wazee majumbani ambao hawana msaada na kwa kuwa hao Wazee ni wengi na ni mzigo mkubwa; je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuwasaidia Wazee hawa ambao wako majumbani na hawako kwenye makazi aliyoyataja?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, wakati natoa jibu la swali la msingi nilizungumza kwamba, matunzo ya kitaasisi ni kimbilio la mwisho kwa sababu humtenga yule mwenye kusaidiwa katika Taasisi. Nia kubwa ya ni kuhakikisha kwamba jamii inaanika na kutambua wajibu wake wa kutunza Wazee wetu na sisi tunaelekeea huko kwenye uzee.

Kwa hiyo, ni vema kila jamii ikakumbuka wajibu wake kutunza Wazee wetu. Hata hivyo, sera hiyo ya Wazee niliyozungumzia hapa ambayo sasa inakwenda kwenye ngazi ya Makatibu Wakuu, lengo kubwa ni kuwaandaa vijana kuukabili uzee ili kuepuka uzee kutuvamia kama wengi wetu inavyotutokea. (*Makofî*)

Na. 367

#### **Upotevu wa Fedha na Vifaa vyta Serikali**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa Kamati za Bunge za Hesabu za Serikali (*PAC*) na Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) wanapokuwa wakikagua hesabu husika hukuta upotevu wa fedha na vifaa vyta Serikali na wakati mwingine malipo hewa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hilo mara linapobainika katika ngazi hiyo baada ya kusubiri mpaka watumishi wengine wapewe uhamisho au kufariki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kutokea kwa upotevu wa fedha au vifaa vyta Serikali hatua zifuatazo zinapaswa kufuatwa na ofisi inayohusika, kwa mujibu wa Sheria mpya ya Fedha ya mwaka 2001 na kama ilivyo katika Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 sehemu ya IV, katika Kanuni ya 22 yenye Kanuni ndogo ya (1) hadi (9).

Mheshimiwa Spika, Afisa Mhasibu anatakiwa kujaza fomu ya upotevu wa fedha au vifaa na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Nakala hupelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Wakati huo huo, Afisa Mhasibu anatakiwa kutoa taarifa ya tukio la upotevu huo Polisi na nakala ya taarifa hiyo pia aipeleke kwa Katibu Mkuu Hazina. Baada ya mtuhumiwa kufunguliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani, kumalizika kwa kesi yake kutategemea mambo yafuatayo:-

(a) Kama mtuhumiwa akipatikana na hatia, atahukumiwa kifungo. Katika hukumu, mahakama itamlazimisha mtuhumiwa kurejesha mali yote aliyoiba mara amalizapo kifungo chake.

(b) Kama uchunguzi wa kesi ukiendelea kwa muda mrefu bila kukamilika, kuna uwezekano wa uchunguzi huo kuzoroteshwa na matukio mbalimbali, kama vile mtuhumiwa kupewa uhamisho kwa mujibu wa taratibu za kazi yake, kupunguzwa kazini au kufariki dunia. Mwishowe kesi kama hizi hukosa ushahidi wa kutosha na jalada kulazimika kufungwa. Matokeo yake ni kwamba, mali zote zilizoibowi zinakuwa ni hasara kwa Serikali.

(c) Kama mtuhumiwa akishinda kesi na kuachiwa huru basi fedha na vifaa vyote vilivyopotea vinakuwa ni hasara kwa Serikali.

(d) Katika hali hiyo Serikali itawajibika moja kwa moja na upotevu huo na italazimika kuufuta kwenye hesabu za Serikali kuititia Mamlaka zinazohusika na kuidhinisha upotevu huo uliotokea. Zaidi sana Serikali itakachowea kufanya ni kuwajibisha kwa kuwachukulia hatua za kinidhamu na kiutawala Maafisa wote waliosababisha mianya iliyoleta upotevu wa mali hizo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Kwa kuwa upotevu huo hutokea kila mwaka na adhabu zinazotolewa hazilingani na upotevu huo na kwa kuwa fedha za Serikali zinatumika vibaya; je, Serikali haioni kuwa inatoa udanganyifu wa upotevu wa fedha wakati adhabu inayotolewa hailingani na upotevu huo wa fedha? (*Makofî*)

(b) Kwa kuwa Wananchi wanajua upotefu wa fedha hizi; je, Serikali haioni kwamba inapoteza imani kwa Wananchi wake? (*Makofî*)

#### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la adhabu hazilingani. Kama mtu ameshtakiwa bila shaka tunaamini kwamba mahakama inatoa adhabu kwa mujibu wa Sheria kama ilivytungwa na Bunge letu Tukufu.

Kama nilivyoeleza kwamba sababu nne ndio zinazotokea, lakini pale panapostahiki, mtu anapopata kifungo anaambiwa alipe fedha zile. Kwa hiyo, sidhani kwamba adhabu hiyo hailingani na kosa alilokwishafanya.

(b) Nakubali kwamba Wananchi pamoja na sisi Wabunge tunakosa imani tunapoona kwamba fedha zinapotea. Serikali inajua suala hili na ndio maana Sheria ya Fedha na Sheria ya Ununuzi wa Vifaa zimetungwa upya na Bunge letu hili.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi mbili zimetungwa upya mwaka 2001 ili kuhakikisha kwamba utaratibu mpya na kanuni ambazo zitalingana zimetungwa na pia kuhakikisha kwamba hakuna upotevu.

Kwa hiyo, tunahakikisha kwamba hili halitatokea na ndio sababu tunakuwa na sheria na kanuni mbalimbali ili kuhakikisha hakuna upotevu unaotokea siku za mbele.

## **Utalii katika Mkoa wa Kagera**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkoa wa Kagera kuna maeneo mbalimbali yenyewe uwezo wa kuvutia watalii kama vile mapango ya Mugana - Bwanjai yenyewe kuonyesha mambo ya kale na kumbukumbu mbalimbali za vya Kagera katika Tarafa ya Misenyi iliyokuwa kambi ya Wajerumani katika Kata ya Minziro na mambo mengine.

Je, Serikali inatambua kuwepo kwa maeneo hayo, kama inatambua, inafanya nini kutangaza maeneo hayo na kuendeleza utalii katika Mkoa wa Kagera?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU RAIS (MHE. ARCARDO D. NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, pamoja na masahihisho aliyoyafanya kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Mkoa wa Kagera una maeneo mbalimbali yenyewe uwezo wa kuvutia biashara ya utalii. Pamoja na maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yapo maeneo mengine kama Ziwa Victoria na fukwe zake, visiwa vizuri yva kuvutia, Milima ya Karagwe, mapori ya Wanyama ya Rumanyika, Ibanda, Biharamulo na Burigi. Aidha, historia ya wenyeji wa Mkoa huo na Tawala zao ni moja ya mambo ya kuvutia wageni wa ndani na nje ya nchi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na sekta binafsi Mkoani Kagera, wamekwishaanza shughuli za kuendeleza utalii Mkoani humo. Sekta binafsi wameanza kuboresha huduma za malazi kwa kujenga hoteli nzuri na za kisasa maeneo ya kambi za wageni na huduma za Wakala wa kusafirisha watalii. Shirika la Ndege binafsi limeongeza huduma zake Mkoani humo na hivyo kufanya mkoaa kufikika kirahisi. Serikali nayo inazidi kuboresha miundombinu hususan barabara pamoja na mawasiliano ili kuleta maendeleo Mkoani humo.

Mheshimiwa Spika, ujumbe wa bodi ya utalii ulitembelea Mkoa wa Kagere na mwezi Aprili, 2003 ili kujionea maendeleo ya sekta ya Utalii. Bodii ya Utalii itaendelea kuvitangaza vivutio yva utalii nchini katika soko la ndani na nje vikiwemo yva Mkoa wa Kagera na Mwanza ili kuongeza pato la wananchi kwa njia ya biashara ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kagera pamoja na sekta binafsi ili kuendeleza sekta ya utalii. Aidha, tutashirikiana na Mkoa ili kuandaa taarifa muhimu za kaitalii zitakazotumika kutangaza na kuendeleza utalii Mkoani humo.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa maeneo ya utalii ni vizuri kuyawakilisha *World Heritage Centre* ni hivyo kuweka kwenye orodha ya urithi wa Dunia. Je, Mheshimiwa Waziri atawahakikishia wana Kagera kwamba maeneo aliyoyatajaa yataorodheshwa na kufikishwa *World Heritage Centre* na hivyo kuwa kwenye orodha ya urithi wa duniani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MHE. ARCARDO NTAGAZWA (k.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kama ifuatavyo:-

Suala la eneo la utalii au eneo la kihistoria kuwekwa katika orodha ya kile kinachoitwa *World Heritage Centre* kuna utaratibu wake. Namshukuru kwa taarifa hii kwa sababu tunajua maeneo haya ya vivutio Wizara ya Maliasili na Utalii itafanya kufuatana na utaratibu ili kuona kama baadaye *World*

*Heritage Centre* tukikidhi vigezo vinavyotakiwa basi maeneo haya bila shaka yatawekwa katika orodha ya urithi wa Dunia. (*Makofî*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha.

Matangazo ya leo ni kama ifuatavyo, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba wajumbe wakutane saa 5.30 asubuhi hii chumba namba 56.

Mheshimiwa Paul Kimiti, Mwenyekiti wa Chama Hiari cha Idadi ya Watu na Maendeleo, anaomba nitangaze kuahirishwa kwa mkutano ambao ulipangwa ufanyike leo ambao utafanyika wiki ijayo. Semina ya kesho vile vile ilikuwa isimamiwe na Mheshimiwa mwenye dhamana ya Kuondoa Umaskini Waziri Edgar Maokola-Majogo, lakini ni mionganoni mwa wale walioruhusiwa kwenda Rufiji. Kwa hiyo, ameahirisha semina yake kwa sababu hatakuwepo. Kwa hiyo, hakutakuwa na semina. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho ni ratiba ya wiki ijayo, kuna mabadiliko kidogo ya ratiba ambayo mtaikuta kwenye *pigeonholes* kwa wale wanaokwenda naomba wachukue kwanza waondoke wakijua badiliko hilo. Ratiba ya wiki ijayo kuanzia Jumatatu.

Kuna shughuli za Kibajeti, ile Miswada inayohusu Bajeti na *Re-Allocation Warrant* na kadhalika. Halafu bado kuna Maazimio yanayohitaji kuridhiwa na Bunge hili yako manne, vile vile kuna taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje inatoa taarifa za kazi zilizofanywa na Wabunge wetu wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Najua tulikubaliana utaratibu wa namna hiyo. Kwa hiyo, hizo ndiyo kazi zitakazofanyika wiki ijayo ziko kwenye *pigeonholes* sasa. Naomba Waheshimiwa Wabunge, hasa wale wanaoondoka kwenda Rufiji wachukue ili waende wakijua. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2003/2003 Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, inayohusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongeza na shukrani zangu za dhati kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa hotuba yake nzuri ambayo imetoe dira ya majukumu ya Serikali yatakayotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba walizotoa ambazo zimetupa picha kamili ya uwezo wa Taifa letu kiuchumi, matatizo yanayolikabili pamoa na hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na hali hiyo kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, iliyojadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu tarehe 2 hadi 3 Juni, 2003. Ushauri uliotolewa na Kamati utaiwezesha Wizara yangu kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wapya waliopita katika chaguzi mbalimbali ndogo zilizofanyika nchini kote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu na ahadi zilizotolewa na Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2002/2003 na mipango itakayotekelezwa kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Idara ya Kazi ina majukumu ya kulinda, kutetea, kuimarisha na kuendeleza uhusiano mwema mahali pa kazi kwa kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi na kujenga mazingira mazuri na ukuzaji wa ajira nchini sehemu za kazi.

Katika mwaka 2002/2003 majukumu na ahadi zifuatazo zilitkelezwu.

Kamati Maalum (*Task Force*) ya wadau iliyoundwa kushughulikia marekebisho ya Sera na Sheria za kazi imefanya marekebisho katika sheria za ajira, sheria ya mahusiano kazini, vyama vya wafanyakazi, taasisi za soko la ajira na kuangalia taratibu za utatuvi wa migogoro ya kazi.

Wizara tayari imepokea taarifa ya awali ya marekebisho na rasimu ya sheria inatayarishwa ili iwasilishwe Serikalini baada ya mwaka huu. Pia Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii nchini imekamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri.

Wizara ilipokea migogoro 39 na kuipeleka Mahakama ya Kazi. Rufaa 127 zilitolewa uamu. Malalamiko 175 yalishughulikiwa na jumla ya shilingi 171,070,830 zililipwa kwa wadai. Mikataba ya hiari 453 ilifungwa na kati ya hiyo 59 imekamilishwa na kipelekwa Mahakama ya Kazi. Pia kaguzi za kazi 277 zilifanyika. Madai 458 ya fidia ya kuumia kazini yalipokelewa na wafanyakazi 324 walilipwa jumla ya shilingi 34,992,000. Vikao 32 vya Utatu vilifanyika kupitisha maombi ya vibali vya kazi kwa wageni.

Maombi 1,520 yalishughulikiwa na Idara ya Kazi na maombi 769 yalishughulikiwa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*Tanzania Investment Centre (TIC)*).

Katika kuendeleza vita dhidi ya utumikishwaji wa watoto kukomesha ajira mbaya ya watoto, Wizara ilizindua programu ya kukomesha utumikishwaji watoto katika kazi za hatari katika Wilaya 11 ambazo ni Urambo, Iramba, Kondo, Arusha Mjini, Simanjiro, Arumeru, Ilala, Temeke, Kinondoni, Mufindi na Iringa. Pia mafunzo ya utekelezaji wa programu ya kupambana na ajira ya mtoto yalitolewa kwa wadau na mipango ya utekelezaji iliandaliwa katika ngazi ya Wilaya. Uzoefu utakaopatikana katika Wilaya hizi utasaidia kutayarisha awamu nyingine ili Wilaya nyingine zifaidike na mpango huu.

Tumetoa warsha kwa wakaguzi wa Kazi, Vyama vya Wafanyakazi na Maofisa Kilimo kuhusu Mkataba wa *ILO* Na. 182 na Mkataba Na. 184 unaohusu (*Occupation Safety and Health in Agriculture*) ili kupanua uelewa wa wadau hao juu ya kazi za hatari kwa watoto na kufanya maandalizi ya kuufanya marekebisho mwongozo wa wakaguzi wa kazi kwa ajira ya watoto (*Child Labour Inspection Guide*).

Mheshimiwa Spika, Wizara inatekeleza mradi wa kuboresha na kuongeza Ajira ya Wanawake na kutokomeza ajira ya Watoto nchini. Mradi huu umeanza kutekelezwu katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mbeya. Katika awamu ya kwanza, jumla ya wanawake 571 wamehusishwa kwa kupatiwa mafunzo na mikopo. Watoto wapatao 449 wameibuliwa kutoka katika sehemu za mashambani, shughuli za mama lishe na shughuli za kugonga kokoto na kuandikishwa shule.

Kamati ya Taifa ya kusimamia utekelezaji wa mpango wa kupambana na ajira ya watoto (*National Inter-Sectoral Coordination Committee- NISCC*) iliunda Kamati ndogo ya elimu Novemba, 2002 li kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa mpango katika nyanja ya elimu.

Wizara iliendelea kutekeleza mradi wa kuondoa umasikini kwa kuchapa kijitabu chenye mafunzo juu ya utaratibu wa watu kuweza kujiajiri. Kazi ya kutambua na kubaini wanafunzi 120 watakaofundishwa kilimo na ufundi imefanyika kwa Halmashauri za Wilaya moja moja za Mikoa ya Arusha, Kagera, Lindi, Mtwara, Iringa na Mbeya. Aidha, Wizara inatekeleza mradi wa kuendesha mafunzo juu ya utafiti wa kuweza kujiajiri kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo haya yanawashirikisha wananchi na viongozi.

Katika mahusiano ya Kimataifa, Tanzania imehudhuria vikao vinavyohusu masuala ya kazi na Ajira vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Umoja wa Afrika (*AU*) na Mkutano wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Pia Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa *SADC* juu ya Kazi na Ajira ambaulifanyika Arusha tarehe 24 hadi 28 Machi, 2003 na kuhudhuriwa na nchi 9.

Katika kuendeleza kwa Utatu vita dhidi ya Ukimwi sehemu za kazi na kukamilisha Kanuni za Maadili (*Code of Conduct*) Idara ilipokea maoni na michango kutoka taasisi ambazo zinatekeleza mapambano juu ya janga hili ili Kamati ya Utatu ya kupambana na Ukimwi sehemu za kazi iweze kukamilisha kanuni hizo.

Katika Kituo cha Ajira (*Labour Exchange Centre*) ambacho kinawaunganisha waajiri na watu wanaotafuta kazi, jumla ya watafuta kazi 4,177 wamejiandikisha. Kati yao watafuta kazi 1,533 au 37% wameunganishwa na waajiri, kati ya hao watafuta kazi 87 au 6% wamepata ajira. Tangu kituo kianzishwe mwaka 2001, jumla ya watafuta kazi 7,069 wamesajiliwa, watafuta kazi 2,748 au 39% wameunganishwa na waajiri na 182 au asilimia 7% ya waliouunganishwa na waajiri wamepata ajira.

Kituo kilishiriki katika maonyesho ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba yaliyoanza tarehe 29 Juni, 2003 hadi 9 Julai, 2003 kwa kutangaza huduma za Kituo kwa waajiri na watafuta kazi wa ndani na nje ya nchi, hasa ndani ya Nchi za Afrika Mashariki.

Kuanzia mwaka 2003/2004 kituo kitatoa huduma kwa kutumia Mtandao wa Kompyuta (*Automative Services*). Ninawashauri waajiri wote walio katika sekta ya umma na ya binafsi wakitumie kituo hiki. Wakati huo huo kituo kimeanza kufanya utafiti juu ya nafasi za kazi zilizopo katika Jiji la Dar es Salaam (*Job Vacancy Survey*).

Mheshimiwa Spika, kituo kimetoa elimu kwa njia ya matangazo kwa waajiri na watafuta kazi ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha watu wengi kutumia huduma za kituo na pia kuwashirikisha wadau wa ajira kushiriki kikamilifu katika kuleta ufanisi wa shughuli za kituo.

Pia kituo kilikamilisha ripoti ya tafiti ambazo zilifanya tathmini ya athari za ajira kulingana na ukuaji wa sasa wa uchumi wa Taifa na Sera ya Uwekezaji.

Katika kuendeleza uongozi bora na demokrasia sehemu za kazi, Wizara imesimamia chaguzi za mabaraza ya wafanyakazi 13 kwa kushirikiana na waajiri na Vyama vya Wafanyakazi. Aidha, mafunzo kwa wafanyakazi yaliendeshwa kwa taasisi 8.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu ilifanya utafiti wa Nguvukazi (*Labour Force Survey*) mwaka 2000/2001. Uchambuzi na utayarishaji wa ripoti ulikamilika mwezi Aprili, 2003. Katika utafiti huu takwimu muhimu zinazohusu hali ya ajira, uchumi na ustawi wa jamii zimepatikana. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa Tanzania Bara ina nguvu kazi ipatayo watu 18,827,578. Kati ya hao 9,739,709 ni wanaume na wanawake 9,087,869. Idadi ya watu wasio na kazi ni 1,282,913. Kati ya hao wanaume ni 518,991 na wanawake 763,922.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 27 Februari, 2002, Tume ya Ulimwengu ya Utandawazi ilizinduliwa rasmi na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) nchini Uswisi na Waheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa wa Tanzania na Rais Tarja Halonen wa Finland, waliteuliwa kuongoza Tume hiyo kama Wenyeviti wenza (*Co-Chairs*).

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa sote tumekuwa tukifua tilia kwa karibu shughuli za Tume hii. Wizara yangu imeshiriki katika majadiliano mbalimbali yaliyoandaliwa na Tume ya Ulimwengu ya Utandawazi, kama vile majadiliano ya Kitaifa (*National Dialogue on Social Dimension of Globalization*) yaliyofanyika Dar es Saalam tarehe 19 hadi 20 Agosti, 2002 na majadiliano ya Kanda ya Afrika (*Africa Regional Dialogue*) yaliyofanyika Arusha tarehe 6 haadi 7 Februari, 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa hiyo fupi ya utekelezaji wa yale niliyahidi mwaka 2002/2003 chini ya Idara ya Kazi, naomba sasa nieleze yale ambayo yamepangwa kutelekezwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004 kama kuendeleza na hatua ya pili ya marekebisho ya Sera na Sheria za Kazi, kusimamia uundaji wa Bodi za Mishahara kwa sekta mbalimbali nchini kwa lengo la kutayarisha vima vya chini vya mishahara kulingana na uwezo na mapato ya sekta, kuendeleza shughuli za utekelezaji wa sheria za kazi ikiwa ni pamoja na kushughulikia malipo ya fidia, kaguzi, migogoro, malalamiko, mikataba ya hiari

na usimamizi wake kwenye vituo vya kazi nchi nzima, kushughulikia kikamilifu masuala ya kimataifa katika nyanja za kazi na ajira kwa utatu, kuendeleza vitia dhidi ya Ukimwi sehemu za kazi na kuendelea kukamilisha rasimu ya Kanuni ya Maadili (*Code of Conduct*), kuandaa mikakati ya kukomesha utumikishaji wa watoto ikiwa ni pamoja na kurekebisha mwongozo wa wakaguzi wa kazi katika kufanya kaguzi za ajira ya watoto, kuwapatia vitendea kazi wakaguzi wa kazi na waratibu wengine ili kurahisisha kazi za uratibu na utekelezaji wa mradi na kuandaa Vikao vya Kamati ya Taifa ya kuratibu utekelezaji wa programu ya kupambana na ajira ya watoto. Aidha, Kamati itatembelea Wilaya 11 zinazotekeleza mradi ili kufanya tathmini ya kiwango cha utekelezaji.

Pia kuandaa warsha kwa Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utumikishaji watoto katika kazi za hatari na Mikataba ya *ILO* inayopinga ajira kwa watoto (Mikataba Na. 182 na 184), kuandaa na kuendesha warsha katika Wilaya 11 kwa waratibu wa programu wa Wilaya juu ya kusimamia utekelezaji wa programu ya kupambana na ajira ya mtoto na kuandaa warsha moja kwa Chama cha Waajiri, Vyama vya Wafanyakazi na Wizara za Serikali (Kilimo na Chakula, Elimu na Utamaduni na Maendeleo ya Jamii na Jinsia na Watoto) juu ya athari za utumikishwaji watoto katika mashamba.

Mheshimiwa Spika, pia kuendeleza kukuza uwezo wa watumishi kitendaji ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao. Kuendelea kupambana na rushwa ili kudumisha Uongozi Bora na Utawala wa Sheria, kuendelea kuimarisha Utatu ili kuwzesha kutatua masuala yatakayojitokeza sehemu za kazi na kuendelea kusimamia uundaji wa uelimishaji wa vyombo vya ushirikishwaji hasa mabaraza ya wafanyakazi kwa kushirikiana na waajiri na Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka huu wa fedha Serikali imeanzisha Idara mpya ya Ajira nchini, chini ya Wizara yangu. Idara ina jukumu la kushughulikia masuala ya ajira hapa nchini na kupendekeza maeneo maalum ya kupewa kipaumbele katika kutekeleza mikakati ya kukuza ajira na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu ni kutoa changamoto ya kukuza ajira na kuwa na mfumo wa uratibu wa shughuli za ajira kwa kuhusisha wadau mbalimbali.

Katika kufanikisha hayo, Wizara itatumia Sheria ya Taifa ya Huduma za Ajira Na. 9 ya mwaka 1999 (*The National Employment Promotion Services Act*) na Sera ya Taifa ya Ajira ambayo kwa sasa inafanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Idara ya Ajira itatekeleza shughuli zifuatazo:-

Kuratibu utekelezaji wa programu na mikakati ya kukuza ajira nchini iliyozinduliwa tarehe 12 Aprili, 2003 kwa kushirikisha wadau wote, hususan Wizara na Idara mbalimbali za Serikali, Sekta Binafsi, Washiriki wa Utatu na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Asasi mbalimbali.

Pia kuratibu utekelezaji wa mikakati iliyopendekezwa katika Ripoti ya Tume ya Ulimwengu ya Utandawazi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali na wadau wengine, kuratibu mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili kutoa ajira zaidi, kuendeleza na kuboresha shughuli za huduma za kituo cha ajira kwa kuboresha vitendea kazi na kuwapatia watumishi wa kituo mafunzo ya kina kuhusu huduma kwa wateja na kuendelea kufanya utafiti wa kazi zilizopo katika Jiji la Dar es Salaam. Utafiti huu utatoo taarifa ya hali ya kazi zilizopo na utawasaidia wanafunzi, Vyuo watafuta kazi na Serikali wakati wa kuandaa Sera za Ajira zitakazosaidia kupata picha kamili ya soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii iliendelea kushughulikia Sera mbalimbali, Sheria, Miongozo na shughuli zinazohusu huduma za ustawi wa jamii. Katika mwaka 2002/2003 majukumu yafuatayo yalitekelezwa ikiwa ni pamoja na Sera ya Taifa ya Wazee ilikamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri, rasimu ya Sera ya Huduma kwa watu wenye ulemavu iko tayari na hivi karibuni itawasilishwa katika Baraza la Mawaziri na mwongozo wa Huduma za Majaribio kwa Maafisa Ustawi wa Jamii umeandaliwa kwa ushirikiano na wadau na kusambaza katika maeneo ya huduma, kama vile Mahakama, Magereza na Ofisi zote za Ustawi wa Jamii nchini.

Pia kudurusu mwongozo wa Kitaifa na mikakati ya malezi na matunzo kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (*National Policy Guidelines and Strategies for Care and Support of Most Vulnerable Children*). Kabla ya kufanya hivyo, Wizara ilifanya majaribio ya utekelezaji wa mwongozo huo kwa walezi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika Wilaya za Mufindi na Makete Mkoani Iringa.

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara yangu imezipitia upya Sheria za Familia na Watoto, watu wenye Ulemavu, Majaribio na Ujenzi wa Tabia, (*Cap. 247*) na Sheria ya Watoto na Vijana (*Cap. 13*), ili iendane na mazingira ya sasa ya kiuchumi na kijamii na Taifa letu, marekebisho ya tabia kwa watoto, vijana na watu wazima wanaopatikana na hatia Mahakamani, mafunzo ya Stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu ili waweze kuajiriwa au kujiajiri, kugharamia elimu ya watoto yatima wanaoishi katika makao na makazi ya wazee, kusuluhisha mifarakano katika familia ili watu waishi kwa amani na furaha na kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo, kutoa matunzo kwa wazee/wasiojiweza katika makazi na uboreshaji wa huduma katika makazi ya Wazee wasiojiweza, vyuo vya ufundi na stadi za kazi, Makao ya Watoto Yatima/Wenye shida, mahabusu za watoto na shule ya maadilisho iliyopo Irambo Mkoani Mbeya.

Pia kuhudumia wahitaji kwa kuwapatia misaada mbalimbali ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vyta kujimudu kwa watu wenye ulemavu, watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu na walioathirika na madawa ya kulevyta, kuendeleza mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu 435 katika Vyuo vya Ufundu vya Yombo, Chang'ombe, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Arnautoglo, Mirongo, Masiwani, Singida na Masasi.

Wizara yangu iliendelea kugharamia na kuhamasisha asasi mbalimbali na watu binafsi ili kugharamia elimu kwa watoto katika makazi ya wazee/wasiojiweza, mahabusu za watoto, shule ya maadilisho, watoto walio katika makao ya watoto yatima/wenye shida na wanaoishi katika mazingira magumu katika jamii.

Pia Wizara iliendelea kutoa huduma ya majoribio na ujenzi wa tabia. Jumla ya washitakiwa 6,898 waliokuwa wanakabiliwa na makosa mbalimbali ya jinai walishughulikiwa. Kati ya hao washitakiwa 988 waliamriwa na Mahakama kuwa chini ya uangalizi wa maaftisa Majaribio na Ujenzi wa Tabia. Watoto 2,133 waliokuwa wanakabiliwa na mashitaka mbalimbali ya jinai walihifadhiwa na kutunzwa kwenye mahabusu 5 za watoto. Aidha, watoto 37 walipewa huduma ya uadilishi katika shule ya maadilisho Irambo Mbeya.

Wizara iliendelea kuhudumia wazee/wasiojiweza 1,649 katika makazi 17 watoto wenye shida/yatima 120 katika makao ya Kurasini na akinamama 55 waliojifungua watoto zaidi wa wawili walipewa msaada wa malezi, pia Wizara iliendelea kutoa huduma za usuluhishi kwa familia zilizo katika mifarakano, kushughulikia mashauri ya ndoa, 6,559, mashauri 9,648 ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa na mashauri 5,386 ya matunzo ya familia yalishughulikiwa.

Kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Wizara imeendeleza zoezi lilowatambua watoto 15,015 waishio kaika mazingira magumu na kupanga mikakati ya kuwahudumia watoto hao mahali walipo katika Wilaya za Bagamoyo, Kisarawe, Magu, Karagwe, Makete na Musoma.

Kwa kushirikiana na Shirika la *Abbott Pharmaceutical and Laboratories* inaendelea kuandaa Warsha zinazohusu utumiaji wa mwongozo wa kuwahudumia watoto waishio kwenye makao. Aidha, Wizara imefanikiwa kuwahudumia watoto yatima mahali walipo kwa kuanzia katika Wilaya za Rungwe, Mbeya Mjini na Muheza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Wizara itaboresha huduma za Ustawi wa Jamii kwa kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara itaelimisha jamii na asasi mbalimbali kuhusu Sera ya Taifa ya Wazee, itakamilisha Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenye Ulemavu, itaandaa taratibu za kuiwezesha Serikali kuridhia taratibu za Umoja wa Mataifa kuhusu fursa na haki sawa kwa watu wenye

ulemavu (*United Nations Standard Rules on Equalization of Opportunities for people with disabilities*), itahamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwatambua na kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu, itaendelea kutoa mafunzo kwa wawezeshaji haki katika ngazi za Wilaya na jamii, itaendelea mikakati ya kitaifa ya huduma kwa watoto wanaoishi mitaani, itaboresha baraza la usuluhishi wa ndoa la kamishna wa ustawi wa jamii na itaandaa mikakati ya Kitaifa kuhusu malezi na maendeleza ya watoto walio katika mazingira magumu.

Pia Wizara itaendelea kutoa msaada kwa akinamama waliojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mara moja, watoto wanaozaliwa wameungana na akina mama wanaopata ulemavu wakati wa kujifungua.

Wizara itasimamia na kukagua vituo, vyuo vya malezi ya watoto na makao ya watoto ili kuhakikisha ubora wa huduma zitolewazo katika maeneo hayo.

Pia itaendeleza kutoa huduma za majaribio na ujenzi wa tabia kwa kuhamasisha wazazi, asasi mbalimbali na jamii kwa ujumla ili kuondoaa unyanyapaa dhidi ya watoto walio katika migogoro ya kisheria, kuchangia malezi bora na kuboresha huduma mbalimbali kama elimu, afya, malazi na kadhalika kwa watoto hao.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara itaendelea kushirikiana na wahisani wa nje na ndani katika kuboresha huduma kwa watoto walio katika mahabusu za watoto wa shule ya maadilisho kuititia mradi mdogo wa majaribio (*Pilot Project*) unaoteklezwa katika mahabusu ya watoto, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta mtazamo endelevu wa maendeleo ya vijana, Wizara yangu inaifanyia mapitio na marekebisho Sera ya Maendeleo ya Vijana kwa kuwashirikisha wadau ili kuweka mikakati ya kuleta maendeleo ya vijana. Mambo mengine muhimu yaliyofanywa mwaka 2002/2003 ni kama ifuatavyo:-

Utafiti wa kina wa vijiwe vya vijana kwa kuanzia na Mikoa ya Dar es Salaam na Tabora kwa lengo la kuvifanya vijiwe hivyo kuwa sehemu za uzalishaji mali na ajira kwa maendeleo ya vijana. Zoezi hili limeiwezesha Wizara kubainisha maeneo ya vijiwe na shughuli zinazofanyika huko, ilishiriki katika uzinduzi wa mtandao wa Taifa ya Ajira ya Vijana Duniani (*Youth Employment Summit YES 2002 - Tanzania Chapter*) uliofanyika Dar es Salaam tarehe 13 Desemba, 2002. Tanzania imekuwa chini ya kwanzu kuzindua mpango huu katika nchi za Afrika, imeendelea kuratibu mpango wa kubadilishana na vijana na nchi ya Japan. Katika utekelezaji wa mpango huu vijana 12 walipelekwa nchini Japan na vijana 12 walikwenda Japan kushiriki katika kuandaa programu ya vijana ya Dunia iliyojumuisha vijana kutoka Mataifa 12 na ilitoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana 30 wazalishaji mali kutoka mikoa ya Morogoro na Iringa na pia iliendesha warsha ya kuboresha mitaala ili ilingane na mabadiliko ya kitaalum yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Mpango wa Vijana wa Jumuiya ya Nchi za Madola, Wizara ilishiriki kwenye Mikutano ya Bodi ya Ushauri ya Kanda ya Afrika uliofanyika Nicosia - Cyprus na Mkutano wa Mawaziri ya Jumuiya ya Madola uliofanyika Gaborone - Botswana. Mikutano hii ililenga kuweka mikakati ya kuimarisha shughuli za vijana katika nchi wanachama. Aidha, kikundi cha *Nguvukazi Partners* kutoka Sengerema kulipata ushindi.

Pia imefanikisha Mbio za Mwenge wa Uhuru zilizoanzia Mjini Sumbawanga Mkoani Rukwa tarehe 2 Juni, 2002 na kufikia kilele chake Mkoani Tanga tarehe 14 Oktoba, 2002 zilizokwa na ujumbe wenye vipengele viwili vya Sensa kwa Maendeleo ya watu na vita dhidi ya Ukimwi kuepuka unyanyaparaa na ubaguzi. Jumla ya miradi 1,555 yenye thamani ya shilingi 29,186,386,981 ilizinduliwa au kuwekewa mawe na msingi.

Wizara iliendesha warsha ya kutathmini Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa Mikoa yote kuanzia tarehe 11 hadi 19 Novemba, 2002 huko Zanzibar. Lengo likiwa ni kuboresha Mbio ya Mwenge katika kuleta maendeleo, mshikamano, umoja na utulivu mionganoni mwa Watanzania.

Pia Wizara imeendelea kuratibu shughuli za wiki ya vijana, iliyojherehekewa Kitaifa huko Tanga kuanzia tarehe 8 hadi 14 Oktoba, 2002. Vijana, Mashirika na Makampuni mbalimbali kutoka ndani na nje

ya Mkoa Mkoa wa Tanga washiriki katika maonyesho ya bidhaa mbalimbali, sanaa za maonyesho, ufundi michezo na mijadala mbalimbali iliyolenga katika kuwahamasisha vijana na jumuiya kwa ujumla ili kushiriki katika shughuli za maendeleo na mapambano dhidi ya Ukimwi. Jumla ya vikundi zaidi ya 150 vilishiriki. Aidha, vijana 800 walijitokeza kupima Ukimwi kwa hiari yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikisha uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru ambazo zilianzia Mkoani Tabora tarehe 7 Juni, 2003, pia imegawa jumla ya shilingi 370,770, 780/= fedha za mikopo kutoka mfuko wa maendeleo ya vijana katika mikoa yote ikiwa ni wastani wa shilingi 3,089,777 kwa kila Halmashauri ya Wilaya na Manispaa.

Kwa kushirikiana na *UNICEF*, Wizara imeendesa Kongamano la Vijana kuhusu suala la ushiriki na ushirikishwaji katika maendeleo na kujenga mitandao mionganii mwao. Jumla ya vijana 145 wa kutoka Wilaya 11 walishiriki. Pia imeendesa warsha ya ukusanyaji takwimu kwa vijana kwa lengo la kuwashirikisha vijana katika kuleta maendeleo kuititia Mbio za Mwenge wa Uhuru. Vijana 30 na maafisa 10 kutoka Wilaya 10 walishiriki.

Kwa kushirikiana na mpango wa Taifa wa kudhibiti Ukimwi (*NACP*), Wizara ilishiriki kikamilifu katika maonyesho ya Kimataifa ya Sabasaba yaliyoanza tarehe 29 Juni, 2003 kwa lengo la kubadilishana uzoefu kuhusu mbinu mbalimbali za kupambana na Ukimwi na stadi za maisha.

Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja na Mataifa (*UNDP*) pamoja na wadau wengine, Wizara ilihudhuria maadhisho ya kutafakari juu ya ari na moyo wa kujitolea yaliyofanyika Mkoani Dar es Salaam tarehe 11 Desemba, 2002.

Pia Wizara ilishiriki katika mkutano wa kuzindua programu ya kukuza ajira kwa vijana ya miaka 10 uliofanyika huko Alexandria, Misri mwezi Septemba, 2002.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Wizara yangu inatarajia kuimarisha shughuli za vijana kwa kukamilisha marekebisho ya Sera ya Maendeleo ya Vijana, kuandaa na kuendesha mafunzo kwa vijana katika masuala ya uongozi, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya uzalishaji mali kwa lengo la kuboresha uzalishaji na hivyo kuongeza vipato kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuratibu shughuli mbalimbali za vijana kwa lengo la kufanya tathmini ya shughuli za maendeleo ya vijana ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa vijana na waratibu wa shughuli za vijana na kuandaa taarifa ya hali ya vijana nchini, kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru, Wiki ya Vijana pamoja na Sherehe za Kilele ambazo zinatarajiwaa kufanyika Mkoani Mwanza tarehe 14 Oktoba, 2003, kuratibu mpango wa ziara za vijana kati ya Tanzania na Canada ambapo vijana 9 wa Kitanzania watakwendwa Canada na vijana 9 wa Canada watakuja Tanzania na kuandaa na kutekeleza programu za elimu na malezi bora kwa vijana ikiwa ni pamoja na kuwafundisha vijana juu ya Stadi za maisha, stadi za kazi, athari na namna ya kupambana na magonjwa ya Ukimwi na yale ya ngono. Jukumu hili litatekelezwa kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali.

Pia kuhamasisha na kujadiliana na viongozi wa Wilaya kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu vijana likiwemo tatizo la ajira, malezi bora na kadhalika. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa katika kutoa mafunzo kwa Watendaji Wakuu wa shughuli za vijana, kutenga maeneo ya kazi kwa Vijana pamoja na kuwapatia mikopo nafuu, kufanya uchambuzi wa kina na hali ya vijana waliomo katika vijiwe katika Mkoa mingine minne. Wizara inatarajia kutekeleza mpango wa kudhibiti Ukimwi mahali pa kazi na vijana utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya Mradi wa (*Multisectoral Aids Project*).

Mheshimiwa Spika, pia Wizara kushiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Madola kuhusu ujasiliamali kwa vijana (*Enterpreneurship*).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu chini ya Idara ya Maendeleo ya Michezo inalo jukumu la kusimamia maendeleo ya michezo hapa nchini kulingana na Sera ya Taifa ya Michezo. Katika mwaka 2002/2003, Wizara imeteketeza yafuatayo:-

Iliendelea kuhamasisha Umma wa Tanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki mazoezi ya viungo nya mwili na michezo ili kuboresha afya zao, kuongeza umri wa kuishi na kujenga ari ya ushindani. Nampongeza Mheshimiwa Joel Bendera Mwenyekiti wa Baraza la Michezo Tanzania kwa kuifanya kazi hiyo vizuri sana hapa Bungeni. (*Makofit*)

Katika kuendeleza jitihada za ujenzi wa Uwanja wa Kisasa wa Michezo, zabuni za mshauri na msimamizi zilitangazwa na kumpatia *B.K.S Group (PTY) Limited of South Africa in Association with Co-Architecture of Tanzania*.

Wizara ilitoa elimu ya maambukizo ya Ukimwi kwa kupitia mafunzo ya Muongoarika (*Peer Educators*) kwa vijana kwa nia ya kuzuia kuenea kwa Ukimwi. Mafunzo yalitolewa Chalinze, Musoma na Chuo cha Michezo Malya, iliendesha mafunzo ya Uongozi, Utawala, Ualimu na Uamuzi wa Michezo kwa waendeshaji wa Michezo Tanzania Bara na Visiwani katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Imeendesha zoezi la upimaji wa afya za wanamichezo na wadau wengine katika Miji ya Zanzibar, Arusha na Mwanza. Ilisimamia marekebisho ya Katiba 225 za vyama mbalimbali vya michezo na ushirikiano wa michezo kati ya Tanzania na Jumuiya za Kimataifa uliimashwa kwa kushiriki mikutano, semina, kongamano na mashindano ya Kimataifa.

Pia kutoa mafunzo kwa Wasajili Wasaidizi juu ya uhamasishaji na uanzishaji wa shughuli za michezo hii ni katika kuunga mkono juhudzi za wananchi ili vikundi vyao vya michezo mbalimbali visajiliwe katika ngazi zote. Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya michezo ya jadi kwa kushirikiana na Chama cha Michezo ya Jadi cha Taifa. Aidha, Sheria na Kanuni za Michezo ya Bao, Mieleka, Kuvuta Kamba na Kulenga Shabaha kwa pinde na mishale zimeandalisti. Ukarabati wa baadhi ya majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya umekamilika pamoja na ununuvi wa Jenereta la Umeme.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliendelea kuhuishwa kwa kufanya mazoezi ya viungo kwa kupitia vyombo vya habari, majumba ya mazoezi na vilabu vya *jogging*. Mwongozo maalum kwa wale wanaotumia majumba ya mazoezi ultolewa na kufanyiwa kazi.

Tanzania iliendeleza uhusiano wa kimichezo na nchi za *SADC* katika mashindano ya Kimataifa. Pia Wizara ilivihimiza Vyama vya Taifa vya Michezo mbalimbali kulipa ada katika Vyama vya Kimataifa ili viweze kushiriki Mashindano ya Kimataifa.

Wizara iliendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za fedha za vyama na vilabu vya michezo mara kwa mara ili kuepuwa ufujaji wa pesa za umma. Mashindano ya Taifa ya watu wenyewe ulemavu wa akili yalifanyika Dar es Salaam. Wizara pia iliwawezesha watu wenyewe ulemavu kushiriki katika mashindano ya Kimataifa ya Olympiki Maalumu (*Special Olympics*) ambapo vijana wetu walipata medali 18 na kushika nafasi ya pili duniani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mabalozi kwa kukubali kucheza mechii ya kuchangia ushiriki wa vijana hao. Wizara vile vile iliendelea kufanya uchaguzi wa hesabu za fedha za vyama vya vilabu vya michezo (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004 Wizara itaendelea kuboresha na kuimashwa michezo nchini kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kusimamia Ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Kisasa ambao utajengwa kwenye eneo kati ya Chuo cha Ualimu Chang'ombe na sehemu ulipo uwanja wa Taifa sasa. Uwanja huu utakuwa na uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu, eneo la michezo ya ndani, eneo la sanaa (*Theatre*), eneo la chuo, viwanja vya mazoezi ya viungo, maeneo ya kuongelea na mazoezi ya mpira mbalimbali. Aidha, Uwanja wa Taifa kwa sasa pia utaboreshweli ilitoe huduma za ziada za michezo na sherehe za Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, pia kuhakikisha timu za Taifa zinashiriki mashindano ya Bara la Afrika huko Abuja Nigeria, kuendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya michezo kwa kiwango cha Kimataifa ili tuweze kutambua vipaji vya wanamichezo mbalimbali na kuviendeleza.

Pia wizara kuendelea kudurusu na kuzifanya marekebisho Katiba na Kanuni za Vyama na Vilabu vya Michezo ili vijiendeshe kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, kuendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kufundisha na kuchezea michezo kwa kuandaa mafunzo mbalimbali ya michezo na kuboresha miundombinu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo - Malya, kuinua huduma za Kinga na Tiba kwa wanamichezo kwa kuwafanya uchunguzi wa afya wachezaji na kutoa elimu kuhusu athari za kutumia madawa ya kuongeza nguvu katika michezo, kuandaa programu ya mazoezi kwa watu wenye mahitaji maalum na kuandaa mashindano mbalimbali kwa watu wenye ulemavu kwa jinsia na rika zote, kukuza na kuendeleza michezo ya jadi kwa kutoa mwongozo na jinsi ya kucheza michezo ya jadi na kufanya utafiti wa Sheria na kanuni za michezo hiyo na kuendeleza ushirikiano wa michezo kati ya Tanzania na Jumuiya za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ambalo ni moja ya Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, litaendelea na majukumu yake ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kulipa mafao kwa wanachama. Aidha, ili kuboresha mafao ya wanachama Shirika litaendelea kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama vile dhamana za Serikali na Mabenki, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*) na katika ujenzi wa Ofisi na nyumba za kupangisha au kuuza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Shirika lilikusanya kiasi cha shilingi milioni 132,008 kutoka kwenye vyano vyake mbalimbali hadi mwezi Mei, 2003. Kiasi hiki ni asilimia 102.9% ya lengo la kukusanya shilingi milioni 128,197.4 katika kipindi hicho, limelipa mafao ya wanachama jumla ya shilingi milioni 16,477.9 kufikia kipindi cha mwezi Mei, 2003. Katika kuboresha mafao ya wanachama, Shirika lilianza kutoa fao la kuumia kazini kuanzia mwezi Oktoba, 2002.

Mheshimiwa Spika, pia Shirika limeshaanza kujenga nyumba 104 za gharama nafuu katika kiwanja cha Kinyerezi. Mradi huu unategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2003/2004. Shirika litaendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo mengine yatakayokidhi vigezo vya uwekezaji, liliendelea kuendesha semina mbalimbali na mafunzo ili kuwezesha wananchi kuuelewa mfumo mpya wa hifadhi ya jamii. Semina na mafunzo hayo yalitolewa kwa waajiri wa wanachama wa *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Shirika litakuwa katika kipindi cha mwaka wa pili wa mpango wake wa miaka mitano (*Five Years Corporate Plan*) ambao uliana kutumika kuanzia Julai, 2002. Mpango huu ndio dira ya Shirika katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai, 2002 hadi Juni, 2007. Katika mwaka 2003/2004, Shirika linakusidia kukusanya jumla ya shilingi milioni 156,656.4 kutoka vyano vyake mbalimbali vya mapato ambavyo ni michango ya wanachama, mapato kutokana na vitega uchumi, vitega uchumi viliviyokomaa na mapato mengine. Shirika lnatarajia kutumia kiasi hicho hicho cha fedha kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo, Shirika litaendelea kutoa elimu kwa wanachama wake, waajiri na umma ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii na kukamilisha ukarabati wa jengo lililokuwa la *NASACO*, mradi ambao kwa sasa unajulikana kama (*NSSF Waterfront House*). Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2003.

Shirika linafanya tathmini ya uwezekano wa kujenga maduka kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo (*Industrial Park*) katika Manispaa ambazo vitega uchumi hivyo vitawenza kurudisha fedha iliyowekezwa na kuboresha mfuko. Pia Shirika litamalizia ujenzi wa nyumba za gharama nafuu huko Kinyerezi na pia litaendelea na mradi wa nyumba za bei nafuu katika maeneo mengine yatakayokidhi vigezo vya uwekezaji vya Shirika na litaendelea na tafiti katika Mikoa mbalimbali ili kuangalia uwezekano wa kupanua maeneo ya uwekezaji.

Shirika linatazama uwezekano wa kushiriki katika utekelezaji wa miradi mikubwa mbalimbali ya Kitaifa ikiwemo ile ya ujenzi wa madaraja. Tafiti zinaendelea kutathmini namna bora ya Shirika kushiriki katika miradi hii. Hii ni pamoja na kushiriki ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundisti (VETA) iliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 1 ya mwaka 1994 kwa lengo la kutoa, kuratibu, kusimamia na kuendeleza mafunzo ya Ufundisti hapa nchini. Mikakati inayotekelawa inalenga katika kufanya elimu na mafunzo ya ufundisti kuwa chombo cha kuleta maendeleo ya uchumi kwa jamii kwa kutoa stadi zinazochangia katika kuondoa umaskini, kupanua ajira na kuinua kiwango cha ufundisti stadi ili wahitimu waweze kushindana katika ulimwengu wa utandawazi. Kwa sasa VETA imewasilisha Wizarani mapendekezo ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Bunge Na. 1 ya mwaka 1994, imefanya mabadiliko katika Ikama (*Organization Structure*) na imeanzisha mfumo uitwao *Competence Based Education and Training (CBET)*, ili kutoa na kuratibu mafunzo na huduma bora zaidi kulingana na mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, VETA imekamilisha zoezi la kuangalia upya Sera ya Taifa ya Mafunzo ya Ufundisti nchini, Vyuo vya Ufundisti vya Mikumi na Songea vimeendelea kupanuliwa na kuboreshwa. Tayari karabati huu utaongeza idadi ya fani za mafunzo ya kodi ndefu na fupi, tayari ukarabati wa Chuo cha Arusha, Kagera, Musoma umekamilika. Aidha, walimu wa ufundisti stadi 200 na viongozi 50 watapatiwa mafunzo chini ya mraidi huu na Chuo kipywa cha Ufundisti cha Mkoa wa Kigoma kimeanza kujengwa Mjini Kigoma. Ujenzi unatarajiwaka kukamilika Desemba, 2004 na mafunzo yataanza kutolewa katika fani mbalimbali 18 tofauti kwa wanafunzi 400 wa kozi ndefu na 2000 wa kozi fupi kwa mwaka.

Kwa kushirikiana na Zanzibar jumla ya mafundi stadi 232 wa Zanzibar walifanya mitihani, kati yao 136 au asilimia 59 walifaulu. Mitihani hufanyika huko huko Zanzibar. Ushirikiano huu unaendelea kuboresha hasa katika maeneo ya utayarishaji wa mitaala, hususan utayarishaji wa *occupational standards*. Jumla ya watahiniwa 1,870 walifanya mitihani ya NABE, kati yao 1625 au asilimia 87 walifaulu na jumla ya watahiniwa 138 wa Zanzibar walifanya mitihani hiyo, kati yao 114 au asilimia 83 walifaulu.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Shirika la kuwashudumia wasioona (TSB) jumla ya watu 10 wenye ulemavu waliosajiliwa katika Vyuo vya Ufundisti walihitimia mitihani yao, ambapo vijana saba walipatiwa vitendea kazi na mitaji ili waweze kujiajiri. Jumla ya *occupational standards* 34 zipo tayari kwa matumizi na nyingine 20 zimo katika hatua mbalimbali za matayarisho. Kwa ujumla *occupational standards* 77 zinahitajika katika sekta za ujenzi, magari, umeme, hoteli na utalii, kilimo, madini, usafirishaji, uchapishaji na utengenezaji nguo na Wizara yangu imekamilisha rasimu ya marekebisho ya sera ya VETA ya mwaka 1994 na hivi sasa inaendelea kujadiliwa kwa mujibu wa utaratibu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, VETA imeendelea kushirikiana na ILO katika kuboresha mtaala wa ujasiliamali (*Entrepreneurship*). Jumla ya walimu wa walimu saba wa Tanzania walijumuika na wenzao kutoka Kenya na Uganda katika mafunzo yaliyoendeshwa na ILO. Lengo ni kutoa mafunzo kwa walimu 600 ambao wataweza kufundisha somo hilo ipasavyo, VETA imeendelea na mpango wa mafunzo na huduma za kupambana na Ukimwi kwenye vyuo vyote vya ufundisti stadi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/04, VETA imepanga kuendelea kukarabati na kupanua vyuo vya ufundisti stadi vya Mikumi na Songea ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa kwa vyuo vyote viliviyokarabatiwa na utoaji mafunzo maalum kwa wafanyakazi, kuanza matayarisho ya awali kwa ajili ya ukarabati na utanuzi wa vyuo vya ufundisti stadi vya Shinyanga, Singida, Mpanda, Tabora, Ulyankulu na ujenzi wa Chuo kipywa cha Hoteli na Utalii Arusha, kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundisti Standi cha Mkoa wa Kigoma, kuendelea kuweka mkazo katika kozi fupifupi ili kupanua nafasi za mafunzo maalum kwa vikundi katika sekta isiyo rasmi na kuendelea kuimarisha na kupanua mafunzo ya ufundisti stadi kwa wasichana katika kozi ndefu na fupi ili lengo la kufikia asilimia 35 ya wasichana katika Vyuo vya Ufundisti ifikapo Desemba 2004 lifikiwe.

Pia kuendelea kuboresha utoaji wa mafunzo kwa kuendeleza ukuzaji wa mitaala, mafunzo kwa walimu wa ufundisti stadi, vielelezo vya kufundishia (*learning materials*) na taratibu za usajili na ithibati ya

vyuo vya ufundi stadi, kuendelea kutekeleza na kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi chini ya mfumo mpya wa mafunzo unaolenga sekta isyo rasmi kwa kuwashirikisha wadau wengine, kuanzisha kitengo maalum cha mafunzo katika Chuo cha *VETA* Dodoma kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa ajili ya kuhudumia sekta ya nyama, kuanza kutekeleza awamu ya tatu ya mradi wa kuboresha mbinu za ukusanyaji na kutoa tafsiri ya mahitaji ya stadi katika soko la ajira na kuendelea kupanua, kuboresha na kutekeleza mpango wa mafunzo ya kupambana na Ukimwi kwenye vyuo vyote vya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la usalama na afya sehemu za kazi liliendelea kupewa uzito unaostahili ili kudumisha afya bora kwa wafanyakazi na mazingira yake na hatimaye kuongeza tija. Kutokana na hali hiyo, Bunge lako Tukufu katika kikao chake cha Februari, 2003 lilipitisha sheria mpya ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, ambayo inatarajiwu kuanza kutumika katika kipindi hiki cili kukazia na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia usalama na afya sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/03, *OSHA* imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jumla ya kaguzi 3,804 za kawaida (*General Work Place Inspections*) zilifanyika na ushauri stahili kutolewa. (*Makofi*)

Kaguzi 900 za zana mbalimbali zitumikazo viwandani (*Statutory Plant Inspections*) na kaguzi maalum 140 za umeme (*Special Electrical Inspections/Test*) zilifanyika. Jumla ya shilingi 127,000,000/= zilikusanywa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, *OSHA* imefanya kaguzi 1860 maalum za kisheria (*Plant Inspection, Electrical Testing, Industrial Hygiene Measurement and Medical Examinations*), kufanya kaguzi 4,300 za kawaida (*General Workplace Inspections*) katika maeneo mbalimbali ya kazi ili kutambua athari ziwapatazo wafanyakazi na kutoa ushauri unaostahili na kutoa mafunzo ya afya, usalama na mazingira ya kazi kwa njia mbalimbali ikiwemo redio na *television* kwa msaada wa *DANIDA*.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara yangu imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Vyama Huru vya Wafanyakazi na Waajiri Na. 10 ya Mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/03, Wizara imesajili Chama kimoja cha Wafanyakazi na hivyo kufanya idadi ya Vyama vya Wafanyakazi vilivyosajiliwa kufikia 16.

Mheshimiwa Spika, ingawa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri inahusika pia na kusajili. Muungano wa waajiri, hakuna chama chochote cha waajiri kilichosajiliwa chini ya Sheria hii hadi hivi sasa. Serikali inatoa wito kwa waajiri kutumia uhuru wao kusajili umoja wa waajiri ili majadiliano baina yao na Vyama vya Wafanyakazi yaimarike zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa ushauri nasaha kwa wafanyakazi wanaofika kuomba ushauri wa kuanzisha vyama vipyta. Wafanyakazi kutoka taasisi tano wamepatiwa ushauri. Aidha, Vyama vilivyopo vimeendelea kushauriwa kubadilika kiutendaji ili viweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi. Wizara yangu imefanya kaguzi 15 za Vyama vya Wafanyakazi vilivyokwisha kusajiliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro ili kujionea utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu itasimamia na kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na waajiri. Aidha, maombi ya usajili wa Vyama vipyta kwa pande zote yataendelea kupokelewa na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria inayohusika. Kaguzi za Vyama vya Wafanyakazi vilivyopo pamoja na matawi yake yaliyoko nchini, zitaendelea na itaendelea kuelimisha vyama kwa njia ya mikutano na semina ili kuwawezesha kurekebisha kasoro zilizopo pamoja na mbinu mpya za kuhamasisha wanachama ambao bado kujiunga na vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi Tanzania imeundwa kwa Sheria Na. 41 ya mwaka 1967, kama ilivyorekebishiwa kwa Sheria Na. 3 ya mwaka 1990 na Sheria Na. 2 ya mwaka 1993 mionganoni mwa

nyinginezo, hususan kwa ajili ya kushughulikia utoaji wa haki unaohusu mambo ya kikazi na kiajira katika maeneo makuu yafuatayo, kusikiliza na kuamua migogoro ya kikazi baina ya waajiri na wafanyakazi, kuandikisha Mikataba ya Hiari ya usuluhishi ya kiajira, kusajili malengo ya kazi na maombi ya Bonasi kwa wafanyakazi, kufanya uchunguzi kuhusu matatizo ya kiajira na kikazi yanayoletwa Mahakamani na kuyatolewa uamuvi na kutoa ushauri na maelekezo kwa Kamishna wa Kazi na Serikali kuhusu vima vya chini vya mishahara ya wafanyakazi na mambo mengine yanayofikishwa Mahakamani. Kutekeleza majukumu mengine yoyote kufuatana na matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Mahakama ya Kazi imepokea migogoro ya kikazi 39 na kati ya hiyo 14 imetolewa uamuvi, imepokea migogoro ya uchunguzi 106 na kati ya hiyo 45 imetolewa uamuvi, yametolewa maamuvi 11 kwa ajili ya maombi ya kukaza hukumu, mikataba ya hiari 59 ilifunguliwa kwa lengo la kuweka hali bora za utendaji kazi mahali pa kazi na kati ya hiyo Mikataba 41 ilisajiliwa na kutolewa tuzo, maombi ya marejesho yalikuwa 34 na kati ya hayo 11 yametolewa uamuvi na jumla ya mashauri 238 yalifunguliwa na kati ya hayo 122 yaliyotolewa tuzo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama imeendelea na juhudi zake za kusogeza upatikanaji wa haki karibu na wananchi walio wengi kwa kuendesha vikao vingi zaidi Mikoani na kwenye Ofisi za Kanda. Vikao vya Mahakama vimefanyika katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dodoma, Iringa na Tanga. Mahakama pia imefanya matayarisho ya ufunguzi wa Ofisi ya Kanda ya Kati Dodoma ambayo tayari yamekamilika baada ya kuifanya ukarabati sehemu ya jengo na Mahakama imeendelea kuwasilisha mapendekezo mbalimbali ya marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Kazi na Sheria nyingine za kazi kwenye vyombo vinavyohusika kama vile kwenye Tume ya kurekebisha sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Mahakama itaendelea kusogeza upatikanaji wa haki karibu na wananchi walio wengi kwa kuongeza kasi ya kufanya vikao Mikoani. Msisitizo mkubwa utaelekezwa katika kutafuta ofisi na kufungua ofisi ya Kanda mpya ya Mahakama ya Kazi katika Kanda ya Ziwa Mwanza na Mahakama ya Kazi itaendelea kuifanya marekebisho Sheria ya Mahakama ya Kazi ili kuboresha huduma za Mahakama kwa kuipa uwezo zaidi wa kiutendaji na wa kutoza malipo/ada kwa baadhi ya huduma.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia na kuratibu shughuli za kuboresha tija katika Taifa letu kupitia Shirika la Tija la Taifa (*NIP*). Katika kutimiza azma hii, shirika limetekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza ufanisi wake ikiwa ni pamoja na kuajiri wataalam na mabingwa katika maeneo mbalimbali ya uboreshaji tija sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya shirika ni kuendesha mafunzo ya uongozi, kufundisha mbinu na maarifa ya kuongeza tija kwa viongozi na watumishi wa Wizara za Serikali, Taasisi za Serikali, Makampuni ya Umma na ya watu binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuboresha maarifa na juhudi. Shirika pia linatoa huduma za ushauri unaolenga kuboresha tija sehemu za kazi. Aidha, shirika linafanya utafiti kuhusu masuala yote yanayohusiana na tija hapa Tanzania na kutumia matokeo ya tafiti hizo kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Shirika liliendesa mafunzo 40 ya yaliyopangwa ambayo yalihudhuriwa na washiriki 692 kati ya 800 waliotegemewa. Aidha, Shirika liliendelea kutoa huduma ya ushauri katika fani za miundo ya shirika, mifumo ya utumishi, mifumo ya mishahara, kanuni za utumishi na kanuni za matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Shirika litaendesa mafunzo 60 ya mbinu za maarifa ya kuboresha tija mahala pa kazi ambayo yanategemewa kuhudhuriwa na washiriki 900 na kwa kutambua umuhimu wa vita dhidi ya Ukimwi, Shirika litaendelea kuwaelimisha washiriki juu ya mbinu za kupambana na janga la Ukimwi.

Pia Shirika linategemea kuanza kuimarisha shughuli za utafiti wa tija kwa kutekeleza mapango wa Taifa wa kuboresha na kusimamia tija katika sekta za viwanda, huduma, kilimo na huduma ya umma. Shirika pia litafanya utafiti kuhusiana na madhara ya janga la Ukimwi kwenye tija sehemu za kazi na athari za rushwa kwa utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Shirika limeanza mtando wa ushirikiano na Taasisi nyingine za umma na binafsi ili kuboresha huduma zake.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.26 ya mwaka 1973. Sera ya Taasisi ni kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu na Vyeti katika fani za Ustawi wa Jamii (*Social Work*), Uongozi Kazi (*Labour Studies*) na Raslimali Watu (*Human Resources Management*). Taasisi pia hutoa ushauri wa kitaalam na kufanya tafiti mbali mbali hususani zinazolenga matatizo ya kijamii yakiwemo ya kikazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, baada ya mabadiliko kadhaa ya kijamii kutokea sehemu za kazi Taasisi imezindua mpango wake wa maendeleo ya miaka ya mitano 2002/2003 hadi 2006/2007. Kutokana na malengo yaliyomo ndani ya mpango huu, taasisi imeweza kuongeza wakurufunzi kutoka 232 mwaka 2001/2002 hadi 320 mwaka 2002/2003 na wanatarajiwa kuongezeka na kufikia 450 mwaka 2003/2004 na imeanza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika fani ya Ustawi wa Jamii (*Post Graduate Diploma in Social Work*) na Stashahada ya Juu katika Raslimali Watu (*Advanced Diploma in Human Resources*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Taasisi inatarajia kusajili wakurufunzi 175 wakiwemo 100 wa Stashahada ya Juu, 15 wa Uzamili na 60 wa Cheti katika fani zote tatu. Usajili huu utaifanya idadi ya Wakurufunzi kufikia 450 ikiwa ni ongezeko la Wakurufunzi 130 ukilinganisha na mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, kulingana na marekebisho yaliyofanywa na Bunge lako Tukufu katika Sheria Na.26 ya mwaka 1973, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, sasa inajulikana kwa Kiingereza kama (*Institute of Social Work*). Jina la Kiswahili linabakia kuwa Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.12 ya mwaka 1967 na marekebisho yake ya Sheria Na.6 ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Baraza la Michezo la Taifa, kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo vya Taifa limetekeleza na lilisimamia maandalizi na kufanikisha ushiriki wa Timu za Taifa za Michezo ya Ngumi, Judo, Riadha na Kunyanya Vitu vizito katika, mashindano ya Jumuiya za Madola yaliyofanyika Manchester, Uingereza Julai 25 hadi 18 Agosti, 2002 ambapo Mwanariadha Francis Naali aliipatia Tanzania medali ya dhahabu na John Yuda aliipatia medali ya fedha, lilihimiza, kueleza na kuwezesha Vyama kuunda timu za vijana ambapo Vyama vya Michezo vya TTTA, FAT, TAHA, TABA, vilindesha mashindano ya Taifa na kuunda Timu za Vijana walio chini ya umri wa miaka 20 na lilisimamia Mikutano ya uchaguzi wa Vyama vya TAVA, TOC, TCA na TABA. Timu ya Taifa ya mchezo wa Golf ilishiriki katika mashindano ya Afrika Mashariki huko Arusha na kunya kua ushindi wa kwanza.

Pia timu ya Taifa ya Vijana ya Mchezo wa Kriketi kwa upande wa wasichana ilipata ushindi wa kwanza katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika huko Nairobi, timu ya Taifa ya Mchezo wa Ngumi ilichukua ushindi wa kwanza katika mashindano ya Afrika Mashariki yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam na Wanawake walihamasishwa kushiriki katika michezo na kwa mara ya kwanza timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake ilishiriki mashindano ya Mataifa Huru ya Afrika na kufanikiwa kuitoa Timu ya Taifa ya Eritrea kabla ya kutolewa na Zimbabwe katika raundi ya pili.

Mheshimiwa Spika, Klabu ya Simba imeendelea kushiriki vema katika michuano ya Klabu Bingwa Barani Afrika na kufanikiwa kuingia hatua ya nane bora baada ya kuzifunga Timu za BDF ya Botswana, Santos ya Afrika Kusini na Zamelek ya Misri. Kuhusu timu ya Taifa ya Mpira wa Mikono ya Wanawake iliwakilisha vema Tanzania kwa kupata ushindi wa pili katika mashindano ya Kanda ya tano huko Addis Ababa, Ethiopia. Aidha, timu hiyo ya Wanawake ilitwaa ubingwa wa Afrika katika mashindano yaliyofanyika hapa Tanzania na Timu ya Taifa ya Wanaume kuwa mshindi wa pili. Wanariadha wetu waliendelea kupata ushindi katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa yaliyofanyika katika nchi za Japan, Ubelgiji, Ufaransa na Uingereza ambapo wanariadha saba walipata ushindi wa kwanza kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, aidha, Baraza liliwezesha wataalam wanne kupata mafunzo maalum ya michezo kwa walemaru huko Misri na Marekani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Baraza la Michezo la Taifa liliendelea kuendela kuwashamasisha wananchi kushiriki michezo ili kujenga afya zao ikiwa ni pamoja na kutumia michezo kutoa elimu ya mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kukamilisha kuhuisha Sheria ya BMT Na.12 ya 1967 na marekebisho yake katika Sheria Na.6 ya 1971, kusimamia maandalizi ya Timu ya Taifa kwa ajili ya mashindano ya michezo ya Nchi Huru za Afrika itakayofanyika Abuja, Nigeria Oktoba, 2003, kusimamamia uchaguzi wa Vyama vitano vya Taifa vya michezo mbalimbali, kuandaa mkakati wa Taifa wa maendeleo ya michezo kwa vijana. Kutoa elimu kwa Vyama vya Michezo vya Taifa na Kamati za Michezo za Wilaya na Mikoa juu ya wajibu wao, sheria na kanuni za Baraza, kuwashamasisha ushiriki wa wanawake katika michezo na kuwashamasisha watu wenye ulemarv kushiriki katika michezo.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, Serikali ipo katika hatua ya kutekeleza Sera ya Menejimenti na Ajira. Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi iliendelea na zoezi la kupanga upya safu za utendaji kazi kwa lengo la kuimarisha huduma katika sekta za Wizara.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu ilikuwa na watumishi 1,231. Ili kuimarisha maadili ya utumishi wa umma, mafunzo ya maadili yalitolewa kwa watumishi 1,039 kwa lengo la kupambana na rushwa na kuendeleza na kudumisha utawala bora. Hii ni sawa na asilimia 84.4 ya watumishi wote wa Wizara. mafunzo yametolewa kwa watumishi wa Makao Makuu ya Wizara, Ofisi za Mikoa na Wilaya, Vituo, Makao/Makazi ya wazee na wasiojiweza na Vyuo chini ya Wizara. Watumishi walio katika Mikoa 17 kati ya 21 wamehusika na mafunzo hayo. Aidha, jumla ya watumishi tisa wamechukuliwa hatua za nidhamu kwa ukiukaji wa maadili ya utumishi wa umma. Watumishi 180 walipandishwa vyeo na TUMEAJIRI na wengine 239 walipandishwa na KAMUS. Watumishi watatu ambao Mamlaka yao ni Mheshimiwa Rais, wamepandishwa vyeo. Wizara yangu ipo katika zoezi la kuajiri watumishi 114 kujaza nafasi wazi katika Idara zake.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia suala zima la ushirikishwaji wa wafanyakazi. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara imefanya Mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi kama ilivyo katika Mkataba. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na PSRC, Wizara ya Mipango na Ubinafishaji ilianda Semina ya Vyama vya Wafanyakazi chini ya Shirikisho lao (TUCTA) ili kujadili Sera na Mbinu za Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kwa kuzingatia ushirikishwaji wa wafanyakazi. Nawashukuru sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Ndugu John Rubambe, Mwenyekiti Mtendaji PSRC, Ndugu Margaret Sitta, Mwenyekiti wa TUCTA na Katibu Mkuu Ndugu Nestory Ngulla, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha Semina hiyo. Semina hiyo ilifunguliwa na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, tarehe 29 Juni, 2002 Mjini Morogoro. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo juu ya mbinu za kupambana na rushwa na kudumisha maadili ya utumishi. Aidha, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na kuboresha mfumo wa Menejimenti na utoaji huduma bora.

Mheshimiwa Spika, huduma zinazotolewa na Wizara hii zinamgusa kila mwananchi kwa njia moja au nyingine. Wizara iko tayari kupokea na kufanya kazi ushauri, maelezo na maoni watakayotoa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusaidiana katika kuboresha huduma hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya yote niliyoeleza katika hotuba hii, naomba niwashukuru wananchi wote wanaohudumiwa na Wizara hii kwa uvumilivu walioonyesha na kuelewa hali halisi ya Taifa lao. Napenda kuwashakikishia kuwa Serikali itaheshimu, italinda na kuendeleza juhudzi zake za kutoa huduma kwa wananchi wake kwa kadri ya uwezo wake na kwa uadilifu.

Napenda kwa namna ya pekee kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mbunge wa Mchinga, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa ushirikiano anaonipa, uchapakazi wake ulio makini na wenye uadilifu wa hali ya juu. Shukrani zangu pia ziwaendee Katibu Mkuu, Bwana Abubakar Rajabu, Wakuu wa Idara na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji

Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara na Bodi zao, ambao wameshirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Vile vile, naomba nimshukuru Mheshimiwa Joel Bendera, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa kwa ushirikiano na juhudhi zake za kuimarisha uongozi wa michezo nchini. Nawashukuru pia Viongozi Wakuu wa Vyama na Vilabu vya Michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nikushukuru wewe na Kamati mbalimbali za Bunge lako Tukufu hasa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mheshimiwa Sofia Simba, kwa ushauri na maelekezo walijotupatia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwashukuru washirika wetu wote ambao kwa namna mbalimbali wametuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa njia ya pekee naomba niwataje Wajumbe wa Bodi ya Ushauri wa Kazi (*Labour Advisory Board*), Shirikisho la Waajiri Tanzania (*ATE*) na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*) kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inatambua naitaendelea kutambua michango mbalimbali ya Wahisani ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yetu. Shukrani za dhati ziende kwa Serikali za nchi na Mashirika ya Kimataifa ya Denmark, Marekani, Japan, Sweden, Canada, Ujerumani na Finland, *ILO, UNDP, UNICEF, FES, Abbott Pharmaceutical and Laboratories, SIDE by SIDE* na Mashirika ya hapa nyumbani ambayo ni *EOTF, TTCL, TBL, OIL COM, Vodacom na Kahama Mining*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Urambo Magharibi kwa ushirikiano wao wanaonipa. Mazingira haya yananifanya niendelee kufanya kazi kwa amani na utulivu huku nikiendelea kuamini juu ya uimara wa mshikamano wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2003/2004, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 14,088,965,600/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo chini ya Fungu 65. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe kiasi cha shilingi 451,653,700/= chini ya Fungu 60 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Mahakama ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. HAROUB SAID MASOUD (k.n.y. MHE. SOPHIA M. SIMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2003 naomba kutoa taarifa ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha taarifa kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Michezo kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Aidha, namshukuru Mwenyekiti, kwa kunipa heshima ya kunichagua kuwasilisha taarifa hii kwa niaba yake.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa wazungumzaji waliopita na mimi nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wameshinda katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini kote Tanzania Bara na Visiwani na kisha kuapishwa katika Bunge lako Tukufu.

Aidha, napenda nimponeze Betty Mkwasa, kwa ushindi alioupata kwa kuwa Mtangazaji wa kwanza katika Afrika kuwa mbunifu mzuri katika kuandaa vipindi vyake vya kuelimisha jamii/umma kupitia *ITV* kuhusu masuala ya Ukimwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanakamati wenzangu napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mbunge, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Ustaadh, Mbunge na Naibu Waziri, vile vile Bwana Abubakar Rajabu, Katibu Mkuu na Wakurugenzi na wataalam wa Wizara hii kwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kisekta kwa mwaka uliopita 2002/2003 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2003/2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwataja Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo, Mheshimiwa Sophia Simba, Mwenyekiti, Mheshimiwa Haroub Masoud, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Jina Khatib Haji, Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame, Mheshimiwa Yussuf Juma Kombo, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Omar Mwenda, Mheshimiwa Cynthia Ngoye na Mheshimiwa Kisyeri Chambiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika Wajumbe hao ndio wale waliochaguliwa katika kipindi cha awali kabla ya uchaguzi mdogo uliofanyika Pemba na Tanzania Bara. Wajumbe hao uliwachagua kwa ujasiri kwa sababu walikuwa ndio wanaonesha umahiri wa kuwa Kamati hii ni Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia kwa sababu walikuwa Waheshimiwa Wabunge wanaume wanane na Waheshimiwa Wabunge wanawake walikuwa wanane. Lakini kwa bahati tuliongezwa Waheshimiwa Wabunge wengine wawili, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa na vile vile Mheshimiwa Mchande Salim Mchande. Kwa hiyo, sasa ina maana wawili watalia tu hao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo hapo tarehe 2 Mei, 2003 Jijini Dar es Salaam. Katika kutekeleza malengo yake Wizara ilizingatia Dira ya Taifa ya 2025. Sera ya Uchumi na Maendeleo, Ilani ya Uchaguzi na Mwelekeo wa Sera za CCM. Masuala muhimu yaliyotolewa maelezo ni pamoja na Dira ya Wizara, majukumu ya Wizara, utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2002/2003, maelezo kuhusu mapato na matumizi kwa kipindi kilichopita 2002/2003, mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji, kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2003/2004 na maombi ya fedha kwa mwa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, ilifanikiwa kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Kamati ya Kisekta ya Maendeleo ya Jamii mwaka uliopita. Wajumbe wa Kamati hii wamepokea utekelezaji wa maagizo uliofanywa na Wizara hasa katika zoezi la kuwapatia wahitimu wa *VETA* vifaa vya kuanzia kazi, vimeanza Chuo cha *VETA*, Mtwara. Jumla ya wahitimu 163 walipatiwa *tool kit* kulingana na fani zao. Vifaa hivyo viligharimu jumla ya shilingi 19,463,300/= ambazo ni michango ya wazazi na Chuo chenyewe.

Kuhusu ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *VETA* imeanzisha utaratibu wa kutoa mitihani kwa Taasisi mbalimbali huko Zanzibar. Katika mwaka 2002 jumla ya watahiniwa 232 walifanya mitihani ya Ufundji Stadi huko Zanzibar na watahiniwa 138 walifanya mitihani ya biashara. Uhusiano huu pia uko katika utayarishaji wa mitaala hususan *Training Standards* na vigezo vya kuthamini mafunzo ya Ufundji Stadi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuwa kutokana na ongezeko kubwa la watoto yatima ya wale wanaoishi katika mazingira magumu, Wizara iwe na utaratibu wa kuratibu idadi ya watoto hao kila mwaka. Wizara iwe na utaratibu wa kuratibu Taasisi ambazo zinagharamia elimu na malezi kwa watoto hao na taarifa yake itolewe kwenye Kamati.

Kamati inashauri, Watoto Yatima wapatiwe misaada wakiwa katika jamii badala ya kuwatenga kwa kuwaweka kwenye Vituo. *NGOs* zihamasishwe kuwatambua na kupeleka misaada kwa wale

wanaoishi na yatima hao. Halmashauri za Wilaya ziwajibike kwa malezi ya watoto hao ipasavyo na hivyo zitenge fungu maalum kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahabusu ya Watoto, Wizara ihakikishe kesi za watoto watukutu waliopo Mahabusu zinashughulikiwa na kumalizwa kwa haraka zaidi ili watoto hao waweze kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vinavyohudumia watu wenye Ulemavu, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo ishirikiane na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kuvihudumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hasa vinavyohusika na kutoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu kama Arnatouglo, Dar es Salaam.

Pia Serikali iwatazame walimu na watumishi wanaofanya kazi katika Vyuo vinavyohudumia walemauvu kama watu wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana na hivyo iangalie uwezekano wa kuwalipa malipo maalum na Vyuo vya walemauvu visaidiwe vifaa vya kufundisha pamoja na kuongezewa walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la michezo Wizara ishirikiane kwa karibu na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika kutenga maeneo ya michezo, makocha wa timu zetu za Tanzania wapelekwe nje ili kupata uzoefu zaidi.

Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha kuwa migogoro ya uongozi ndani ya *FAT* inamalizika. Aidha, Kamati inashauri Wizara kufuatilia kwa karibu zaidi suala la *FAT* kushindwa kuipeleka timu yetu Sudan.

Kamati inaelewa tosha kuwa matatizo yote ya *FAT* hayasababishwi na Serikali kwa mujibu wa kanuni na sheria za *FIFA*, bali matatizo yote hayo ni ubabe, ubinagsi, ukiritimba na Uongozi wa *FAT* unaonuka. Narejea tena. Ukiritimba na Uongozi wa *FAT* unaonuka, usio na uchungu kwa nchi na michezo. (*Makofî*)

Kamati inatoa tamko kuwa itasimamia kwa gharama yoyote ile ili kurejesha imani ya Watanzania wapenda michezo. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Michezo, Mungu Ibariki Kamati ili kuikomboa michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutembelea Vyuo vya *VETA*, Dar es Salaam na Mtwara na kuridhishwa na kazi zake, Kamati ilishauri Vyuo hivyo kuangalia uwezekano wa kuzipitia upya bei za vifaa vyao kwani wateja walilalamika bei hizo kuwa ni juu.

Mheshimiwa Spika, Wizara iendelee kuzihamasisha Halmashauri kutoa Mikopo hii lakini izingatie kuwapatia elimu juu ya namna ya kutumia mikopo hii ili iwe na manufaa kwa wakopaji.

Aidha, mikopo inayotolewa ilenge katika kuwasaidia vijana kuwekeza katika kilimo hasa wale walioko Vijiini.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kazi imekuwa na tatizo la upungufu wa wafanyakazi kwa muda mrefu sasa. Tunaishauri Serikali ilimalize tatizo hili ili Mahakama hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano na Kamati yangu, niliombwa kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mafungu yake yote kiasi cha shilingi 14,540,619,300/=. Katи ya hizo, shilingi 8,649,577,300/= zikiwa ni kwa mpango wa maendeleo na shilingi 5,891,042,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kusimamia ipasavyo utekelezaji wa shughuli zote zitakazoidhinishwa katika Bajeti hii kwa kuzingatia ushauri, maoni na mapendekezo tuliyoinisha katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote walioshiriki katika kupitia, kujadili na hatimaye kukamilisha uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Naibu Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Bwana Abubakar Rajabu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wakurugenzi na Wataalam wa Wizara hii, Wakurugenzi Wakuu na viongozi wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hii ikiwemo Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi (*VETA*), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Baraza la Michezo, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), Shirika la Tija (*NIP*) na Mahakama ya Kazi. Afisa Mwakilishi kutoka Wizara ya Fedha, Katibu wa Bunge Bwana Kipenka Msemembo Mussa na bila kumsahau Katibu wetu wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Bibi Angelina Sanga. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaunga mkono hoja hii ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

**SPIKA:** Wasemaji wanenye wa mwanzo ni Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Peter Kabisa na Mheshimiwa Salim Omar Ali. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, atoe maoni ya Kambi hiyo. (*Makofit*)

**MHE. KHALIFA MOHAMMED ISSA – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kutujalia sote uzima, pia mimi kuweza kusimama mbele yenu kuchangia machache.

Pili nakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Soika, kwa kunipa fursa hii adhimu ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) toleo la 2003. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo Kisiwani Pemba na Tanzania Bara. Sote kwa ujumla wetu tukumbuke kwamba, lililotuleta hapa ni kuwatumikia wananchi waliotuchagua kwa maslahi ya wapiga kura wetu na Taifa kwa jumla. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nami pia niwashukuru kwa dhati wananchi wote wa Jimbo la Mtambwe Kisiwani Pemba kwa kunichagua kwa kura nyingi mno, ili niwe Mbunge wao, kitendo hicho kwangu mimi ni deni kwao na ni dhamira yangu kulilipa inshaallah. Papo hapo nimshukru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Kamati ya Uongozi ya Kambi na Wanakambi wote wa Kambi ya Upinzani, kwa kuniwezesha kutayarisha na kufanikisha kutoa hotuba hii. Kwa hilo, nawapa ahsante sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naweza kuwa mchache wa fadhila, kama sikuwapongeza kwa dhati sana, Mheshimiwa Alhaji Profesa Juma Athuman Kapuya, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Naibu wake Mheshimiwa Ustaadh Mudhihir M. Mudhihir. Kwa ushirikiano wao wa kidugu kwangu, kwa kuniwezesha kukamilisha hotuba yangu hii. Naomba waendelee kuniwekeea wazi milango ya Ofisi zao ili isiwe taabu kwangu kwenda kubadilishana mawazo juu ya Wizara hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina maeneo makuu matatu yaani Idara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni kwa kila eneo, kwa hiyo, nitaanza na Idara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, nchi hii iliwhahi kuwa na misemo maarufu kama kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, afanye kazi. Misahafu inasema: “Asiyefanyakazi, asile.” Misemo na kauli hizi zinasisitiza umuhimu wa kazi. Kwa maana ya kisiasa, ajira inasisitizwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya vijana kwa kiasi kikubwa yanategemea kazi. Bila kazi yaani ajira, basi maendeleo ya vijana yatakuwa kidogo au hakuna kabisa. Kama Serikali ambavyo imekuwa ikitisema, kuna kazi za kuajiri na kazi za kuajirini. Kazi za kuajiriwa zimepungua sana na hivyo kuleta tatizo la kijamii na hata hizo kazi za kuajirini hutegemea mtaji na kuwezeshwa.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa ajira ni kiashirio kikubwa cha umaskini. Kwa sababu ya umaskini, uchumi wa nchi yetu haujamudu kutoa fursa timilivu ya ajira kwa vijana wote wanaomaliza masomo katika Vyuo mbaimbali. Hali mbaya za maisha Vijijini, hasa ukosefu au upungufu wa huduma za jamii husababishwa vijana kukimbilia Mijini na wafikapo Mijini hawapati ajira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya vijana hawana ajira. Hali hii imeanza kuleta madhara makubwa kwa jamii kwa mfano, kuongezeka kwa Watoto wa Mitaani wasiokuwa na Wazazi, zaidi ya hapo maovu mengi yanazidi kuongezeka Mitaani na Vijijini kama ulevi wa kupindukia, ubakaji, ulawiti, mauaji, uzinzi, ushoga na magonjwa mbalimba hasa yale ya zinaa kama Ukimwi, Kaswende na Kisonono.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa zaidi, kuna dalili na uwezekanao wa vijana wengi kutoona umuhimu wa kujiedeleza kimasomo baada ya kushuhudia wenzao waliopata elimu katika fani mbalimbali wanavyohangaika bila ajira. Baadhi ya Wazazi hawaoni sababu ya kupeleka watoto wao Shuleni na Vyoni baada ya kushuhudia watoto wa wazazi wenzao waliosoma na kupata Stashahada, Shahada na hata Shahada za Uzamili hawana kazi.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Wizara iwe makini na suala hili kuzuia madhara zaidi. Vijana wasio na kazi ni bomu ambalo linaweza kulipuka wakati wowote kwani vijana hawa huwa wamekata tamaa. Tusipokuwa makini, watu wasiokuwa na nia njema na nchi yetu wanaweza kuwatumia vijana hawa kuharibu amani na umoa ambavyo tumekuwa tukijivunia kwa muda mrefu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali kuititia Wizara hii na Halmashauri za Wilaya kuongeza mikopo kwa makundi ya vijana ili waanzishe na kuendeleza miradi mbalimbali kama ya uvuvi, kilimo, sanaa, ufundi na ihakikishe inatoa elimu kwa vijana walipewa mikopo ili waweze kunufaika nayo. Taratibu za kupata leseni zirahishishwe ili kutozidi kuwakatisha tamaa vijana. Tusipofanya hivyo, Serikali itaendelea kutumia pesa na nguvu kwa kupambana na maovu niliyotaja hapo juu. Vijana wataendele kujiona kama viumbe vyaa pembezoni. Serikali imekuwa ikitoa kauli za kuwataka vijana kuajirini baada ya kumaliza masomo yao.

Suala hili ni zuri na lina nia nzuri lakini, kwa mfano, kijana aliyesomea mambo ya utawala au mahusiano ya kimataifa atajirini namna gani? Kuna haja ya Serikali kuititia Wizara hii kuiangalia upya kauli hii na kuitafsiri kulingana na fani mbalimbali za masomo. Kwa kijana aliyesoma masomo ya ufundi kama *VETA* anaweza kuajirini kama atawezeshwa tofauti na fani kama utawala, uongozi na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na madhara ya ukosefu wa kazi na umaskini, idadi ya watoto yatima inazidi kuongezeka. Bahati nzuri kuna asasi na Taasisi (*NGO*) mbalimbali zinazojitolea kutoa misaada kwa watoto yatima. Watoto hawa hukusanywa katika vituo maalum. Kwa kufanya hiyo, watoto hawa hukosa malezi ya kijamii na mwilingiano na watoto wenzao. Kwa hiyo, vijana hawa huzidi kujiona ni wapweke pamoja na nia nzuri ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, tunashauri na kusisitiza kuwa watoto hawa wabaki kwenye jamii na wasaidiwe wakiwa katika jamii. Misaada ipelekwe kwa ndugu, jamaa au marafiki wanaoishi nao baada ya kuwatambua. Serikali ishirikiane na Serikali za Vijiji na Mitaa kuhakikisha misaada hiyo inafanya kazi iliyokusudiwa na sio vinginevyo. Bila kufanya hivyo, misaada hiyo itatumika kinyume na makusudio.

Mheshimiwa Spika, kesi za watoto watukutu waliowekwa mahabusu zimekuwa zikichukua muda mrefu. Hali hii inazidi kuathiri watoto hao na hasa kuendelea kukosa masomo. Tunadhani tatizo hili linaendena pamoja na tatizo la upungufu mkubwa wa wafanyakazi wa Mahakama. Kesi za Watoto

Watukutu ni vizuri zimalizwe haraka iwezekanavyo ili waweze kuendelea na masomo. Tunaamini kuwa elimu inaweza kuwa dawa au suluhisho la utukutu hasa baada ya watoto hao kuelimika.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ijithahidi kumaliza tatizo la muda mrefu la upungufu wa wafanyakazi katika Mahakama ya kazi. Hali hii imekuwa ikiathiri wafanyakazi na waajiri wao kwa kusubiri maamuzi ya kesi zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza na kuishukuru *VETA* kwa kuanza kuwapa wahitimu wake vifaa vya kuanzia kazi. Hii ni hatua nzuri ya kupunguza ukosefu wa ajira kwani inasaidia vijana kujajiri wenywewe. Kamati ya maendeleo ya jamii iliambiwa kwamba kuna gharama za kupata vifaa hivi zinazotokana na michango ya wazazi na Chuo. Kwa kufanya hivyo, *VETA* inazidi kuwatwisha wazazi mzigo mzito licha ya umaskini mkubwa unaowakabili. Tunaishauri Wizara itoe mikopo ya vifaa kwa wahitimu, kisha wapangiwe muda na kiasi kitakachokuwa kinalipwa polepole. Kwa kufanya hivyo tutawasaidia vijana na kuwapunguzia wazazi mzigo wa michango. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *VETA* iangalie upya bei za vifaa vyao ambazo zinalalamikiwa kuwa ziko juu sana. Tunaishauri ipunguze bei za vifaa hivyo ili hata wananchi wenye kipato cha chini waweze kumudu kuvinunua. *VETA* ifikirie kipato halisi cha wananchi walio wengi ambacho ni kidogo sana. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya nguvu kazi inatokana na vijana. Kambi yetu inaungana na Wabunge ambaeo wamewahi kutoa ushauri katika Bunge hili kuwa Serikali kupitia Wizara hii ijenge Vyuo vya *VETA* kila Mkoa ili vijana wapate ujuzi na stadi za kujitegemea na kujajiri pindi watakapezeshwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara hii kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana ni kupanga, kuratibu na kusimamia ukimbizaji Mwenge nchini Kote. Mwenge umekuwa ukichukuliwa kama alama ya Kitifa inayochangia kudumisha umoja wa kitaifa. Vyombo vya habari kwa muda mrefu vimekuwa vikiripoti madhara yanayojitokeza katika mikesha ya Mbio za Mwenge. Kwa mfano, unywaji wa pombe wa kupindukia, vitendo vya ngono na kadhalika. Utafiti unaonyesha kuwa kila penye kulala Mwenge huzagaa mipira ya kiume (*condom*), je hali hii inaashiria nini? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iangalie kwa kina faida na hasara zinazotokana na Mbio za Mwenge kwa mazingira na wakati wa sasa. Pamoja na malengo mazuri ya kuanzisha Mbio za Mwenge, Serikali ifanye utafiti wa kina juu ya mwamko wa wananchi wa Mijini na Vijijini juu ya suala hilo. Pia sio vizuri kupuuzia madai kuwa pesa na michango inayokusanywa kipindi cha Mbio za Mwenge ama inawasaidia kidogo wananchi kimaendeleo au haileleweki inafanya kitu gani. Aidha, isimamie kwa ukaribu ili madhara yaliyotajwa awali yasiweze kutokea tena. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la tofauti kubwa ya mishahara katika Mashirika ya Umma, Idara na Wizara mbalimbali za Serikali. Sio kitu cha kushangaza kuona watu wawili au zaidi wenye sifa zile zile wanatofautiana kwa kiwango kikubwa sana. Suala hili hukatisha tamaa sana hasa kwa wale wafanyakazi wanaopata mishahara midogo. Pia sio ajabu, ukakuta wafanyakazi hao ndio wenye majukumu mengi na mazito, ukilinganisha na hao wanaopata fedha nyingi.

Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya utumishi iangalie suala hili kwa makini lisiwe linaendelea kutupunguzia ari na mori ya wafanyakazi wetu itakayopelekea kupunguza tija. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mazoea mazuri ya Wizara, Mashirika, Makapuni, Idara na kadhalika ya kutoa zawadi kwa Wafanyakazi Bora na Hodari katika sehemu mbalimbali za kazi. Pamoja na kuwa huu ni utaratibu na mazoea mazuri, kwa maana kwamba unategemewa kuboresha utendaji wa kazi, lakini kumekuwepo na manunguniko kutoka kwa wafanyakazi wa sehemu tofauti kuwa zawadi hizi hazitolewi kwa haki. Watendaji wazuri wamekuwa wakiachwa na kupewa watu wengine kwa sababu zinazofahamika na Waajiri.

Mheshimiwa Spika, suala hili linaweza kuwakatisha tamaa wafanyakazi wengine na kushusha uzalishaji mali. Kuondoa hali hii, wafanyakazi wote katika eneo husika wawe wanachagua wenywewe mfanyakazi au wafanyakazi kwa utaratibu watakaojipangia wenywewe. Hiyo ndiyo demokrasia hasa na

ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kufanya maamuzi. Bila kufanya hivyo, lazima malalamiko yataendelea kuwepo sehemu ya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, zoezi la ubinafsishaji linaanza kuwa na dosari nyingi, licha ya ajira kupendelea wageni kuna tatizo la kutokusikilizwa au kutokushirikishwa kwa wafanyakazi wachache wazawa wanaojiriwa. Mgomo wa wafanya kazi wa *NBC* siku chache zilizopita na jinsi wawekezaji walivyowatendea wafanyakazi hao ni ushahidi tosha. Tunaishauri Serikali iwaambie wawekezaji mambo matatu ya msingi.

Kwanza, wawaheshimu Watanzania kwa sababu sisi wenyewe pia tunaheshimiana na ndiyo asili yetu. (*Makofî*)

Pili, wawekezaji washirikishe wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali. (*Makofî*)

Tatu, wawekezaji waheshimu vyama vyaya wafanyakazi katika sehemu za kazi hata kama hawapendi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mambo yaliyotokea au yanayotokea *NBC*, *TTCL*, *TANESCO* na kadhalika yanatupa wasiwasi kuwa sasa tunaelekea katika ukoloni mamboleo uliofikia hatua ya juu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wawekezaji waambiwe lisiwe suala la wao kuamua wanavyotaka eti kwa sababu wamekuja na pesa yao, asili ya Tanzania ni kupendana, kuheshimiana, kusaidiana, amani, umoja, utu na kadhalika. Hatuna historia za ubaguzi kama wenzetu. Umaskini wetu usiwe kigezo cha kutunyanyasa. Waambiwe hivyo na watuelewe hivyo, kama mwekezaji hayawezi hayo, basi ameshindwa kazi afunge virago aende zake. Wasifanye mambo ya kutuvunjia amani na umoja wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya michezo. Suala lingine nyeti katika Wizara hii ni maendeleo ya michezo. Kabla ya kueleza mengi kwanza kabisa napenda kuitumia fursa hii kuipongeza sana timu ya Simba, kwa kututoa Watanzania katika aibu na kufanikiwa kushiriki katika Ligi ya Mabingwa Barani Afrika. (*Makofî*)

Timu hii imetuletea sifa kubwa Watanzania wote bila kujali ushabiki na ukereketwa. Pia tunamshukuru Mzee wetu Rais Mstaifu Alhaj Ali Hassan Mwinyi kwa kukubali kuipokea na kufuta kauli yake kuwa Tanzania ni kichwa cha mwendawazimu, kinachonyolewa na kila anayejifunza kunyoa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa jinsi walivyoshirikiana uongozi mzima wa Simba, wafadhili na wachezaji wote kuhakikisha mafanikio yanapatikana. Pia tunaziombea roho za Watanzania waliokufa katika mapokezi ya timu ya Simba. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema Peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 1995 ilitolewa Sera ya Michezo, ambayo ilisainiwa na Waziri wa Elimu na Utamaduni wakati ule, Profesa Philemon Sarungi, Sera imeainisha umuhimu wa michezo katika jamii ikiwa ni pamoja na kujenga tabia ya ushirikiano, upendo, udugu na uzalendo. Pia michezo hujenga uhusiano, uelewano na mshikamano wa Taifa. Michezo hujitambulisha na kulitangaza Taifa nje ya mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya madhumuni ya Sera hiyo ni kufafanua majukumu na kutoa mwongozo kwa vyombo mbalimbali vyaya michezo kama vile Baraza la Michezo la Taifa, Vyama vyaya Michezo na kadhalika. Pia sera ya mipango na malengo mengi ya kuendeleza michezo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha timu na wachezaji wetu wanafanya vizuri katika mashindano ya michezo ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Michezo la Taifa, lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1967 na marekebisho hayo ya sheria hiyo Na. 6 ya mwaka 1971. Chombo hiki ni moja ya vyombo vyenye jukumu la kutekeleza Sera ya Michezo. Vyombo vingine ni vyama vyaya michezo, Vilabu na mashirikisho ya michezo. Kazi ya BMT ni pamoja kuandaa utaratibu wa kujenga uhusiano wa kimichezo

kati ya vyama vya michezo na wachezaji wenyewe. Pia kuchambua, kuthibitisha ratiba za mashindano ya michezo zinazoandaliwa na vyama vya michezo vya Taifa. Ni jukumu la BMT kuhakikisha kuwa fedha za vyama na vilabu vya michezo vinakaguliwa na matumizi mabaya ya fedha yanaondolewa katika vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya michezo kwa ujumla katika nchi yetu kwa sasa hivi inasikitisha sana na kukatisha tamaa. Kambi ya Upinzani na wananchi kwa ujumla wangependa waelezwe wazi kama vyombo vyenye dhamana kusimamia michezo mbalimbali vimeshindwa kutimiza wajibu na majukumu yake au tatizo ni kuhofia vyombo la michezo la kimataifa. Vyombo hivyo ni Wizara hii, Baraza la Michezo la Taifa, vyama vya michezo, vilabu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, je Wizara hii pamoja na BMT wanajishughulisha vipi kupata uhakika kwamba wanaongoza michezo ni watu walio na sifa zinazokubalika? Je, viongozi wa michezo wana uthalam wa michezo wanayoongoza? Je, wana uzoefu wa kuongoza na wana taaluma za michezo? Je, viongozi wa vyama vya michezo na vilabu ni waaminifu? Wanaopenda haki na ni wa kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina jibu fupi kwa masuala yote hayo. Nalo ni hapana! Kiini cha matatizo yote ni utaratibu usiofaa wa jinsi ya kuwapata viongozi wenye sifa zinazotakiwa. Uwakilishi wa wananchi katika uchaguzi wa kupanda ngazi ni mdogo sana. Kwa hiyo, watu wachache wasio na sifa wana nafasi kubwa ya kuhujumu chaguzi mbalimbali hata kama hawana sifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uteuzi wa timu ya Taifa umekuwa ama haufuatwi, au haueleweki. Hii ni pamoja na malezi ya wachezaji wa timu ya Taifa. Huduma za wana michezo na kukuza ari ya kucheza na ufundi wa kuwatia hamasa ya kuzidi kupenda michezo zimekuwa mbovu kwa muda mrefu sana. Kwa mfano, huduma za afya, chakula, bima, posho ya kujikimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa mpira wa miguu una wapenzi wengi hapa nchini kuliko michezo mingine. Lakini pia ndiyo michezo unaoongoza kwa vurugu, migogoro, matokeo mabaya kuliko michezo mingine. Mambo haya yamekuwa yakiwasanoneshwu wapenda michezo na wananchi kwa ujumla. Soka kwetu imekuwa ni malumbano, kejeli, kesi Mahakamani. *FAT* kwa muda mrefu imekuwa ikiyumbishwa na viongozi wabovu na wasiotaka kufuata Kanuni na Sheria zilizopo. Hali ambayo imekifanya chama hiki kutokuwa na mwelekeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *FAT* inaongozwa na watu ambao ama wameshindwa kuheshimu Kanuni na Sheria za mpira au hawazijui kabisa. Na ndiyo maana vurugu haziwezi kumalizika ndani ya chama hiki. Sasa tunajiliza hali hii itaendelea hadi lini? Wananchi na wapenzi wa soka wamechoka na malumbano yanayosababishwa na uelewa mdogo wa Sheria na Kanuni za michezo kupigania maslahi binafsi, uchu na uroho wa madaraka na ugomvi usio na mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka iechezwe ni mikakati gani iliyopangwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kama chombo kikuu cha kusimamia michezo nchini na kuhakikisha migogoro inaisha. Suala la kuhofia kufungiwa na *FIFA* kwa hatua zitakazochukuliwa isiwe ndiyo sababu ya kuacha mambo yaende ovyo. *FIFA* lazima itambue kuna Serikali za nchi mbalimbali duniani. Sheria za *FIFA* zisikwamishe utekelezaji wa Sheria wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inawashauri viongozi wa vyama vya michezo na vilabu nchini kujenga utamaduni wa kujiuzulu mara moja kwa manufaa ya maendeleo ya michezo na wananchi kwa ujumla pale wanapoona mambo hayaendi vizuri, kauli kali na za vitisho kwenye vyombo vya habari ni ubabaishaji mtupu ambao hautusaidii. (*Makofi*)

Kwa kuanzia, tunaitaka Kamati nzima ya Utendaji ya *FAT* ijiuzulu mara moja. Kwa sababu hali ya soka nchini ni mbaya sana. Haiwezekani timu ya Taifa ishiriki mashindano ya Kimataifa ifungwe michezo yote. Pia timu hiyo, imeshindwa kusafiri kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha. Viongozi wote wa *FAT* waondoke mara moja kisha Wizara na BMT wasimamie marekebisho ya Katiba na Sheria za Vyama na Vilabu vya Michezo ili kupata uwakilishi wa kutosha. Baada ya hayo uchaguzi uitishwe haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo inahitaji sana uongozi bora katika Idara zote. Maendeleo ya vijana yanategemea sana ajira, vijana ndiyo Taifa la leo na kesho. Vijana hatutaki pembezoni. Tunaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuunda Wizara ya Michezo na Utamaduni inayojitegemea. Hatua hii itasaidia kunusuru hali duni na hafifu ya michezo nchini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Timu ya Michezo ya Bunge kwa kushiriki na kushinda michezo mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Joel Bendera na Wasaidizi wake naitakia kila la kheri. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshiriki *Five Kilometer Marathon Race* hapa Dodoma, siku ya Jumamosi tarehe 26 Julai, 2003. Hongera kubwa iwafikie wale walioongoza na kupata medali za aina zote na wale pia waliopata nafasi ya mwanzo kutoka mwisho. (*Makofî/Kicheko*)

Mwisho, ingawa siyo kwa umuhimu nawapongeza *Cargo Stars Limited* kwa kudhamini mashindano haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Michezo chini ya Uongozi thabiti wa Mheshimiwa Sophia Simba na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Said Masoud. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie machache katika Wizara hii muhimu sana katika jamii ya Watanzania.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri wanazofanya za kuendeleza michezo kujaribu kusuluhisha migogoro ya wafanyakazi na kuleta tija katika nchi hii. Pamoja na hayo napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niseme kuwa michezo ni muhimu sana kwa jamii na kwa mtu mmoja. Inajenga afya, inaongeza akili. Lakini vile vile michezo ni furah, inaimarisha udugu na mahusiano baina ya jamii.

Kwa hiyo, ningependa kutoa mwito kwa wananchi wengi wanamichezo, mashirika ya umma, makampuni binafsi na hata watu binafsi, wawe wanapenda kudhamini na kuendeleza michezo katika jamii. Huu ni wajibu wao, kizungu wanasema *Social Obligation*, kuwa katika jamii yoyote basi hata kuendeleza michezo katika eneo lile, ni wale ambaao waliweza. Wakiweza kuendeleza michezo katika mashule, wakiweza kuendeleza michezo katika mitaa ile wanayokaa, basi vipaji vinakuwa vimeibuka au vimeibuliwa na kunakuwa na maendeleo. Tusingoje kila wakati kutafuta wadhili kutoka nje kwenye masuala haya.

Pili, Mheshimiwa Spika, ni suala la kuimarisha michezo katika mashule yetu. Michezo katika mashule ni muhimu kwa sababu pale tuna-monitor vipaji vya vijana. Natoa mwito kuwa yale mashindano ambayo yalikuwa yanafanyika baina ya shule na shule, Mikoa na Mikoa na kitaifa yarudiwe au yarudishwe. Kwa sababu hii ndiyo itahakikisha kunakuwa na *continuity* ya maendeleo ya michezo yote na mashule yaimarishwe kwa kuwapatia vifaa vya michezo na walimu ambaao wana elimu na uzoefu mzuri katika michezo mbalimbali, *football, netball, basketball*, tenesi na kadhalika. (*Makofî*)

Vile vile ni vizuri *at least* katika kila Mkoa iwepo shule maalum ya kuendeleza vipaji vya wanamichezo. Hili suala ni muhimu kwa sababu kila mkoa kuna vipaji, sasa namna ya kuvijua vile vipaji ni lazima wakutanishwe na waonekane. Sasa hawawezi kuonekana. Sasa hawawezi kuonekana kama hakuna maandalizi ya kutosha na vile vile napendekeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iwe na Kitivo Maalum cha michezo au na Chuo Kikuu Kishiriki cha mambo ya michezo tu ili kuendeleza fani hii.

Mheshimiwa Spika, linaloambatana na hilo ni suala la uundaji wa timu ya Taifa. Juzi tumeona aibu iliyotufika Taifa letu kwa timu yetu kuboronga sana hasa ile ya mpira wa miguu na walifika mahali walikosa hata nauli ya kwenda mashindano ya kimataifa ya Afrika. Sasa hii inatokana na maandalizi duni. Lakini vile hata wale wachezaji wenye kutoptaka na namna wanavyotafutwa, wanavyopatikana, sasa hivi imekuwa tumejjengea tabia ya kuwatafuta kwenye vilabu. Zamani kulikuwa na mashindano ya kimko ambayo yalikuwa yanapata watu wenye vipaji kutoka katika kila Mkoa na Zanzibar wanatoka watu, Unguja, Pemba. Pale wanaweza kupata timu ya mchezo wowote. (*Makofsi*)

Kwa hiyo, natoa mwito kwa mashindano ya Taifa yarudishwe kwa sababu pale ndiyo kwenye wachezaji. Siyo wachezaji wote kwa kweli wanatoka Yanga, Simba, hapana! Wapo wachezaji wazuri sana ambao hawawezi kuonekana bila kuonekana katika mchezo. Kwa hiyo, mashindano ya kitaifa yale yarudi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba tuliona michezo ya walemavu. Watu wenye ulemavu wana vipaji vingi na pale ambapo sisi watu wazima wenye afya zetu tumeshindwa kuleta medali. Wao walipotuwakilisha huko nje wameleta medali hapa. (*Makofsi*)

Napenda kuwapongeza sana kwa hilo na hiyo inatutia ari zaidi kuwa tuwasaidie. Tuwasaidie tuhakikishe kuwa vile vipaji vyao ambavyo ni *hidden* basi viweze kuibuliwa. Linaloendana na hilo vile ni zile fursa, fursa kwa watu wenye ulemavu, vihakikishwe kuwa zinapatikana. Huduma za jamii katika majengo tuhakikishe zile *facility* zinakuwepo ili wapate urahisi wa kujihudumia. Kwa hiyo, viwepo *lift* zao maalum, ziwepo ngazi zao maalum, ziwepo vigari na kadhalika.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuanza mkakati wa kujenga uwanja mkubwa wa Kimataifa kwa ajili ya michezo. Ni matumaini yangu kuwa katika kipindi hiki cha fedha basi uwanja huu utaanza kujenga na nimefurahi vile vile kuona kuwa ule uwanja wa Taifa hautavunjwa tena, maana yake mwanzo kulikuwa na tetesi kwamba ungevunjiwa. Lakini uwanja ule utakuwepo utaimarishwa na ule mwininge utajengwa. Kwa sababu Tanzania tunahitaji viwanja vingi zaidi. Kwa kweli hata hicho kimoja hakitoshi. Lakini ni mwanzo nzuri napenda kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufanikisha hilo suala moja muhimu sana. (*Makofsi*)

Suala la *VETA*, napenda kupongeza sana uongozi wa *VETA* kwa kuwa wanatoa msukumo mzuri sana kwa kuwapatia ujuzi vijana wetu katika nyanja mbalimbali. Ningependa kutoa rai kuwa suala la *VETA* hivi vyuo vya ufundi ambavyo vimetapakaa bila utaratibu maalum basi waige, wajaribu kufikia zile *standards* za *VETA*, ili wapate kusajiliwa na ifike mahali at least kila Wilaya iwepo *VETA* moja. Kiwepo Chuo Kikuu kimoja, *I mean*, Chuo cha *VETA* ili zile amali, elimu ya amani iweze kusambaa kwa vijana na waweze kujitegemea na hiyo *of course* iende sambamba na upatikanaji wa mikopo kwa ajili kuwasaidia kurahisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kurudia kuwa naiunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofsi*)

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya mimi kujadili hoja ya Bajeti ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, mimi nasimama hasa ilikuwa nichangie kwenye maendeleo ya michezo. Lakini kwa vile Wizara hii ni Idara nyeti, naomba uniruhusu niongelee maeneo machache. Kwa kuanzia Ustawi wa Jamii. Idara hii ni muhimu sana na ishara kwamba Idara hii ni muhimu inajionyesha wazi katika majedwali mbalimbali ambayo Waziri ameainisha katika kitabu cha hotuba yake.

Kazi ya Idara hii ni kubwa zaidi hasa Wilayani ambako Maafisa Ustawi wa Jamii wanakuwa karibu sana na watu wenye matatizo ya kila aina. Lakini bahati mbaya sana nchini Tanzania Wizara hii wala haijionyeshi kuwa iko wazi, au iko wapi. Wizara ambayo tunajadili sasa ambapo Idara ya Ustawi wa Jamii iko inaitwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, wala haitaji Ustawi wa Jamii. Kwa ajili ya umuhimu wa Idara hii ningependekeza irejeshwe Wizara ya Afya ili itoe mchango wake kwa

wananchi vizuri zaidi kwa sababu sijawahi kumsikia Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya au rafiki yangu Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, hata mara moja akiitaja Idara hii muhimu na nyeti sana katika maendeleo ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, *VETA* Kielelezo (F) katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaanisha vituo vilivyoko nchini ambayyo viko chini ya *VETA* ni vituo vingi sana. Lakini jambo la kustusha ni idadi ya vituo hivi katika mikoa yetu mbalimbali. Mkoa unaongoza ni Dar es Salaam ambaou una vituo 182 ukifuaatiwa na Kilimanjaro vituo 62, Arusha vituo 52 na Iringa vituo 50. Lakini mikoa ambayo iko nyuma sana bahati mbaya ni Mkoa wangu wa Manyara una vituo vinane na Rukwa vituo nane.

Sasa nchi yoyote duniani hata Amerika imeweza kuendeshwa na kuendelea haraka siyo kwa ajili ya watu wenye shahada za udaktari au falsafa isipokuwa mafundi stadi ambaou wanaandalowi katika utaratibu kama huu wetu wa *VETA*.

Mikoa ambayo iko nyuma sana kwa kweli ina nafasi ndogo ya kuendelea. Mikoa hiyo ni Rukwa, Manyara, Lindi ambayo ina vituo 15 na Singida ambayo pia ina vituo 15. Kwa hiyo, natahadharisha Wizara hii kwamba hatua za haraka zisipochukuliwa ili kurekebisha dosari hii kutakuwa na tatizo kubwa sana katika kuleta maendeleo karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulisemea ni Sheria za Kazi Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba sheria za kazi katika nchi yetu zimepitwa na wakati. Tumeambiwa kwamba zitaletwa Bungeni hivi karibuni na kuwa Kamati zimeundwa kushughulikia Sheria hizi. Lakini kadri tunavyoenda matatizo yanazidi kuwa makubwa.

Kwa hiyo, athari ambazo zinasababishwa na sheria za zamani ni kubwa na bila shaka tunaona migogoro imekuwa mingi, migogoro ya kazi ni mingi, athari ambazo zinaletwa na sheria hizi ni nyingi. Tunasisitiza basi, sheria hizi ziletwe Bungeni ziende na wakati tulionao sasa hivi yaani karne ya 21. Migogoro sehemu za kazi kama vile *NBC*, *TTCL*, *TANESCO* na Shirika la Vifaa vya Elimu, kwa kweli inatia uchungu na pia inahatarisha amani katika nchi yetu. Tungependa Serikali ituambie inafanya jitihada gani kupambana na migogoro hii. (*Makofî*)

Kwa manufaa ya Watanzania watoa jasho lakini pia kwa wawekezaji walioko na wanaokuja. Sijasikia Serikali ikitoa tamko rasmi kuhusu hali hii ambayo inatisha kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu niseme machache kuhusu michezo. Michezo ni muhimu sana. Duniani kote hakuna nchi ambayo itajivuna, kutembea kifua mbele kwa maendeleo yake ya uchumi, maendeleo ya jamii bila kuhusisha michezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kweli, ndiyo maana nchi maskini sana tukiwa kwenye Maziwa Makuu kama Rwanda, inajitahidi sana kujitutumua kuonyesha kwamba na yenyeve iko. Rais Kagame wa Rwanda anajitahidi sana kuongoza nchi yake pia kuonyesha kwamba katika jumuia ya mataifa ukitaka uonekane uko pia utilie michezo maanani na ndiyo maana sasa hivi Rwanda inaenda kifua mbele, inaenda Tunisia kwenye kilele cha michezo wa mpira wa miguu kombe la Afrika. Ni zoezi ambalo sisi ni nchi ambayo tumepata sifuri hatukupata hata *point* hata moja. Hii siyo fedheha kwa Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya au kwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, peke yao hii ni fedheha kwa watu milioni 34 ya Tanzania.

Kwa hiyo, jitihada kubwa ambazo zinafanywa sasa hivi za kuleta maendeleo ya Jamii, maendeleo ya Uchumi, kujenga barabara, wenzetu wameondoka sasa hivi kwenda kufungua daraja kule Rufiji. Hii sherehe kubwa sana na wanakuwa mashuhuda kutoka sehemu mbalimbali katika Kanda yetu. Lakini hii yote haitoshi, kama katika nyanja hii ya michezo sisi tunakuwa kama aliyosema Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, tumekuwa kichwa cha mwendawazimu.

Kwa nini tunafika hapa? Kama kunakuwa na mwanga mbele ya safari katika maendeleo ya uchumi na jamii, kwa nini hapo tunashindwa? Hakuna asiyefahamu wote hapa wameongea, tatizo ni uongozi katika eneo la michezo. Uongozi wetu katika eneo hili ni mbovu kabisa na pale ambapo

tumejaliwa kuwa na nishani kwa mfano tulipopata nishani ya kwanza katika mchezo wa *All Africa Games Lagos*, Waziri wakati ule *Major General* Mstaafu ambaye sasa ni Balozi wetu Nairobi Mrisho Sarakikya, baada ya pale tumeshuka sana mpaka chini. Lazima Wizara hii ituvushe hapo, ituvushe katika aibu hii. Rais imeonekana kwa nia mzuri ameliona hili na ndiyo maana ameamua kujenga uwanja wa kisasa. Lakini uwanja wa kisasa ni kisingizio tu, Rwanda hakuna uwanja wa kisasa. Zambia hawana uwanja wa kisasa. Tatizo ni uongozi.

Mheshimiwa Spika, kule Kijijini kwangu, Mwenyekiti wangu anaitwa John Stephen Akhwari, mtu wa makamu kiasi ana miaka 70. mtu huyu alifanya maajabu katika *Olympics* kule Mexico mwaka 1968, siyo kwa kushinda, lakini kwa kumaliza *Marathon* ile akiwa ameumia mguu na anajulikana siyo kwa sababu ameshinda lakini kwa sababu mwenyewe amejitahidi akamaliza akiwa ameumia sana.

Mheshimiwa Spika, mahali ambapo udhaifu wa uongozi wa michezo Tanzania umejionyesha ilikuwa tangu wakati huo. Wale Maofisa aliofuatana nao hawakumpa hata maji ya kunywa hata maji ya matunda. Ni wananchi wachache wa Mexico ndiyo walikuwa wanampa maji ya machungwa na hali hii ya uongozi mbaya katika mchezo wa riadha kwa mfano, *Olympic* iliendelea hadi wakati wa *Olympics* kule Korea ya Kusini na robo tatu ya msafara wa Tanzania walikuwa Maafisa, yaani walioenda kule kama wachezaji ni robo tu. Watu wengine walikuwa Maafisa na wake zao na wafanyabiashara. Mwaka juzi tulikuwa na *Olympics*, hatukujaliwa kurejea na nishani lakini John Stephen Akhwari, ambaye *Olympics* ndiyo waliomtafuta mpaka wakampata, alipewa nishati ya heshima.

Mheshimiwa Spika, kwa vile hatukuwa na Ubalozi kule Sidney na Australia kwa ujumla, Watanzania walikabidhiwa kwa Mwanasheria mmoja mashauri pale Sidney akawa kama Balozi wao. Alipowaona ni watu wazuri na hasa John kuwa ni mtu muungwana sana, walimwita baadaye akakaa kule miezi sita ili kuendeleza michezo kwa watoto wadogo wa Kiaustralia na watoto wale waliweza kumchangia fedha nyingi tu na baadaye John, aliporudi akaiarifu Wizara ya kwamba kuna Mradi huu wa Uwanja wa Kisasa wa Mchezo wa Riadha na pesa zipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ikaunda Kamati na Kamati hiyo chini ya uongozi wa Ndugu Hashim Mbita, Balozi wetu wa sasa wa Zimbabwe. Kamati ile haikukutana hata siku moja toka wakati ule kwa sababu eti hakuna posho ya kukutana. Sasa sijui wale watoto wadogo wa Australia ambao wamechangisha mamilioni ya dola wanalionaje hili. John angeweza akaunda hata kampuni au *Foundation* yake akajenga uwanja huu na kituo kikubwa cha mchezo lakini ni kwa ajili ya uzalendo amewakabidhi Wizara. Sasa hii ndiyo iliyotufikisha hapa Wizara inasemaje kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu soka sijui tuseme nini kwa sababu uongozi wake ni mbovu sana, watu wametaja hapa kila aina ya uchungu jinsi ambavyo soka inaendeshwa. Lakini ningependa kuwaelekeza wenzangu wasome Jarida hili la JKT miaka 40. Katika mafanikio makubwa ya JKT miaka 40 kuna mwana-sport mmoja ameandikwa mwishoni na ametoa mapendekezo machache kuhusu tatizo la soka katika nichini. Naomba ninukuu sehemu chache sana ya makala ya mwana-sport huyu ambaye amechangia katika Jarida la miaka 40 ya JKT akitathmini miaka 40 na sisi pia tumefanya nini katika nyanda ya michezo?

Mheshimiwa Spika, kwanza, amesikitika sana kwamba *FIFA* inaona uchungu sana kuhusu Uongozi wa *FAT* Tanzania na anasema kwamba, napenda kumnuuu: "Sote tunaelewa kilichotokea baada ya akina Ndolanga kukimbilia *FIFA*. Shirikisho hilo bila aibu likatangaza kuifungia Tanzania kushiriki katika mashindano mbalimbali na matokeo yake Serikali nayo ikasalimu amri. Jambo hili lilitimvimbisha kichwa Ndolanga na wapambe wake. Cha kujiuliza sisi Watanzania ni hivi, kufungiwa kwa Tanzania kulikuwa na athari gani kiuchumi na kisiasa kama lengo letu lilikuwa ni kurekebisha mambo ili hatimaye tuondokane na aibu hii ya kufanya vibaya kila mwaka? Je, halikuwa jambo la busara kushikilia msimamo wetu wa kuwaondoa madarakani akina Ndolanga?" Anaendelea: "Nakumbuka jinsi Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alivyokuwa na msimamo katika maamuzi yake, mwaka 1965 Tanzania ilichukua uamuzi mzito wa kuvunja uhusiano wa Kibalozi na Uingereza kutokana na suala la Rhodesia sasa Zimbabwe. Bila shaka uamuzi huu ambao ulichukuliwa na Baba wa Taifa uliliumiza Taifa kiuchumi, lakini ilionekana ni muhimu kufanya hivyo ili kuionyeshea Uingereza kwamba tumechukizwa na jambo hilo. Suala la sisi kujiuliza sasa ni kwamba, je, ni kitu gani kilishindikana katika

suala hili la *FIFA*? Anasema, nia yake si kukumbusha yaliyopita, anachotaka kusema hapa ni kwamba tupende tusipende ipo haja ya kufanya mabadiliko ndani ya *FAT*. Viongozi walioko madarakani hivi sasa hawana uwezo wa kuendeleza mawazo mapya ambayo yanaweza kutusaidia Watanzania ili tuondokane na aibu hii.

Mheshimiwa Spika, Ndugu Ndolanga na wapambe wake ni lazima waukubali ukweli huu, mengi wamefanya na hakuna asiyefahamu, mchango wao tunaudhamini lakini ukweli hauleti tija yoyote katika Taifa letu, bado soka letu limebaki pale pale siku nenda, siku rudi. Tunataka wafahamu hilo kwamba Watanzania hawana tena haja na mchango wao wala wa mawazo yao, wanapenda kuwaona viongozi ambao siku zote wanakuwa wabunifu badala ya kulalama tu. Vitisho na kulalama hakusaidia kuondoa tatizo la soka.

Hivi majuzi iliripotiwa kwamba wachezaji wa timu ya Taifa kwa kuchukizwa na mambo fulani fulani yanayofanywa na *FAT*, kubwa ni kwamba walikosa posho zao, waliamua kugawana jezi za timu yao. Hii ni aibu sana siyo tu kwa Ndugu Ndolanga au Mheshimiwa Waziri, lakini ni kwa nchi nzima. Nani asiyefahamu jinsi wachezaji hawa waliviyolazimika kusafiri kwenda Zambia bila kulipwa posho zao licha ya kufadhiliwa usafiri na watu binafsi lakini ukiuliza *FAT* wanasema hakuna pesa. Huu sasa umekuwa wimbo wa chama hicho miaka nenda, miaka rudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa Mtanzania wa kawaida hawezi kuelewa hata kidogo kilio cha *FAT* kuhusu fedha wakati kila siku michezo ya ligi inachezwa na wao wanachukua mgao wao, sasa suala la ukata linatoka wapi? Ni suala ambalo Ndugu Ndolanga na wapambe wake wanapaswa watujibu. Vitisho na kulalama kwa Ndugu Ndolanga kusituogopeshe na wala kusitubweteshe Watanzania na kuendelea kupata aibu hii kila mwaka, kiongozi mzuri ni yule anayepima uongozi wake kwa kuzingatia mafanikio kwa lile analoliongoza na si vinginevyo. Wakati sasa umefika kwa Serikali ya Tanzania kuchukua hatua za makusudi, kurekebisha mambo ndani ya *FAT* bila kujali kama tutafungiwa na *FIFA*. Kwetu sisi tunaona ni kheri kufungiwa kuliko kuendelea kupata aibu na fedheha,” mwisho wa kunukuu. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau naomba niseme tu kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kuanza kuchangia naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Sir George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa kufiwa na mtoto wao. Mungu aiweke mahala pema roho ya marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Katibu Mkuu, Bwana Abubakar Rajabu, Wakurugenzi wa Idara mbalimbali katika Wizara yake na Taasisi mbalimbali ambazo zipo chini ya Wizara yake kwa kutuletea hotuba ambayo ni mzuri. Napenda kusema nawashukuru na kuwapongeza sana na pia napenda kuunga mkono hoja tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo machache lakini labda nianzie na hili linalotukera sana, nalo ni tatizo la ajira ya vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sisi ambao tunaishi Dar es Salaam kwa kweli hili ni tatizo ambalo linatisha, unaweza kusema *is a simmering but a very loud tricking time bomb*. Napenda kusema kwamba kwa kweli Wizara pamoja na wadau mbalimbali lazima tutafute mikakati ya aina yake ili kweli kuwanusuru vijana wetu katika tatizo la kuwa na ajira. Hili ni tatizo la kutisha sana. Kwa mfano, mimi nikipita katika kila kona ya Jimbo langu kuna vijana wanasmama kwenyela kona wananiambia njaa njaa,

*that is true* hawana mahala pa kupata kipato, nani ataweza kuwasaidia? Napenda kusema tu kwamba tatizo lipo. Kwa hiyo, napenda kuiomba sana Wizara hii iliwekee maanani suala hili.

Mheshimiwa Spika, naona hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 5 mpaka ukurasa wa 6, amezungumzia juu ya *Labour Exchange Centre* halafu kuna *Automative Services* na *Job Vacancy Survey*. Haya yanahitaji yapewe maelezo zaidi kwa sababu sisi kama Wawakilishi tungependa tusaidiane na Serikali yetu kwa kupata nini hasa kinatakiwa tukifanye ili tuweze kuwasaidia vijana wetu katika kupata kazi ambazo zinaweza kupatikana. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba naomba maelezo zaidi yatolewe katika hili ili tuweze kusaidiana na wenzetu Wizarani pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda nzungumzie ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kweli nimeshangazwa kwa sababu ninavyokumbuka mimi mwaka 2000 tuliambiwa hapa kwamba Sera ya Wazee imeandaliwa na mwaka 2001 ikawa imepita na katika moja ya majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa swali langu ni kwamba, kweli wazee wangeanza kupata pia mikopo katika mwaka huo wa fedha lakini baadaye tukaambiwa ya kwamba bahati mbaya sana kulikuwa na *technical problem*.

Mheshimiwa Spika, sasa ningedhani kwamba badala ya kusema hapa, naomba ninukuu, anasema: “Idara ya Ustawi wa Jamii, ka-sentensi kamoja tu, Sera ya Taifa ya Wazee ilikamilika na kuitishwa na Baraza la Mawaziri.” Sasa napenda kuuliza kwamba baada ya kuitishwa na kukamilika nini kinaendelea au tatizo liko pale pale?

Napenda kusema kwamba kwa kweli Mheshimiwa Waziri hii sentensi moja hainiridhishi, najua wewe ni rafiki yangu sana na wote tuna vibara tunavyofanana, basi naomba kabisa kwamba katika hili unipe majibu ili nikirudi Jimboni niweze kuwaeleza wazee wangu nini kinaendelea kuhusu sera yao na hasa utekelezaji wa hiyo sera kwa maana ya kuwapatia mikopo na ikiwezekana pia kuwasaidia kwenye usafiri, usafiri kwa maana ama wapunguziwe nauli au waingie kwenye mabasi bure kwa maana ya wazee.

Sasa naomba haya yote utakapokuwa unajumuisha basi unisaidie ili niende na kitu ambacho kinaeleweka kwa hao wananchi wangu. Pia nadhani nazungumzia kwa nchi nzima. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo naomba sasa nigosie hili tatizo la NSSF. Wote tumekuwa na uzoefu kidogo kwa wale ambaa walikuwa ni wafanyakazi wa *East African Community* ili yovunjika, jinsi wanavyosota mpaka leo hii wengi wao hawajapata fedha zao, pensheni zao. Sasa tunaambiwa kwamba Bunge hili, sisi sote humu ndani tulikaa, tukapitisha kwamba kuanzia sasa ye yeyote ambaye atakuwa anachangia kwenye pensheni ya NSSF kwa mfano ameacha kazi au ameachishwa kazi kwenye umri wa miaka 35 au 40 hatakubaliwa kuchukua zile fedha mpaka afikishe miaka 60.

Sasa napenda kusema kwamba kwa kweli kama tulipitisha hapa hii Sheria basi ni kosa kubwa sana. Ningependa kuomba kabisa kwamba hii Sheria irekebishwe kwa maana ya kwamba endapo mwananchi anaachishwa kazi au yeye mwenyewe akiacha kazi kwa umri mdogo sana, basi aruhusiwe kuchukua kile alichochangia ili kiwe ndiyo mtaji wake wa kuanza maisha yake mapya. Ukisema asubiri mpaka kustaafu mtu huyu anaweza akafa, zitakwenda wapi hizo pesa.

Kwa hiyo, napenda kusema naomba sana kama kweli kuna tatizo hilo basi wataalam Wizarani na Sheria nzima irekebishwe ili kuwaruhusu wananchi waweze kupata fedha zao pale wanapoacha kazi ili wawe na chanzo cha kuanzia kufanya kazi kuliko hivi sasa wanapowaambia wasubiri mpaka wafikishe miaka 60.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni ombi tu, nalo ni kwamba katika miaka ya 1990 nakumbuka kulikuwa na Shirika likiitwa *Tools for Self Alliance*. Ni Shirika ambalo linakarabati vifaa na hatimaye kuwapa vijana bure kwa ajili ya kuvifanya kazi kwa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, hili Shirika ninavyokumbuka lilikuwa Uingereza, Houghton wakati ule lilikuwa linasimamiwa na Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, pamoja na *Father Trevor Huddlestane*.

Sasa napenda kuomba kwamba kama hivi vifaa vipo basi Wizara inayohusika itusaidie kutuunganisha na hawa jamaa ili tuweze tena kupata hivi vifaa ili kusaidia kuwapatia vijana wetu vifaa nya kufanya kazi na kuweza kujajiri wao wenye.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo machache tu lakini napenda kusema kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa asilimia mia moja. Lakini naomba nipate maelezo kuhusu Wazee na kuhusu *NSSF*. Nashukuru. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuongea machache katika Bunge hili la kihistoria la Mfumo wa Vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza na hotuba yangu kitu ambacho kilinhamasisha hasa niweze kuchangia ni suala zima la kimichezo yaani *football*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini awali ya yote ningependa pia nimshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa namna ambavyo ameweza kuiwasilisha hotuba yetu kama tulivyotuma kwa siku ya leo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa namna pia naye alivyoiwasilisha hotuba yake na kwa namna ambavyo nimemfahamu mimi binafsi. Lakini sitasita pia kuchangia ambayo yeeye hakuyagusia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda nianze na suala zima la Mwenge wa Uhuru. Mwenge wa Uhuru ulikuwa ni mali ya Chama cha CCM hapo mwanzo wakati wa Mfumo wa Chama kimoja. Lakini baada ya Mfumo wa Vyama vingi, Serikali kwa makusudi iliweza kusema kwamba Mwenge wa Uhuru sasa uwe mali ya Serikali. Kwa maana hiyo basi, ningependa kusema ya kwamba mfumo mzima ambao unatumika katika kukimbiza Mwenge uangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu wanaokimbiza Mwenge wanatoka katika Umoja wa Vijana wa CCM...

**MBUNGE FULANI:** Aah, siyo kweli.

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Hayo ni maneno yangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hata wakimbizaji wa Mwenge basi inaonekana wanaeneza Itikadi ya CCM kwa sababu hata vazi wanlovaa linaashiria rangi ya kijani. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo ni kinyume na mfumo ambao sasa hivi tunao na unawenza ukaleta mashaka namna ya kukimbiza kwa Mwenge huu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ileweke wazi kwamba mimi nikikuona wewe umevaa Nembo ya CCM na mimi nikivaa Nembo ya *CUF*, mwingine akivaa Nembo ya CHADEMA au vyama vilivyoko, hatujui Mwenge huu tutaupokea namna gani. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la wazi ya kwamba kufanya hivyo ni kosa ili sote tuwe na haki ya kushiriki katika mapokezi ya Mwenge huu na siyo sisi ambao si Wanachama wa Chama hicho cha CCM kushiriki katika kueneza Itikadi ya Chama kimoja ambapo na mimi nina Sera za Chama changu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, kabla ya mapokezi ya Mwenge tunakumbuka sote tunasema ya kwamba pia Mwenge ni moja kati ya vyanzo vya uhamasishaji wa maendeleo. Mwenge huu hupangiwa Viongozi wa Chama na Serikali ili kufungua baadhi ya miradi ya eneo lile ambalo Mwenge utafika.

Kwa hiyo, viongozi hawa pia nao wanatakiwa wapate elimu kwamba pale wanapokwenda kufungua miradi ya Kiserikali katika eneo lile kwamba siyo miradi ya chama fulani kwa sababu hotuba zinazotumika pale zinaashiria pia alama au dalili za mchafuko wa hali ya hewa kwa wakati ule. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nina mifano mizuri, mimi binafsi wakati niko nje ya Bunge hili na kabla ya mbio hizi ambazo zitaanza sasa hivi, Msemaji aliyejukua katika Jimbo langu kwa kweli nilikuwa ni mstaarabu tu wa kivazi pamoja na moyo, lakini siku ile ingekuwa ni kasheshe kubwa kwa wapiga kura wangu. Ilikuwa mara Kidumu Chama cha Mapinduzi, sasa nilikuwa najiuliza kuna nini? Badala ya kufungua miradi wameleta nini?

Mheshimiwa Spika, wengine wakaniambia Mheshimiwa Mbunge sasa tumefika wapi, tuondoke, nikawaambia leteni ustaarabu, kama Mbunge wako tua. Wakaniambia haiwezekani, nikawaambia itawezekana kaeni. Sasa napenda kusema kwamba haya ni matatizo, yarekebishwe. Suala la Mwenge linatosha. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa napenda kuzungumzia Taasisi za Watu Wasiojiweza. Kwanza, napenda niwapongeze kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ushujaa wao. Ningekuwa mimi katika Wizara hii ningewambia Mheshimiwa Rais kuwa kazi aliyonipa mimi imenishinda, kweli kabisa kiungwana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ni muhimu kuwepo, tunaelewa sote kwamba tunao watu ambao hawajiwezi iwe vijana, wazee na hata vikongwe. Lakini Taasisi hii haipatiwi fedha ya kuwasaidia watu wetu hawa, sasa tunakusudia nini? Ukiisoma Katiba yetu ujenzi wa ujamaa na kujitegemea, haiendi sambamba na kukosa huduma kwa Watanzania hawa, kabisa. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba Taasisi hii ipatiwe fedha ili iweze kuendesa shughuli zake ipasavyo kama ambavyo imejipangia.

Mheshimiwa Spika, Taasisi hii ni pamoja na walemovu na walemovu nao ni wanadamu walioumbwa wakiwa huru. Nimechoshwa niliposoma ujumbe wa wenzetu hawa walemovu, kwa kweli nilihisi kilio lakini sikuwa na namna zaidi ya kuyasemea haya.

Mheshimiwa Spika, nini wameyasema, kwa idhini yako Mheshimiwa Spika ningeomba ninukuu ambapo ujumbe huu kila Mheshimiwa Mbunge ameupata, inaitwa Sera ya Watu wenye Ulemavu, nitanukuu kwa kifupi sana: "Hivyo sisi watu wenye ulemavu nchini Tanzania tunasema tunanyanyaswa kiasi cha kutosha, tunaonewa kiasi cha kutosha na tunadharauliwa kiasi cha kutosha na ni kutokana na unyonge wetu unaotokana na ulemavu wetu ambao hatukuumba kwa Mwenyezi Mungu wetu, lakini sasa tunasema basi imetosha na tumechoka. Serikali iwathamini watu wenye ulemavu kwa kuwatendea haki kama ilivyokwishakufanya kwa watu wa makundi mengine na masuala mengine yaliyohitaji sera kwa kupitisha Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na jamii ya Watanzania kwa ujumla mtusaidie kuisukuma Serikali ili iweze kutoa sera kwa watu wenye ulemavu haraka iwezenavyo," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kilio hiki ni kikubwa mno wa kuyasemea na kuyasikiliza ni sisi, kilio kifike Serikalini na Serikali ndiyo hii, iwaone wenzetu hawa, tuwahurumie tukijua ya kwamba na sisi ni walemovu leo au kesho. Ni juzi tu Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, tulikuwa naye katika michezo, leo ameingia Bungeni akiwa na fimbo, ni sehemu ya ulemavu. Aah! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuongelea kuhusu michezo. Nilikuwa nizungumzie fedha za Miradi kwa Vijana, Sheria ya Matunzo kwa Mtoto na aah Vyuo Stadi lakini sasa naona niende katika kabumbu kwanza, kama muda upo nitazungumzia haya.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeza Mheshimiwa Philip Marmo, kwa namna ambavyo amewasilisha kilio cha michezo na mimi nilikuwa nimepanga kusema hivyo lakini nilikuwa sitaki nimtaje ni nani anayesababisha migogoro. Lakini napenda kusema Ndolanga aah!

Mimi sitaki nimtaje huyu kwa sababu yeje siyo Mbunge, hana sehemu ya kujitetea lakini kitabu kimemtaja Ndugu Ndolanga kwamba ni chanzo cha migogoro, kwa nini? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wengine wameisifia Simba, ni Klabu Bingwa, imeshinda, wameisahau Yanga kwa nini? Right kama Yanga si timu staarabu wakijijua kwamba wamebeba jina la Tanzania kwa kuitwa *Dar es Salaam Young Africans*, leo kungekuwa na migogoro zaidi ya ile iliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita Waheshimiwa Wabunge tulifika Jamhuri kwenda kuangalia kati ya mchezo wa Yanga na Palson. Vijana hawa wallingia mitini, tukasoma magazeti wakasema, kwa vile timu moja haikufika uwanjani Yanga inakabidhiwa *point* tatu. Baadaye tunasikia Yanga inajimwanga tena uwanjani kesho, aah, sasa kwa nini? Na Yanga nasikia wapo wanachukua mazoezi, Yanga watafanya mauaji ya kinyama kesho. Lakini nina wasiwasi mauaji haya kwamba Yanga watanyang'anywa *point* tatu, nina wasiwasi kwa moja tu.

Juzi nilisoma Gazeti la Nipashe kwamba *Referee* alimtolea kadi nyekundu mchezaji, akamwambia toka nje, mchezaji akamwambia nitoke nje kwa nini, hivi kupiga chenga tatu, tano ni makosa? *Referee* akamwambia wewe umefanya madoido, umepiga sijui nini, toka nje. Sasa nina wasiwasi kwamba na huyu Yanga akifanya mauaji ya namna hiyo ataambiwa *point* tatu hauna. Sasa Mheshimiwa Waziri nithibitishie kama Yanga atafanya mauaji ya kinyama kesho hatanyang'anywa *point* tatu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ningetaka kujua Sheria za Michezo kwa sababu Sheria kila siku zinaongezeka. Hivi leo tunasikia kuna *Yanga Family*, ni migogoro hiyo hiyo inayotokana na huyu ambaye kwamba sitaki nimtaje, ndio mgawanyiko huu.

Mheshimiwa Spika, Yanga inaitwa *Dar es Salaam Young Africans*, jina la kwanza hilo na Simba inaitwa Watoto wa Msimbazi, ukipenda Watoto Wekundu, je, kwa majina haya zaidi ya moja klubu ambayo inasajili si kinyume na taratibu ya Katiba zao na Katiba za *FAT*? Kama hivyo ndivyo basi Yanga iitwe *Dar es Saalam Young Africans*, hakuna tatizo kwa sababu Yanga itakuwa ni kubwa kuliko Simba, Simba anaishi ndani ya Mji wa Yanga. Kwa hiyo, mara zote tanguliza Yanga kuliko Simba.

#### **WABUNGE FULANI:** Sawa sawa!

**MHE. SALIM OMAR ALI:** Mheshimiwa Spika, napenda na hapa nisemee kidogo kuhusu matunzo ya mtoto. Sheria ya Matunzo ya Mtoto naomba haraka ifanyiwe mabadiliko kwa sababu Sheria hii ni sawa na Gazeti la Alasiri. Gazeti la Alasiri linauzwa kwa bei ya shilingi 100/= na Sheria ya Mtoto ambaye ametekelizwa na baba au mama faini yake ni shilingi 100/=.

Mheshimiwa Spika, sasa ninapenda kusema kwamba hii sheria imepitwa na wakati, irekebishwe haraka ili kuokoa kizazi cha baadaye, hili ndilo Taifa la baadaye. Majaribio ni mengi ya kutupa watoto ovyo.

Kwa hiyo, haraka sana Sheria hii ifanyiwe marekebisheso ili kuweza kuwalinda watoto wetu hawa. Tukiendelea kulifumbia macho hili tatizo basi tutawakosa vijana wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zaidi ya mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanen watakaotufikisha Saa 7.00 mchana ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalam wake kwa ujumla. Kwa kweli kazi waliyofanya, wamefanya kazi nzuri, wameandika vizuri sana hotuba yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Dr. Radhaman Dau wa NSSF, kwa kweli amefanya kazi kubwa sana na nisimsahau Mwenyezekiti wake anaitwa Silaju Juma, kazi inaonekana na ninawaombeni msikate tamaa. Fanyeni kazi, ujenzi mnaoufanya ni wa uhakaki na nafikiri Dodoma hapa kuna kitu mtakuja kufanya kizito zaidi, tunawaombeeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi natoka kwenye Wilaya mpya ya Kilolo sehemu ya Ilula tunahitaji soko. Nakuomba *Doctor* tuma wataalam wakafanye tathmini utusaidie tujenge soko utakuwa umetusaidia sana kuondoa tatizo la ajira kwa vijana kwa sababu tatizo ni kubwa vijana wako wengi na wamekimbilia pale kwa hiyo, tusaidie, *Doctor* kwa kweli utakuwa umefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia niwapongeze sana *VETA* kwa sababu wanamsaidia sana Mheshimiwa Waziri Kapuya kwenye Wizara yake kwa sababu vijana wengi wamepita kule na sasa hivi wameanza kujitegemea kwa hiyo tatizo la ajira limeanza kupungua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, isipokuwa ushauri wangu ni kwamba wale vijana wanaomaliza *VETA* wakopeshwe vifaa ili waende kuanzia maisha. Wakishakopeshwa watakuwa wamepunguza tatizo la ajira kwa sababu sasa hivi kama mnnavyojua vijana kwa sababu hakuna shughuli wakiambiwa twende mkale pilau wanakwenda kesho wataambiwa twende tukaanzishe Jeshi au chukueni silaha watakwenda kwa sababu hawana ajira, kwa hiyo, tusaidiane katika suala hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Wilaya yetu ya Kilolo kwa sababu ndio tumeanza kupima tumeshawatengea nafasi, naomba waje tuwaonyeshe sehemu na sisi tutawasaidia kufyauta tofali ili waweze kutujengea Chuo. Kama mnnavyojua vijana wengi sana hawa *ma-house girls* wanatoka Iringa – Kilolo. Sasa ni vizuri wakatusaidia kwa sababu baadaye athari yake itakuwa kubwa. Kwa hiyo, naomba sana *VETA* mje kwenye Wilaya yetu mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana wale vijana walioqwenda kushiriki katika *Special Olympic* kule Ireland bahati nzuri nilipata bahati ya kuhudhuria. Kwa kweli kwa mara ya kwanza toka tumpata uhuru nafikiri nchi yetu haijawahi kupata medali nydingi kama zile, medali 18 na nne za dhahabu. Kwa hiyo, niipongeze Wizara lakini pia niwapongeze Wabunge na hasa Mwenyekiti wetu Anne Makinda kwa sababu alishiriki katika kuchangia ili timu ile iende Ireland. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kimoja Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, wale vijana wana hamu ya kukuona kwa sababu hawakukuona angalau ukawape mkono ili waone mchango wao umefika kwa sababu mpaka leo wanajisikia wapweke.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Margareth Mkanga, kwa kweli amekuwa bega kwa bega kuwasaidia wale mavu, maana siku zote husemwa kwamba hata ninyi wazima ni wale mavu watarajiwa kwa hiyo lazima tumuunge mkono. Kwa hiyo, watu hawa wawe na michezo yao *special* nao washiriki kwa sababu kuna michezo mingi wasioona wanacheza mpira, *basket* na michezo yote kwa hiyo tuisiwaterenge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kusaidia Wizara, hii nazungumza kwa michezo yote, kwamba tunapoambiwa tutayarische programu ya michezo maana yake wanataka kutusaidia kutupa fedha, leo hii na wasiwasi kama *FAT* programu yao ya mwaka huu wameleta. Ukiangalia fedha ambazo tumetengewa kwenye michezo kwa mwaka huu nafikiri haizidi shilingi milioni 90 pesa ya nauli ya timu moja kwenda kwenye *Olympic*. Ukingalia unatakuta wenyewe hawakuleta wakiambiwa walete programu wanaleta ratiba. Sasa Wizara iwasaidie, tuwape programu. Bahati nzuri Mwenyekiti wa BMT mnajua uwezo wake ni mkubwa anapiga kelele kila siku na mfano amenzia hapa Bungeni mmeona timu ya Bunge inavyofanya vizuri yote ni juhudji yake kwamba mambo yanaanzia hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wanasema kwamba ukiona mtu mzima analia mbele za watu ujue kwamba kuna jambo, Waheshimiwa wote wamezungumzia habari ya *FAT* lakini mtu wa kwanza kulaumiwa ni yule anayebeba bango lazima tukubaliane kwamba kwanza tunaanza na Mwenyekiti kuna tatizo, Katibu kuna tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kumaliza tatizo hili lakini ye ye binafsi hawezi kulitata kwa sababu mimi nimeshakaa na pande zote mbili upande mmoja unasema hapana Waziri hawezi kutenda haki kwa sababu ambazo wao wanazijua labda kuna mtu ambaye, sielewi. Lakini ni vizuri kwa sababu Mheshimiwa Waziri juzi ametoka kutatua mgogoro wa Benki mkubwa kuliko ule awakalishe

chini wanatutia aibu, Ndolanga na Wambura wanatutia aibu. Wanatutia aibu kwa sababu Mheshimiwa Rais sasa hivi ameamua kujenga uwanja ule sasa uwanja utakuwa na maana gani kama migogoro itaendelea?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Kapuya uombe mtu ambaye unafikiri anaweza kuwa *neutral* kama ambavyo mech ikechezwa ukiona hujatendewa haki unaenda *neutral ground* kwa hiyo, uwaombe watu wawapatanishe hawa kwa sababu ni aibu. Kwa sababu leo hii Wambura ameshtakiwa kwa kupeleka michezo Mahakamani kitu ambacho ni aibu, mimi sjawahi kusikia duniani michezo inapelekwa Mahakamani lakini Tanzania ndio mara ya kwanza. Leo hii tena Ndolanga anarudia anampeleka Wambura Mahakamani, sasa hii mimi sielewi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uwaombe wale wakae chini wamalize tofauti zao.

Mheshimiwa Spika, tusingekuwa tunashiriki kwenye michezo ya Kimataifa kwa mfano wenzetu Simba wanaingia kwenye michezo hiyo mikubwa inayokuja, tungeomba kabisa tuondolewe kwa sababu wenzetu wa Benin walikubali kuondolewa kwenye michezo wamekaa miaka mitatu wamejimirisha wamekuja kutufunga na sasa hivi wanashiriki kwenye michezo mikubwa. Kwa hiyo na sisi ingekuwa ni nafasi nzuri lakini kwa kuwa wenzetu wa Msimbazi wanashiriki basi tunalifumbia macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri mkutano mkuu wa *FAT* na mimi niko tayari kukuchangia kidogo ufanyike haraka sana. Kama hutanijibu suala hilo vizuri mimi kwa kweli kwenye mshahara wako nitalia na wewe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amedai anaendelea kufanya ukaguzi kwenye Vyama na Klabu za michezo ukweli ni kwamba hakuna Chama hata kimoja ambacho kimefanyiwa ukaguzi. Nitashukuru kama atanielezea hapa kuna Chama chochote kimefanyiwa ukaguzi kwa sababu ukiangalia *FAT* yenye mwaka jana wamepata bilioni moja na laki mbili tuulize hizo fedha ziko wapi mpaka wameshindwa kupeleka timu Sudan kwa milioni tisa?

Mheshimiwa Spika, nzungumzie tatizo ambalo linasababisha migogoro, moja wale viongozi ambaao wanakuwa kwenye madaraka wengi sio wanamichezo. Kwa hiyo inapofikia kipindi kile cha kuchaguliwa wanaleta upinzani mkubwa wa mabadiliko. Wanaposhindwa hoja wanakwenda Mahakamani, wakishaenda Mahakamani basi biashara hapo imekwisha. Tatizo ni nini? Katiba ya *FAT* haifai kwa sababu uchaguzi haushirikishi wadau wenye kama vile Makocha, Waamuzi, wanachama, wakereketwa, wapenzi, wafadhili, Madaktari, watazamaji na Waandishi wa Habari. Cha kushangaza wanaochagua uongozi wa *FAT* wako watu 67 utashindwa kuwanunua?

**SPIKA:** Naambiwa na wanaoandika *Hansard* kwamba umekaribia mno microphone kwa hiyo sauti yako inadunda kwenye mashine zao. (*Kicheko*)

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Nashukuru.

**SPIKA:** Kaa mbali kidogo.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Nashukuru. Kwa hiyo, wigo ule upanuliwe waongezwe watu wafifikie hata 3,000 kwa sababu Watanzania tuko zaidi ya milioni 39 kwa hiyo tukiongeza wigo tutapata viongozi wazuri na sifa zianishwe wazi maana viongozi wengi ambaao wako kwenye michezo sasa hivi wako pale kwa sababu ya kujijengea umaarufu zaidi kuliko kuendeleza wanamichezo kwa sababu michezo kwa ujumla inatakiwa iendeshwe na watu wenye ambao wanajua nini maana ya michezo.

Mheshimiwa Spika, suala la bajeti nimesema bajeti tuliyopewa ni finyu lakini inasababishwa na sisi kutopeleka programu mapema.

Mheshimiwa Spika, turekebishe Sheria ya *BMT* ipate meno zaidi kwa sababu Mheshimiwa Joel Bendera, pamoa na kuwa tumempa Uenyekiti meno hana ni kibogoyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuandaliwe mpango maalum wa michezo kwa vijana. Tutamwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu ili atufikirie kwanza tuanze toka chini kwa sababu bila hivyo itakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, halafu pia kama ambavyo tuna *special schools* za watoto wenye vipaji maalum basi na michezo iwekwe hivyo. Naamini suala la michezo Watanzania wengi hawajalitia mkazo, wanajua ukishiriki kwenye michezo basi unakuwa mhuni, mhuni. Michezo ndio kipimo cha afya yako, ukiona mtu hashiriki kwenye michezo ujue ana tatizo na tatizo lipi, anaumwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iipe BMT fedha za kuendeleza shughuli za michezo na kutafuta vyanzo vingine vya kujiungezea mapato. Nashukuru Serikali kwa kuamua kwamba michezo ile ya kubahatisha fedha zitengwe lipolekewe Baraza sasa hivi angalau tutaona umuhimu wa michezo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa nimalizie kwa sababu Mheshimiwa Spika kaniongezea muda, ni suala la sheria. Kuna sheria nyingine ambazo zinapingana na ajira, sitaki kuizungumzia sheria ambayo juzi nilisema imeleta matatizo kidogo isipokuwa niseme hivi kuna sheria anabidi ziangaliwe kwa mfano kuna sheria inayosema kwamba mtu anapokuwa na shilingi 15,000/= mfukoni lazima apewe ulinzi wa Polisi, sheria kama hii imepitwa na wakati.

Kwa hiyo sheria nyingine ambazo zinaweza kukusababishia migogoro ni vizuri tukasaidiana, tukazzungumza zikafutika mapema kabla migogoro haijaanza. Sasa hivi watu wameshaanza kukosa ajira kwa sababu fulani fulani ambazo sitaki kuzisema na watu wakikosa ajira unawalazimisha kufanya kitu ambacho hawakutegemea. Sasa hivi kuna UKIMWI unamlazimisha yule mtu aache ile ajira yake ya kawaida aende kushiriki kwenye biashara nyingine ambayo itamletea madhara. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba mjaribu kupitia sheria zile ili zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, suala la Ukimwi, Wizara hii bado halijalitia kipaumbele na ndio Wizara yenye vijana.

Mheshimiwa Spika, tunasema mikopo kwa vijana, unawapa vijana Sh.200,000 watu watano hivi kweli tunataka kuwasaidia au tunataka kuwalaliza? Tuwape mikopo inayokubalika halafu tupitishie kwenye *SACCOS*. Sasa hivi bahati nzuri sehemu nyingi wameshaanzisha *SACCOS* zile fedha badala ya...

(*Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Mwalimu wangu pamoja na Wizara yake kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kutayarisha bajeti hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, michezo huburudisha, michezo hujenga akili na mwili, michezo husaidia kuzuia maradhi. Hivyo basi, ni muhimu kila mtu kushiriki katika michezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni muhimu kila mtu kucheza kwa mfano mimba huhitaji kucheza na mimba isipocheza mama huwa anakuwa na wasiwasi atakwenda hospitalini kwa sababu michezo ni muhimu kwa kila kiumbe na mimba ni kiumbe. Kwa hiyo, michezo ni uhai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mtoto asipocheza vile vile mama yake anakuwa na wasiwasi atamuuliza maswali mbalimbali, unaumwa tumbo, masikio na mtoto asipoweza kujieleza mama atakimbia hospitalini ili kuona kujuu kama mtoto wake ana matatizo kwa sababu michezo ni dalili ya uhai. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kijana naye anahitaji kucheza na ndio maana tunaomba michezo iwepo mashulen. Ninaposema michezo sio mpira wa miguu tu ni michezo ya aina yote. Kuna michezo inaonekana kufifia mashulen kwa mfano michezo ya kutupa tufe, kutupa mkuki, kuogelea, sarakasi,

*volleyball* na aina nyingi za michezo. Kwa hiyo, tunamwomba Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu waone umuhimu wa michezo na michezo ya namna hii ifufuliwe mashulen. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni muhimu kwa kila mtu kucheza, basi tunaomba kila mtu ajengewe mazingira ya kucheza. Wazee nao wanahitaji kucheza kwa sababu kama nilivyosema michezo inasaidia sana kupunguza maradhi na kuna maradhi ya uzeeni kama vile *rheumatism, gout*, watu wengi wanalamika hapa kwamba miguu inawasumbua ni kwa sababu hawachezi. Nashauri kila mtu ajitahidi kucheza. Kuna watu wana *pressure* na kisukari, hayo yote ukiwaliza Madaktari watakushauri kucheza. Nashauri sana michezo itiliwe maanani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, michezo ni taaluma, tunamwomba Waziri anayehusika akishirikiana na Waziri wa Elimu wahakikishe kwamba michezo inakuwepo katika vipindi vyetu mashulen. Kila darasa liwe na kipindi kimoja cha michezo angalau kila siku ili kuwajenga watoto wetu kiakili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwepo na vilabu kwa michezo, saa za jioni wakati watoto wanakuwa hawapo shulen wawe na klubu mbalimbali kama tulivyokuwa navyo zamani waweze kucheza kuburudisha akili.

Mheshimiwa Spika, viwanja vyetu vya michezo vinahitaji kuboreshwa. Viwanja vingi ni vibovu, viwanja vya Dar es Salaam utakuta watoto wetu wanachezea katika michanga lakini wanahitaji hamasa ili kuviboresha viwanja vyetu. Nadhani kuboresha viwanja hakuhitaji pesa nyingi ni kuhamasisha vijana kwa sababu wanapenda michezo viwanja vilivyo vingi wanaweza kutengeneza wao wenyewe kama kupanda majani.

Mheshimiwa Spika, nchi kama Saudi Arabia wana viwanja vizuri sana vya michezo vyenye majani mazuri ingawa ni jangwa kwa nini sisi tusiboreshe viwanja vyetu? Ni hamasa tu kwa hiyo tuhamasishe vijana watengeneze viwanja vyetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vijana wanahitaji motisha, kuna vijana wanaoishi vijiji wanahitaji kucheza na wanapenda sana michezo lakini hawana motisha ya kutosha. Kuna vilabu vya michezo kama vile *Mbanga FC* na *Gungu Rangers* kule Kigoma wanahitaji motisha kwa kuletewa timu nzuri nzuri waweze kupambana nazo kusudi waweze kujiendeze kimichezo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia michezo, naomba niendelee na upande wa kazi, vijana kwa kukaa vijiweni utakuta wanapatwa na matatizo mbalimbali, wanajuhisha na vitendo viovu kama vile ulevi, uvutaji bangi, ubakaji na kadhalika. Lakini kuna vijana wametambua ubaya huu wameamua kuijunga katika vikundi mbalimbali au kuanzisha *NGOs*. Kule kwetu tuna *NGO* ya wavuta bangi au tuna *NGO* ya vijana walioamua kuachana na mambo ya bangi kusudi waweze kujiendeze. Vijana hawa wanasema bado wanavuta kidogo kidogo ili kusudi waweze kupunguza polepole. Vijana hawa tunapaswa tuwape moyo tuwajengee mazingira mazuri waweze kuachana kabisa na uvutaji bangi kwa sababu wenyewe wameshatambua ubaya wake. Kwa hiyo, vijana hawa tuwape misada. Sasa hivi kuna mfuko wa pembejeo lakini vijana hawa hawana dhamana. Kwa hiyo naomba Wizara hii iwadhamini vijana hawa ili waweze kupata pembejeo mfano trekt na mashamba nina hakika baada ya mavuno wataweza kulipa kwa sababu wameshatambua uovu wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna vituo vya kulelea watoto yatima, kule kwetu kuna vituo vinavyolea watoto yatima amba wana umri wa kuanzia siku moja mpaka mwaka mmoja na nusu. Naomba kutoa shukrani kwa *NGOs* za kidini na nyingine zilizojitolea kuwalea watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni kwamba watoto hao wa mwaka mmoja na nusu amba wamefiwa na wazazi wao wanapoachiwa kulelewa na ndugu hali zao zinarudi nyuma. Naomba wasaidiwe angalau kijengwe kituo cha kuwalea watoto kuanzia mwaka mmoja na nusu mpaka saba kwa sababu umri huu ni mdogo mno kwa mtoto kuachiwa kusaidiwa na watu amba wakati mwininge hawana elimu ya kutosha ya kuwatanza watoto hawa, kuwapa mazingira ambayo walikuwa wamezoea. Watoto hawa wanahitaji msaada wasaidiwe, huu ndio ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, tumepata mifano mizuri ya vijana ambao wameamua kujikwamua kiuchumi kwa mfano vijana wa Kiluvya Dar es Salaam. Vijana hawa wanafanya kazi nzuri lakini wanatumiwa vibaya. Tunaomba Serikali ikiangalie kituo hiki iwasaide vijana hawa ili waweze kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wa Kisukuma ambao wanaishi Kigamboni, ni mfano mzuri wa kuigwa wanalima nyanya na wana maendeleo mazuri. Nina hakika vijana hawa wataondokana na umaskini. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kupitia *TASAF* wameweza kuwasaidia na wenyewe wakajisaidia wakajenga zahanati nzuri ambayo inawasaidia kimaisha lakini tungeomba vijana hawa wapatiwe soko la kutosha ili waweze kunufaika na jasho lao. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nazidi kumpongeza Mwalimu wangu na Wizara hii na naunga mkono hoja. (*Makofsi*)

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kupongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameiwasilisha asubuhi hii. Nimpungeze Naibu Waziri, katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote kwa kazi ambazo wamekuwa wakizifanya hasa ukizingatia kwamba Wizara hii ina umuhimu mkubwa sana kwa sababu inashughulikia makundi makubwa na muhimu sana kwa upande wa vijana, michezo, kazi na walemvu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nichukue nafasi hii kupongeza shirika la *NSSF*, *Cargo Stars* kwa kuona umuhimu wa michezo na kuwafadhili Waheshimiwa Wabunge katika mashindano yao waliofanyika wiki iliyopita bila kumsahau Mwenyekiti wa BMT, Mheshimiwa Joel Bendera, kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya kuhakikisha kwamba na sisi Waheshimiwa Wabunge tunashiriki kikamilifu katika shughuli nzima ya michezo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia pale ambapo wenzangu wamesisitiza hasa kwa upande wa michezo. Michezo badala ya kuwa faraja kwa kweli *FAT* imeweza kutuletea migongano mikubwa sana. Sasa ni nini kinapelekea kuleta matatizo haya? Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema lakini nikianzia kwa Wizara kwa sababu msisitizo mkubwa umekuwa kwa mchezo ya mpira wa miguu, nafikiri michezo yote ni muhimu na ilitakiwa itiliwe mkazo. Lakini nini ambacho kimepelekea sasa ni kwamba hatuna sheria ya kuboresha michezo na ndio maana tunayumbayumba. Ndio maana mtu anaweza kufanya vitu vyake bila kuwa na kifungu ambacho kingeweza kumchukulia hatua.

Kwa hiyo, napendekeza angalau kuwe na sheria ya kuboresha michezo kwa sababu sheria hii itaweza kusimamia vizuri sana michezo na kuzingatia michezo ya aina zote na mtu ataogopa kukiuka sheria hii ambayo itakuwa imewekwa katika sheria za kuboresha michezo. Kwa hiyo, hili ni pendelezo langu ambalo nafikiri lingeweza kusaidia katika kuboresha shughuli nzima ya michezo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kwa upande wa *FAT*, malalamiko mengi yanatokea na kila mtu anasema anayehusika inafaa tusimtaje kwa sababu kanuni haituruhusu hataweza kujitetea lakini nini ambacho kinapelekea hili, kwa sababu mengi tunayasoma kwenye magazeti, wanachama wanalamika, kikubwa ni kwamba taratibu hazifuatwi.

Kwa mfano, Mkutano Mkuu wa *FAT* mpaka sasa haujafanyika, kila mwaka lazima mkutano ufanyike ili wanachama wawe na nafasi ya kutoa malalamiko yao na kama kubadilisha uongozi ndio nafasi yao kubwa ambayo wangeweza kuitumia. Mpaka sasa hatuoni hata kama uhalali wa Katiba wa wao kuwepo kama upo sina hakika lakini ninavyofahamu kwa upeo wangu nilionao nafikiri Katiba haipo kwani mwisho wake mwezi wa nne ndio ilikuwa iwe mwisho. Kwa hiyo, Mkutano Mkuu ungeitwa ufanyike haraka ili sisi wanachama au wapenzi wa michezo tupate nafasi ya kutoa yale ambayo tunafikiri yataweza kuboresha michezo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie na kuipongeza Serikali ya Chama cha Mpinduzi katika Ilani ya Uchaguzi kuamua kwa makusudi mazima ya kujenga Uwanja wa Kimataifa wa Michezo Dar es Salaam. Bila kumsahau Mbunge wa Jimbo la Temeke kwa juhudini kubwa ambazo amekuwa akizifanya ndani ya Bunge na nje ya Bunge katika kuhakikisha kwamba Uwanja huu unajengwa Temeke. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa tumeambiwa kwamba mwezi Juni, 2005, uwanja ule utatakiwa uwe umekamilika. Nina wasiwasni kwa sababu na hii migongano ambayo inatokea na tunategemea uwanja uwe mzuri, wa Kimataifa na vitu vingi vijengwe. Sasa sijui naomba Waziri atakapokuwa anajumuisha anieleze ni mkakati gani ameuweka kuhakikisha kwamba kweli mwaka 2005 uwanja huu utakuwa umekamilika na utakuwa umeanza kutumika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa upande wa michezo, ningeomba nipewe ufafanuzi na Waziri kuhusu mahesabu ya *FAT* kwamba ni nani anayakagua na taratibu za ukaguzi, taarifa zinapelekwa kwa nani ili wanachama wawe na imani na michango yao na fedha ambazo zinatolewa na *FIFA* na viingilio ambavyo vinatolewa na wachezaji au na timu mbalimbali. Kwa hiyo, hili ningeomba Mheshimiwa Waziri alitoe wakati anajumuisha kwenye majumuisho yake tuwe na taarifa kwamba ukaguzi unafanywa na taarifa hizi zinapelekwa wapi na wanachama kweli wanapewa taarifa hizi wakati wa mukutano mkuu wa *FAT* unapofanyika. (*Makofî*)

Baada ya kuchangia upande wa michezo ningeomba nihamie kwa upande wa ajira kuhusu migongano ambayo inajitokeza mpaka sasa. Kwa kweli ni jambo ambalo linatusikitisha sana. Hata jana nilikuwa nasikiliza kwenye vyombo nya habari, nilikuwa sina taarifa kwa sababu muda mwingu tumekaa hapa Dodoma kwamba wafanyakazi wa *TES* wamekuwa wakilala nje kwa muda wa wiki mbili wakisubiri malipo yao. Sasa unashindwa kuelewa ni vipi wananchi wameweza kupoteza imani yao kwa Serikali yao. Kwa sababu kauli za Serikali zimekuwa zikitoka kwamba mwende, msubiri mafao yatalipwa lakini wamekuwa hawaamini. Hawajaona ni vipi watalipwa ndiyo maana wameamua kulala pale. Sasa hii imani tutairudishaje kwa wananchi wetu, kwa wafanyakazi wetu, kuhakikisha kwamba mafao yao yanalipwa kwa wakati muafaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini huko nyuma kulikuwa na ile *ownership* kwa sababu yale mashirika yalikuwa ni ya kwetu, mtu unaona kwamba hii mali ni ya kwangu. Kwa hiyo, unafanya kazi kwa uchungu na ukiwa unafanya kazi kwenye shirika kama *TANESCO*, *TTCL*, mkikaa unaona kabisa unatetea *TTCL* au mwajiri wako. Sasa kwa kukosa ule uaminifu, uzalendo na uhakika kwamba nani ananufaika na hiki na wafanyakazi ndiyo wanaosikia yale ambayo yansemwa na hawa waajiri na kashfa mbalimbali za waajiri hawa ambao labda ni wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kero zote hizi wao ndiyo wanaozipata kwa karibu na wanatoa kilio chao, lakini hawaoni ni vipi Serikali inasimamia. Sasa *NBC* juzi mpaka benki zimefungwa, lakini minong'ono ilianza muda mrefu kwamba kuna migogoro *NBC* na *NMB* sasa inakuja. Je, Serikali kwa mini hiki kitu isifanyie tafakari mapema na kujua ni vipi matatizo haya yanaweza kutatuliwa mapema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwamba hili limekuwa ni fundisho kwetu kwa mashirika yote ambayo tunabinafsisha. Wizara yako Mheshimiwa Waziri nafikiri ndiyo iwe ya kwanza kuzingatia kwamba ni vipi mafao ya hawa wafanyakazi yatakuwa yamechukuliwa na watalipwa vipi kabla shirika halijaanza kubinafsishwa badala ya kuanziwa wabinafsishaji, kwanza hii inawanyima haki wafanyakazi, inawanyima imani kwamba kweli watalipwa haya mafao.

Kwa mfano, tuchukulie shirika la *NBC* mwaka 1997 wakati linaingia kwenye *NBC* (1997), wafanyakazi waliombe kwanza mafao yao halafu waanze Mkataba mpya lakini nafikiri hawakulipwa na ndicho kinachokwenda *TRC* nafikiri hata *SUMATRA* na *TTCL*. Nafikiri ni vizuri mngejua kwamba wafanyakazi wanapenda kwanza walipwe mafao yao. Mwajiri mpya au utawala mpya unapokuja waanze upya na Mkataba mpya, hii itawezza kutupunguzia migogoro kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, ningeomba nitoe mapendekezo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nichangie kwa upande wa vijana. Kwa kweli kundi la vijana ni kubwa sana na ni nguvu kazi kubwa kwetu. Lakini ajira imekuwa ni tatizo. Waziri yeye ni Mbunge wa Jimbo anafahamu kabisa kwenye mikutano yake akitembelea ziara kwenye Vijiji vyake jinsi kundi kubwa linavyokuwa mbele yake na kuhangainka na kulalamika ni vipi wanaweza kumudu maisha yao. Wamekimbilia Mjini hawapati nafasi ya kufanya kazi.

Sasa huko walipo tungeomba sana Wizara ifanye utafiti au itafute utaratibu gani utumike ili kuweza kuboresha maisha ya vijana hawa. Pamoja na juhudhi ambazo wanazifanya upande wa *VETA*, vyuo vipo lakini mwenzangu kama Mheshimiwa Venance Mwamoto amechangia na mimi nilikuwa na hiyo hoja kwamba wale ambao wanafanikiwa kwenda kwenye Vyuo vya *VETA*, basi wakimaliza wapewe na nyenzo za kwenda kufanya kazi. Hata kama Serikali haina uwezo basi kwa kukopeshwa ili wakienda kwenye Vijiji walivyotoka itakuwa ni changamoto au ni ajira kwa vijana wenzao ambao hawakupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, hili ningeomba liangaliwe kwa karibu sana kwani katika kila Kijiji au Mijini vijiwe vimejaa na kwenye vijiwe hivi hakuna mambo muhimu ambayo yanaleta maendeleo kwao bali ni katika kupotoshana kimaisha na kuangalia ni vipi wanaweza kwenda nchi za nje, ni vipi wanaweza, wanasema ni store away na ni vipi wanaweza kujaribu kumwibia mzazi ili aweze kutoroka kwenda *South Africa* au nchi nyininge kwa ajili ya kuhangainka na maisha.

Kwa hiyo, kwa kweli ningeomba sana Wizara iliangularie kundi hili la vijana ili wawawezeshe. Hii mikopo ya milioni tatu kila Wilaya haisaidii kitu kwa kundi kubwa la vijana kama lilitivo bila kuwasahau walemaru, kwa kweli walemaru ningeomba sana Mheshimiwa Waziri uwaangularie kwa undani katika kuwawekea mazingira mazuri ambayo yatawasaidia wenzetu hawa kuweza kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri ulemavu mwangi unawafanya waweeze kufanya kazi zao wenyewe. Kwa hiyo, tuwatafutie sehemu au mazingira mazuri ambayo yatawawezesha wao kumudu maisha yao ya kila siku na kuweza kujajiri. Hii ni pamoja na wazee, wenzangu wamelizungumzia hili kwamba hatuna utaratibu kama nchi zilizoendelea kuwawekea wazee katika nyumba maalum, sana sana tulizonazo sasa ni taasisi za kidini ndizo zinazoshughulikia suala hili.

Sasa kwetu kifedha hatuna uwezo, lakini basi tujaribu kuweka utaratibu kama tulioweka wa vijana na akina mama kuona ni vipi ambavyo tutaweza kuwasaidia wazee hawa nao waweeze kumudu maisha yao wakati wa uhai wao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba nikushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofsi*)

**MHE MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kuweza kunipa muda wa kuweza kuchangia kabla ya saa saba. Pili, napenda kumpongeza Waziri mhusika wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu wake Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na wataalam wote wa Wizara hii kwa kuweza kutuandalia hotuba nzuri inayoleweka, inachobidi sasa ni kuitafsiri hotuba hii katika vitendo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi ningependa kumpongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, kwa kupitia shirika lake la Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*) kwa kuwa mstari wa mbele kusaidia makundi ya jamii yenyeye matatizo maalum kama watu wenye ulemavu, watoto yatima na mengine yote kwa michango yake mikubwa.

Mimi binafsi mwezi Februari, 2003 alinishirikisha na akaniidhinisha *wheel chairs* 130 ambazo ilibidi nizigawe Mikoa yote 25 kwa *ratio* ndogo ndogo, lakini cha kupewa ni cha kupewa na kwa kweli niliweza kumshukuru sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo kwake, nichukue nafasi hii kuwapongeza au kuwashukuru Wabunge wa Viti Maalum, kwa sababu ndio waliopeba jukumu la kusafirisha *wheel chairs* hizo kupeleka Mikoani wakishirikiana na watu wenye ulemavu wakagawa jinsi walivyoona inafaa. Kwa kweli niwashukuru sana na hiyo inanipa moyo kwamba nipo pamoja na Wabunge wenzangu katika kuliona

suala la watu wenyе ulemavu kwamba sasa lina msingi na ni haki ya kijamii kwamba kila mmoja anapaswa kushiriki. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo napenda nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Wizara inashughulikia Vyuo vya mafunzo stadi kwa watu wenyе ulemavu. Mchango mzuri upo, lakini ningependa kuiuliza au kuishauri Wizara kwamba katika vyuo hivi kuna matatizo mengi. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia hakuna, waalimu wa kutosha hakuna, hata wakati mwengine chakula cha kumudu kula wale wanafunzi ambaо wanakaa mabwenini ni shida. Sina uhakika kama Wizara mpaka sasa hivi ina habari ya Chuo cha Mirongo Mwanza kwamba kuanzia mwezi wa nne wale wanafunzi wa bweni walipewa likizo ndefu kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Watu wenyе ulemavu wanahitaji mafunzo hayo na ustadi huo kwa sababu kama Chama cha Mapinduzi kilivyoelekeza katika Ilani yake ni njia mojawapo ya kuwasaidia kuweza kuwijiri.

Sasa kama vyuo vinafungwa katikati ya muhula na Aprili ilikuwa ni katika mpango wa Bajeti ya mwaka jana ambayo tulipitisha hapa, sijui ilikuwa ndogo sana kiasi kwamba chuo kikabidi kifungwe mapema, mimi hilo ningependa kulifahamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba tujaribu kuangalia kwa kina zaidi Vyuo hivi kuweza kuvipatia fedha zinazotosha ili viweze kuijendesha.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo ningependa nijikite kwenye suala la Sera ya Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu. Hili mimi ninasikitika kwa sababu huu ni mwaka wangu wa tatu nasema hili kila wakati wa session ya Bajeti. Mwaka jana katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 15 ilielezea hili na mwaka huu ukurasa wa 15 yamerudiwa tu maneno yale yale, Wizara itaandaa sera, Wizara itakamilisha, ni miaka mitatu, itaandaa, itakamilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kweli mimi niseme kwa hili kinaniuma sana kwa sababu inavyoelekea sera hii mimi sijui kwa nini inasua sua kumalizika kwa sababu *other disadvantaged groups* mbona sera zao zimeshakamilika. Sera ya wazee ilikuja nyuma, nimeisoma hapa kwamba ipo tayari, haya wenzetu waliopo kwenye Wizara zingine kama Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wana sera zao, wanawake na watoto wana sera zao. Hivi watu wenyе ulemavu kuna tatizo gani? Au ukamilifu wa sera hii unahitaji dola za nje kuweza kukamilishwa? Mimi sifahamu. Kwa kweli kwa msingi huo kwa sababu ni jambo ambalo ninalirudia, nimelirudia na maandishi yanabadilishwa tu, itakamilisha, itakamilisha, mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, nitaomba maelezo ya kina na ukweli wa jambo hili wakati wa kujumuisha vinginevyo nislazimishwe kutoa shilingi katika sehemu ya *policy* na mengineyo. Tafadhali sana, kwa sababu inasumbua na sera ndiyo msingi wa mwongozo wa utendaji wa masuala mbalimbali ya kitu chochote kile. Sera hiyo ndiyo itafanua watu wenyе ulemavu wasomeje, wasaidiweje, wakopeshweje kiasi kwamba Wizara zingine zina *take off* kutokana na maaazimio au miongozo ambayo ingepatikana kutokana na sera hiyo na kanuni zake na hivyo kuwa na sheria ambazo kwa kweli zingeweza kuelekeza kundi hili la watu wenyе ulemavu liweze kuwa treated namna gani. Kinyume chake mambo yanafanyika kama hisani kumbe ni wajibu wa jamii kuyatekeleza hayo kwa sababu ya hali halisi ilivyo.

Kwa hiyo, tafadhali sana ningeomba ufanuzi, vinginevyo nisije nikalazimika kama nilivyosema kuondoa shilingi ambayo haipendezi kwa sababu Chama changu cha Mapinduzi katika Ilani yake imefanuua suala hili, kwa hiyo ni wajibu wa Serikali kutekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kulikuwa na utaratibu wa Vyama vya Watu wenyе Ulemavu kupata ruzuku hiyo miaka ya nyuma. Sasa hapa, labda nimepitwa na wakati, niombe tu ufanuzi hivi utaratibu huu bado upo au umekwisha au umefutwa? Kwa sababu kimsingi sasa hivi Vyama unaweza ukakuta vinapewa 50,000/= kwa mwaka mzima kuweza kuijendesha. 50,000/= ni fedha kidogo sana, kwa hiyo sasa sijui Wizara iongezewe bajeti au kwanza nifahamishwe kama utaratibu huu upo au haupo. Nisije nikawa ninasema kitu ambacho labda hakipo kwenye utaratibu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hilo nataka kufahamu ni kwa kiasi gani Serikali chini ya Wizara imejaribu kuweka utaratibu au mikakati ya kuweza kuboresha maisha ya watu wenyewe ulemavu hasa kwa kupitia ile taasisi ambayo sisi ni wanachama. Taasisi ya Marekebisho ya Watu Wenye Ulemavu Barani Afrika, sisi ni wanachama. Je, mpaka sasa hivi baada ya kujunga ndani ya Taasisi hii Wizara ina mikakati gani ya kuboresha maisha ya watu wenyewe ulemavu hasa katika kipindi hiki cha Muongo wa watu wenyewe ulemavu wa miaka kumi amba Muongo huu uliana 1999 na utaisha 2009? Miaka inapita, kwa hiyo ili angalau pawe na *impact* ya kuweza kuonyesha kwamba Muongo huu ulikuwa wa manufaa, ningeshauri Wizara ifanye itakavyoweza kufanya kwa kushirikiana na taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Wizara kuendelea kuandaa taratibu za kuweza kuridhia utaratibu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Fursa sawa na Haki kwa Watu Wenye Ulemavu. Hili nalo ni wimbo, mwaka jana iliandikwa hivyo hivyo naomba ninukuu: "Wizara itaandaa taratibu za kuwezesha Serikali kuridhia na kuendelea... Mwaka huu imeandikwa hivyo, ni yale yale ita, ita, ita.

Mheshimiwa Spika, kipengele hiki ni muhimu kwa sababu ndani ya Fursa Sawa kwa Watu Wenye Ulemavu, Umoja wa Mataifa umejaribu kuelekeza Mataifa husika yafanye nini kwa mwelekeo gani kuhusu huduma za watu wenyewe ulemavu katika nchi zao. Kwa hiyo, hili linaendana na sera. Labda nitaambibi baada ya sera ndiyo itakuja fursa au baada ya fursa itakuja sera, hapo nitaomba niweze kusaidiwa kiukamilifu. Kwa ujumla kwa sababu kama wengine walivyoweza kuzungumza Wizara hii kwa kweli ina mambo mengi sana tangu mtoto, ndoa zinazoteteka wahudumie wao, wazee wahudumie wao, vijana wahudumie wao, ajira wahudumie wao, *VETA* na mengineyo. Kwa kweli Wizara hii ina mzigo sana. (*Makofî*)

Kwa msingi huo nashauri kwamba labda wakati umefika kuweza kuangalia, kupanga upya kazi za Wizara hii vinginevyo wanalemewa na Bajeti yake ni ndogo. Tutaendelea kuwalaumu lakini labda kazi ni nzito sana na mimi napendekeza kwenye sehemu yangu ya watu wenyewe ulemavu iweze kuhamishwa labda ipelekwe kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, ambaye labda ata-*delegate* Wizara zingine zote katika shughuli zao kuweza kuangalia mambo ya watu wenyewe ulemavu yafanyweje yaani iwe jumla, ndiyo maana Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, haiwezi kum-*dictate* kwa mwenzake afanye kitu gani, hilo lilikuwa pendekezo langu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa pongezi kwa Serikali na Wizara kwa kushirikisha timu za watu wenyewe ulemavu mwaka 2002, pale Walemaru wa mchezo wa kuinua Vitu Vizito walikwenda Manchester, walishinda na mwaka huu kama iliyoelezwa na wenzangu timu ile ya *Olympic* Maalum wamekwenda na wameshinda wakawa wa pili kati ya nchi 160, wakarudi na medali 18 na kati ya hizo nne ni za dhahabu. Ni mafanikio makubwa na hii mimi inanipa faraja kuonyesha kwamba watu wenyewe ulemavu wana vipaji na wanaweza kama wakiwezeshwa.

Kwa hiyo, hapa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika kuchangia hasa timu hii iliyokwenda Ireland mwezi Juni, 2002 kwa kucheza mchezo ule na Mabalizi na fedha zilizopatikana ndizo zote zilisaidia ku-*sponsor* timu hii na nashukuru Mungu haikuibisha Taifa, imeweka ramani mpya, Tanzania imesifika, inafahamika, tuendeleze wadau wote kuwezesha timu mbalimbali. (*Makofî*)

Kingine ni marekebisho ya sheria. Kama wenzangu walivyosema sheria za kazi na matunzo kwa watu wenyewe ulemavu zimepitwa na wakati. Hivi nikizungumzia za watu wenyewe ulemavu kiasi kwamba ilikuwa asilimia mbili ya waajiriwa katika sehemu za kazi wawe walemaru.

Mheshimiwa Spika, hiyo sasa haiwezekani, ajira haiko sana Serikalini, ipo kwa watu binafsi na huwezi kuwalazimisha kutekeleza hilo. Ile ya matunzo iliyositisiza kuwa watu wawekwe makambini, makambi yenyewe mpaka sasa hivi kuyamudu ni shida. Watu wasiojiweza wanaokaa makambini hali ni mbaya. Hakuna huduma ya kutosha hata kidogo, chakula, malazi hakuna. Inawapasa watoroke kutoka makambini kwenda kuombaomba Mjini. Sasa hizi Sheria zinatusaidia nini? Wakati umefika tuweze kuzibadilisha kwa sababu kwa kweli zimekwishapitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana. Wapo na vijana wenye ulemavu. Ninashauri katika mikopo ambayo Wizara hii inatoa pamoja na uchache wake ishirikiane na TAMISEMI kuhakikisha kwamba vijana wenye ulemavu katika Wilaya na Halmashauri nao wanaweza kukopeshwa. Kuna malalamiko mengi ambayo nimeyapata, wanasema wao wanatengwa, hawafikiriwi na zile Kamati.

Kwa hiyo, naomba Serikali na hapo labda nihimize Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambaa kwa kiasi fulani ni Madiwani katika Kamati zetu hizi hili nalo mliangalie kwamba lina umuhimu wake. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo kuhusu michezo, nishukuru kwamba Serikali na hasa chini ya uongozi wa Rais wetu imesisitiza ujenzi wa uwanja mpya wa michezo. Imedhihirika hapa kwamba walemau wanaweza kucheza kwa sababu wameshaleta medali kila wanapokwenda nje.

Sasa kiwanja hicho michoro yake ihakikishwe kwamba inakidhi haja ya michezo mbalimbali ya watu wenye ulemavu, inakidhi haja ya sehemu zao watakazokaa kuwaangalia na kufurahi. Inakidhi haja ya sehemu za maliwato watakazopaswa kuzitumia hao wanatimu, wanapojiandaa kuingia ndani ya sakata la michezo yoyote ile. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli mimi yangu ni kushauri lakini nasisitiza kuhusu Sera ya Watu Wenye Ulemavu. Hivi kweli itaendelea kukamilishwa, kukamilishwa kwa miaka mingapi ijayo? Kwa suala hili kwa kweli sitakuwa na suluhu, sasa nitaunga mkono hoja lakini wakati wa kupitisha vifungu kwa vifungu wala isiwe jumla.

Mheshimiwa Spika, hata ikiwa jumla mimi hapa nitasimama kama majibu yatakayokuwa yametolewa hayaniridhishi nitatoa shilingi yangu niende nayo mpaka kesho kutwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja kwa sasa hivi nikisubiri maelezo ya mwisho. Nashukuru kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. (*Makofsi*)

**SPIKA:** Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo tumefikia mwisho wa kikao cha asubuhi. Watakaochangia mchana, walikuwa wengi ambaa wamechangia mara moja tu au mara mbili tu na bado katika hao waliochangia mara mbili ninao watatu ambaa watachangia mchana nao ni Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki na Mheshimiwa Zahor Juma Khamis. Huwa tunapanga wanen hao ni watatu, kwa hiyo, katika waliochangia mara tatu nimetoa nafasi moja tu kwa Kiongozi wa Upinzani Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, wengine waliokwishachangia mara tatu na nne kwa kweli wachangie kwa maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kuna tangazo kwamba leo jioni baada ya kumaliza kikao cha jioni baada ya kuahirisha Bunge mpaka kesho Benki ya CRDB wameniomba niwaalike Wabunge wote waliopo, kwenye hafla ya uzinduzi wa shughuli za *Tembo Card* ambayo wataifanya jioni hii.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mliopo mnakaribishwa kwenye viwanja vyetu vya kawaida vya burudani ili kushuhudia uzinduzi wa hizo shughuli za CRDB za *Tembo Card* pamoja na mengine waliyoyaandaa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.54 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kwa jioni ya leo kwa ajili ya kuchangia katika Wizara ya Kazi, Maendeleo na Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba na mimi niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Sir George Kahama na familia yake kwa kufiwa na mwanaye na Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi yao nzuri ambayo inaonekana kuitia kwenye hotuba yao ya leo, ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri, nawapongeza sana. Ni hotuba nzuri, yenye kutia matumaini na yenye kuleta mwelekeo na hasa kwa wakati huu ambapo ndiyo tunakazana sana katika kujitoa kwenye hili lindi kubwa la umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi, naomba basi nichangie kidogo katika yale ambayo mimi labda nina matatizo nayo au ninapenda niyajue na kufahamu katika Wizara hii. Machache katika hayo na hasa langu ni moja ambalo ningependa nilichangie katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida tuna Chuo cha *VETA* kidogo kimoja kiko Singida Mjini. Chuo hiki kipo kwenye majengo ambayo yalikuwa ya shule kwa wakati huo yakiitwa *Middle School*, ambapo yalikuwa ni ya darasa la tano mpaka darasa la nane. Kwa kweli ni ya muda mrefu na ya miaka ya 40 au 50 huko na ni majengo ya zamani kiasi kwamba yameshachoka. Lakini Chuo hiki ndiyo kipo pale na bahati nzuri kwa sababu kinachotoa huduma hii, ndiyo maana tumelazimika kuendelea nacho mpaka sasa hivi. Majengo yake kwa kweli yamechoka kwa sababu ni ya muda mrefu na ni ya matope. Halafu ni majengo madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imelazimika katika majengo mengine kuhamisha walimu ili kuweza kupata majengo ya kuwaweka wanafunzi na kuyafanya kama mabweni. Lakini hata hivyo ni madogo, kwa hiyo yanatu-*limit* sana katika kuchukua idadi ya wanafunzi wanaotakiwa pale. Tungependa kuwa na wanafunzi wengi, lakini tunakuwa *limited* na majengo machache yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo haya ya shule kwa sababu ni ya zamani hata eneo limezingirwa na makazi ya watu. Kwa hiyo, eneo la Chuo limebakni eneo hata kwa shughuli ambayo itatakiwa ipanuliwe pale imekuwa pia ni *limited*. Sasa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, nimeona kabisa akisema kwamba, kutakuwa na ukarabati na kupanuliwa kwa Vyuo vya Ufund Stadi, akavitaja pale pamoja na Singida. Lakini nachelea kusema kwamba, kwa sababu ukiangalia kile Chuo sasa hivi kwa ukarabati au kwa upanuzi wowote, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, badala ya kuyafanya ukarabati angeyabomoa na kuwajengea majengo mengine mapya. Kwa sababu hayawezekani kufanyiwa ukarabati kwa sababu ni ya zamani sana na halafu ni ya udongo sasa hata namna ya kuyafanya ukarabati haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati mmoja Mheshimiwa Waziri alitutembelea na alifika katika kile Chuo akatoa ahadi moja ambayo nimeangalia katika Kitabu cha Hotuba yake pamoja na vile vitabu vya Bajeti sijaona. Sasa namwomba basi baadaye wakati ana-*wind up* anisaidie alituahidi kwamba, pamoja na kile Chuo ambacho kipo, lakini kwa sababu ya majengo ambayo yamechoka pamoja na eneo ambalo ni dogo aliahidi kutujengea au kutupa msaada mwingine wa kujenga majengo mengine mapya. Kwa msaada huo au kwa ahadi hiyo tumeweza kutafuta eneo moja pana na kubwa ambalo ni njie ya sehemu hiyo kilipo kile chuo. Sasa kwa sababu sijaona hapa na sisi tayari tumeshatafuta eneo lisilopungua eka kama 20, ambalo ni la wazi na ni zuri kwa kujenga majengo mengine kwenye nafasi nzuri. Sasa tukiangalia na kujua kwamba, sasa hivi stadi zinazotolewa ni za kisasa kwa kuzingatia soko la ajira lililopo sasa hivi. Kwa hiyo, tumeipata nafasi ya kupata eneo moja zuri. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, ni wapi ambapo ahadi yake ile aliyoitao ameiweka katika Vitabu hivi. Aidha, katika Kitabu hiki hapa siioni, labda katika Vitabu vya Bajeti kuna mahali ambapo ameweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu hata wafanyakazi walioko pale wana matatizo ya mahali pa kuishi, hawana nyumba za kuishi na kwa sababu hakuna eneo basi hakuna namna ya kuweza kujenga. Sasa kwa sehemu ambayo tumeifikiria na tumeipata baada ya kutuambia ni sehemu

kubwa inayoweza kuzingatia mahitaji yote haya ya kujenga Chuo na mahitaji ya kujenga nyumba za kuishi na karakana zote ambazo zinahitajika. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, baadaye ikiwezekana basi anisaidie kunifafanulia au kunielekeza ni wapi mahali ambapo ulipotutengea ahadi yako ambayo ulituambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande mwagine, Waheshimiwa Wabunge, wameendelea kuchangia kuhusu masuala ya michezo. Kama ilivyo kawaida ama walivyozungumza wenzangu ni kwamba, Tanzania kwa muda mrefu, kidogo hapa katikati angalau tulikuwa tumeonekana kama tunajitoa kwenye kichwa cha mwendawazimu. Lakini inaonekana tena kutoka pale tumerudi tena kwenye kichwa cha mwendawazimu si kwenye mpira wa miguu, si kwenye riadha, si kwenye ngumi, si kwenye chochote kile. Kila tunapokwenda kwenye mashindano sisi ni watu wa mwisho au watu wa kubabaishababaisha. Lakini katika kubabaisha huko ndipo tunapoteza fedha. Maandalizi yetu ya michezo hii yote si kwenye mpira wa miguu, si kwenye riadha, yamekuwa ni kama maandalizi ya zimamoto ya haraka haraka. Tukiambiwa tunajikuta hatuna maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile hatujui ratiba ya michezo hii, wakati tunajua ratiba ya mpira wa miguu, tunajua ratiba ya michezo ya riadha, lakini maandalizi yetu mara nyingi kwa mfano, kama sasa hivi Simba ndiyo imekwenda kule Zanzibar kwa ajili ya maandalizi ya kwenda kwenye mashindano. Sasa wiki moja, wiki mbili, wakati wenzetu hutumia muda mrefu sana wanajiandaa kwa ajili ya mashindano haya. Lakini sisi tunapeleka timu kwenda kufanya mazoezi kwa muda wa wiki moja, tunapeleka timu ya riadha labda kwenye mazoezi au ya ngumi kwa muda wa wiki mbili. Sasa hii kweli Mheshimiwa Waziri, tutafika mahali tutaondokana na suala la kuambiwa kichwa cha mwendawazimu. Kila siku tutakuwa ni kichwa cha mwendawazimu kwa sababu hatuzingatii yale yote ambayo tunatakiwa tuyafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na matatizo tuliyonayo katika uongozi wa michezo, mimi ningeomba pia maandalizi yetu katika michezo yetu yawe ni ya kutosha. Inawezeekana tukawa tumekalia kitu kimoja cha kusingizia pengine masuala ya uongozi peke yake, tukajisahau je, ni viyi tunajiandaa katika michezo yetu hii. Sasa pamoja na uongozi mbovu wa michezo na hasa kwenye michezo wa mpira, basi nimwombe Mheshimiwa Waziri, hebu tujiandae vizuri katika michezo yetu kwa muda muafaka, ili tusiwe tunaibika. Ni Taifa kubwa lenye watu wengi zaidi ya watu milioni 34. Sasa unakuta nchi nyingine zina watu wachache lakini unakuta ndiyo wanafaalu katika michezo kwa sababu wanawekeza katika michezo. Michezo sasa hivi ni siasa, michezo sasa hivi ni uchumi na michezo sasa hivi ni kufahamika kila mahali. Sasa sisi tunaidharau michezo, lakini ndiyo hivyo tunajikuta tunafanya vioja wakati tunaheshimika katika dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, kwa kweli sikuwa na mengi ya kuzungumza, nilitaka nitoe ujumbe katika masuala hayo mawili. Kwa hiyo, natamka wazi kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa jioni ya leo. Kabla sijaendelea ningeomba niunge mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya na vilevile kwa kuanda hotuba hii ambayo kwa kweli inaonyesha wapi tunapotoka na wapi tunakoelekea. Kwa hiyo, nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Wizara hii mimi nasema ni Wizara ambayo inabeba mzigo mzito sana. Kwa sababu mambo yote ambayo kwa kweli yana matatizo yako katika Wizara hii. Ukiangalia suala la walemau lipo katika Wizara hii, ambalo nalo vilevile ni matatizo makubwa. Ukiangalia suala la vijana na hasa vijana watukutu na vijana wenye tabia mbaya mbaya liko kwenye Wizara hii na vile vile suala zima la wafanyakazi. Kwa hiyo, mimi nasema Wizara hii ina kazi nzito na kazi ngumu sana. Lakini bado kwa jitihada zao na jinsi wanavyofanya kazi vizuri, wanajitahidi kwa kweli, naendelea kuwapongeza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi sana ya kuchangia, ila nitachangia kwa kifupi sana. Mimi nilikuwa naomba nichangie kuhusu suala la michezo. Suala la michezo kwa vijana kama tunavyofahamu, kijana ni kijana hawezu kukaa akatulia, hawezu kukaa akafanya vitu ambavyo pengine sisi tunadhani anaweza akafanya vizuri zaidi. Lakini unapokuwa kijana wote ndiko tulikotoka, unakuwa na mambo mengi ya kuchanganyika. Vijana wetu katika umri wao wanahitaji kufanya vitu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kwa kweli ningeomba nzungumzie juu ya suala la wazazi. Malezi ya vijana wetu tuliyonayo kwa kweli bado si mazuri sana na nikianzia na suala la michezo lenyewe. Vijana wanahitaji wacheze michezo kama vile mipira, michezo ya ngoma na michezo ya aina mbalimbali. Lakini jambo la kushangaza na la kusikitisha mimi kama mzazi, kwa kweli hili ningeomba nilisemee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vijana sasa hivi wamejitoa mhanga katika kucheza michezo mbalimbali na hasa ukiangalia kwenye Televisheni, siku hizi kumekuwa na vikundi nya dansi au bendi, lakini pamoa na kwamba shughuli hizo wanazozifanya za michezo ni ajira. Lakini jambo la kushangaza na la kusikitisha ni kwamba vijana wetu hawa hasa vijana wa kike ni kwamba, mavazi wanayovaa wakati wanapocheza si mazuri. Sasa sijui ni wale wanaoanzisha hivyo vikundi, ndiyo wanaweka mashinikizo hayo au ni wao wenyewe wanapenda. Uizingatia hasa wasichana, unakuta vijana wa kiume wanavaa nguo nzuri sana. Lakini jambo la kushangaza ni kwa vijana wa kike, ni jambo la kusikitisha wanavaa nguo ambazo si za heshima. Kwa sisi wazazi sijui tutumie utaratibu gani na sijui Wizara itumie utaratibu gani. Lakini vijana wetu kama wangkuwa wanavaa nguo za heshima, nadhani ni vizuri basi wale amba wanaoanzisha hivi vikundi walione hilo. Si vizuri binti wa kike anavaa kaptula imefika huko juu na fulana imefika katikati, tumbo liko wazi na sehemu zote za mwili ziko wazi. Sasa sina uhakika watu wanaoangalia hivyo vikundi wanafurahi, sijui kama ni wote wanafurahi. Mimi kama mzazi, sifurahishwi hata kidogo na kama kuna mzazi humu ndani na ni kweli tunaangalia wote lakini ni wangapi wanafurahi mimi sina uhakika, nadhani wazazi wengi tunakasirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba Wizara ijaribu kuliona hilo. Kwani kuna ubaya gani wakivaa nguo za heshima wakacheza muziki, mbona inafurahisha zaidi kuliko kuva ovyo ovyo. Mimi nasema wanavaa ovyo ovyo na mimi napenda wale vijana wanisikilize na kama wanansikia kwa kweli wanavaa ovyo ovyo na wala hawavai nguo za heshima. Wavae nguo za heshima na wacheze muziki vizuri na waweze kueleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutafuta wachumba na nini, kwa kweli hawatafutwi kwa kuva nguo zisizo za heshima. Ukvaa nguo ya heshima ndiyo akina baba watakutafuta na watakupenda. Lakini ukivaa nguo za ovyo ovyo, mimi sipendi na hata barabarani vijana wetu wanavaa nguo zisizo za heshima. Jambo la kushangaza vijana tunawalea wako nyumbani wanatoka majumbani mwetu, lakini wazazi tuko tayari tunawaacha watoto wavae nguo ambazo si za heshima. Mimi napenda vijana wa kike wavae suruali, hata mimi navaa suruali na ni nguo nzuri na ya heshima. Lakini ukiivaa ikakukaa ni nzuri, inapendeza sana. Lakini vijana wa kike wanavaa suruali ambazo zinawabana mwili mpaka mtu anashindwa hata kutembea. Kweli jamani naomba Wizara angalau siku moja itoe hata kauli ya kukemea hayo. Watanzania tuko makabila mengi sana, tuna ngoma nzuri za utamaduni ambazo kwa kweli zinapaswa kuimariswya. Kwa mfano, nichukulie ngoma ya hapa Dodoma tuko Wagogo, Warangi, Waburunge, Wasandawe na Wamasai wapo, lakini tunacheza ngoma nzuri za utamaduni na zinapendeza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshawishi sana vijana wetu wanaoanzisha vikundi hivi hebu wajaribu kurudi kwenye utamaduni wao, vinginevyo tutaanza kurukaruka ovyo. Vijana watapoteza utamaduni wetu na matokeo yake mwisho tutakuwa makabila ambayo hayana utamaduni hata wa michezo, hata wa ngoma na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nzungumzie suala la utaratibu wa Ma-*miss* huu. Hivi huu u-*miss* lazima uvae nguo za kuonyesha mwili ndiyo uonekane wewe ni *miss*. Kwa nini tusiwe na utaratibu mzuri, wale amba wanaotengeneza zile kanuni za kuingia kwenye u-*miss* na kutoa *marks* kukawa na kanuni za kuva nguo za utamaduni, kwa nini tung'ang'anie vitu ambavyo vimeletwa na wenzetu, kwa maana tunaheshimu mila na desturi za wenzetu kuliko zetu wenyewe. (*Makofi*)

Naomba Wizara ibadilike maana ni sisi wenyewe ndiyo tunapaswa kuwababilisha vijana wetu wa Tanzania na wala si watu wengine na wala si Taifa lingine. Tukiwaacha vijana wetu waendelee kuiga vitu vya watu wengine maana yake ni kwamba, mavazi yetu yatapotea na heshima ya vijana wetu itapotea. Kwa hiyo, ningeomba Wizara hebu ijaribu kutengeneza taratibu nzuri za mashindano hasa kuhusu hizi taratibu za mashindano ya *u-miss*. Hata sisi juzi tulishindana hapa kwenye viwanja vya Bunge, basi watuige sisi mama zao tulivyofanya. Tulivaa vizuri hata pamoja ni watu wazima lakini tulipendekeza na watu wakafurahi. Sisi tulivaa vizuri hata kama ni watu wazima lakini tulitoka na tukapendeza na watu wakafurahi. Sasa wakivaa vizuri nadhani wanapendeza zaidi. Nawaomba sana sana, vinginevyo kwa kweli tutapoteza mambo mengi ambayo tumeachiwa na wazazi wetu ya makabila yetu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine sisi Dodoma, tunayo shule ya Buigiri ambayo iko chini ya Dhehebu la Anglikana na tunacho Kituo cha Kulelea Watoto cha Hombolo na vituo vingine ambavyo kwa kweli hapa Mjini vimeanzishwa. Sasa ningeomba basi nimeviona katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri, sasa vituo hivi kwa mfano, Buigiri, zamani ilikuwa inafanya kazi nzuri sana. Wale vipofu walikuwa wanatengeneza vitu, walikuwa wanasuka vikapu, walikuwa wanatengeneza *table mats* na walikuwa na vitu vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sina uhakika kwa sababu hicho kituo kiko chini ya dhehebu la Anglikana. Sasa Serikali inajihusishaje. Hebu naomba basi Serikali ivione hivi vyuo na vituo wavitembelee na wajaribu kwa kweli kutoa ushauri unaofaa. Kwa sababu kuna baadhi ya *NGOs* hizi tulizonazo kwa kweli nyangi zimeanzisha vituo vya kuwakusanya watoto. Kwa sababu kuna utaratibu wa kutafuta fedha kwa wafadhili basi *NGOs* zikipata fedha na watoto hao wanapata kidogo na wenye *NGOs* ndiyo wanapata kikubwa. Kwa hiyo, matokeo yake vituo hivi vya kuangalia watoto haviangaliwi sana. Ningeomba Wizara ijihushe vile vile kuvikagua vituo hivi na kuona kweli vinafanya kazi sawasawa au *NGOs* zinaomba fedha kwa ajili ya kujinufaisha wao wenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nzungumzie suala la mitafaruku ya familia ambayo ni kazi ngumu inayofanywa na Wizara hii. Kwenda kusikiliza kesi Mahakamani, kuwasuluhisha watu na wakati mwininge kupokea fedha za wale wanaokataa kulea watoto wao na nini. Mimi ningeshauri kwamba, ikiwezekana Serikali ianzishe Mahakama Maalum, kwa ajili ya kushughulikia kesi za mifarakano ya ndoa na wale wanaume wanaokataa watoto, mpaka wanakwenda kulazimishwa na Mahakama kupeleka fedha za kuwatunza watoto. Sasa ningeomba basi kuwe na Mahakama Maalum, ambayo itashughulikia mitafaruku hiyo na mingine kwa kweli ni midogo midogo ikishughulikiwa inaweza ikaisha haraka sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tunacho Chuo cha Ustawi wa Jamii, ambacho sasa hivi kiko Kijitonyama Dar es Salaam. Chuo kile sasa hivi kinatoa vijana wengi ambaio wanasaidia sana na wanapata taaluma ya kutosha kwa ajili ya kushughulikia wananchi na matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile Chuo sasa hivi kwa kweli mimi nasema pengine ni katika vyuo ambavyo nafikiri vinawenza vilkapandishwa hadhi yikawa hata Vyuo Vikuu ni kweli Serikali ingekuwa imefanya la maana sana. Kwa sababu vijana wanaotoka pale wanakuwa na taaluma ambayo kwa kweli ndiyo inayosaidia kutatua matatizo ya walemovu, kutatua matatizo ya wenye mifarakano ya ndoa, watoto watukutu na vitu chungu nzima. Ndiyo maana niseme hii Wizara ina mzigo mzito sana. Halafu kile chuo ndicho kinachofanya hiyo kazi nzito. Mimi ningeshauri Serikali ikiangalie sana kile Chuo ili kukiwezesha hata kuwa Chuo Kikuu kwani kuna ubaya gani. Ningependa nzungumzie hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na vile vile kwa kumalizia, nilikuwa naomba nzungumzie suala la mchezo wa mpira wa miguu. Mimi mama yenu napenda sana mchezo wa mpira wa miguu. Suala la mchezo wa mpira wa miguu ni kitu ambacho kwa kweli ni cha Kimataifa na mchezo huo wa mpira wa miguu unapendwa na dunia nzima. Sasa sisi Watanzania sijui tuna matatizo gani huko kwenye *FAT*. Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba, ni Shirika linalojitegemea au ni kitu ambacho kinajitegemea, lakini kuna haja ya kufanya kazi na kuna haja ya kuangalia, kwa sababu timu inaposhinda kama ilivyoshinda Timu ya Simba si ni sifa ya nchi nzima.

Hata Timu ya Yanga ikishinda vile vile ni sifa ya nchi nzima na hata Timu ya Taifa ikishinda ni sifa ya nchi nzima. Sasa inakuwaje mchezo wa mpira wa miguu unakwenda legelege kila kukicha. Sasa

Waheshimiwa Wabunge, wananihnikiza niseme mambo mengine ambayo sikupanga. Ningombwa kwa kweli Serikali ijizatiti kuhakikisha kwamba, mchezo wa mpira wa miguu unaboreshwaa zaidi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makof*)

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwanza, niungane na wachangiaji walio tangulia kuiunga mkono Hotuba hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na wataalam wake, kutokana na kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze katika mchango wangu kwa kuizungumzia hii Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Taasisi hii inaonekana kukua kadri siku zinavyokwenda. Nakumbuka kama miaka 10 iliyopita kiwango cha juu cha elimu iliyokuwa inatolewa pale ilikuwa ni *Diploma* ya Ustawi wa Jamii, mpaka sasa hivi wameshafikia kwamba, kuna *Diploma* nyininge mbili zaidi. Pia sasa hivi wako katika *Post Graduate Diploma* hiyo ni hatua ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na maendeleo hayo, bado pale Chuoni kuna matatizo ambayo kwa sehemu kubwa Serikali ingeliweka mkazo maalum ili hiki Chuo kikaonekana kukua kwake kunakwenda sambamba na hizo fani zake. Hali iliyoko pale Chuoni sasa hivi ongezeko la majengo haliendi sambamba na ongezeko la hizo fani zinazofundishwa pale au majengo yaliyokuwepo pale kuna nyumba ndogo ndogo ambazo kwa kweli hazilingani na Chuo ambacho kinatoa elimu kwa kiwango hicho na zile nyumba nyiningine zilizokuwepo pale zinafananafanana kama zile nyumba zilizokuwepo kwenye zile *quarter* za Mkonge. Sasa nadhani tubadilike ili tunaposema kwamba, hiki Chuo kinatoa Elimu ya Juu basi kiwe na hadhi hiyo ya Elimu ya Juu hata katika majengo yake. Hilo nafikiri ujumbe utakuwa umefika. (*Makof*)

Kwa hiyo hiki chuo kinastahili kusaidiwa katika hali zote, kwa sababu mchango wa Serikali pale naona ni mdogo sana. Hata katika hii Bajeti sikuona hata sehemu moja ambapo Serikali inalenga kukisaidia hicho chuo. Ninavyofahamu miaka mingi ya nyuma kile chuo kilikuwa kikisaidiwa saidiwa na wafadhili lakini Chuo ni chetu, waendelezaji ni wafadhili. Sasa hii nadhani haiendi sambamba na si vizuri kuendelea na hali hiyo. Kwa hiyo, Serikali ionyeshe ule umahiri wa kusaidia hiki chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo niende kwenye Idara ya Kazi. Kwanza nitoe pongezi kwamba nakumbuka kama sikosei mwaka huu tulipitisha sheria ile ya afya na usalama kazini. Kwa hivyo, kwa hilo natoa pongezi kwamba tumeanza kuzipunguza zile sheria kongwe na za zamani na uzamani wenywewe ni wa kupita kiasi. Lakini hata hivyo bado kuna kazi moja kubwa sana mbele ambayo inapaswa ifanyike ili mabadiliko hayo ya kuzibadilisha hizi sheria yaende sambamba na wakati tulionao.

Miongoni mwa sheria ambazo katika hali hii tunayokwenda nayo hasa katika mwelekeo huu wa ubinafsishaji basi ni hatari kubwa sana. Nadhani ingelikuwa Watanzania wengi sana wanazielewa sheria zinavyosomeka basi sijui wanglielewa elewa vipi haya mambo mengine namna yalivyo, mfano, Sheria ya Fidia. Kulingana na hali ya sasa hivi huu mfumo wa ubinafsishaji nadhani kwa mwekezaji ambaye anazingatia ku-*maximise profit*, basi kwake yeeye ni nafuu kubwa sana kwamba, mfanyakazi wake atapata ajali na atakufa kwake yeeye ni nafuu.

Ninaamini kimoyomoyo hata kama hataonyesha hadharani basi atafurahi kuliko mfanyakazi yule kama ataumia, aendele pengine kama labda amelazwa hospitali mwezi mmoja au wiki mbili, pengine ije itokee bahati mbaya kama ame-*invest* huko Mererani anaambishiwa huyu itabidi umpeleke Muhibili, kukodi ndege ya kumsafirisha, hizo gharama ni kubwa na kwa kawaida kwa mwekezaji hizo huwa hazipendi. Zile *figure* nimezisahau lakini hazifiki hata shilingi 200,000/=. Sasa linganisha gharama za matibabu kwa wakati tulionao na kulipa fidia kwa wafiwa kwa shilingi ambazo hazizidi hata shilingi 200,000/=.

Hali kadhalika hata yule ambaye anaumia katika kile kiwango kinachoitwa katika ulemavu wa kudumu nayo ni vile vile sikumbuki ziko ngapi lakini hazizidi shilingi 200,000/=. Sasa masuala kama haya kwa wakati huu tulionao ni vizuri watu wetu tuwarahisishie katika kiwango kama hicho. Hali kadhalika

iko Sheria ile ya *Employment Ordinance*, nayo sijui ya tokea mwaka gani mpaka hii leo hizo zipo na zinaendelea. Kwa maana hiyo hizo haziwasaidii wafanyakazi katika wakati huu. Zaidi ya hayo sikuona katika hotuba hii wala katika yale mahesabu nimeangalia suaona kama kuna mwelekeo ndani ya mwaka huu kutakuwa na mabadiliko yoyote kwenye sheria hizo. Kwa hiyo, ningeliomba hili suala tuliangalie kwa kina na kwa undani sana kuona kwamba, mabadiliko hayo yanafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumekuwa na hili wimbi la migomo na migogoro mingi tu katika maeneo ya kazi. Hali hii haiashirii mwelekeo mzuri kiuchumi katika nchi na hiyo inachangiwa na hizi sheria ambazo zimepitwa na wakati kupita kiasi. Kwa hiyo, ni vema kukawa na utaratibu maalum, unaoleweka kwamba sasa tunaelekewa wapi katika mabadiliko haya kwa maslahi ya Watanzania wenyewe na kwa maslahi vile vile ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mizozo tuliyonayo hivi sasa hawa watendaji ambao tunategemea watanzue matatizo haya kutokana na utafiti mdogo niliofanya. Unajua ukiangalia hata hizi Ofisi zenyewe za kazi katika Mikoa kwa kweli haziridhishi hata kidogo, hayo majengo yao ni duni sana. Kwa hiyo, ni vema Serikali ifanye mabadiliko ya hali hiyo ili iendane sambamba na hili jukumu zito ambalo wanabeba watendaji hawa katika ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tu Wizara hii kwa kuwa ninaamini kimoyomoyo hata kama hataonyesha hadharani basi atafurahi kuliko mfanyakazi yule kama ataumia, aendelee pengine kama labda amelazwa hospitali mwezi mmoja au wiki mbili, pengine ije itokee bahati mbaya kama ame-*invest* huko Mererani anaambiwa huyu itabidi umpeleke Muhimbili, kukodi ndege ya kumsafirisha, hizo gharama ni kubwa na kwa kawaida kwa mwekezaji hizo huwa hazipendi. Zile *figure* nimezisahau lakini hazifikii hata shilingi 200,000/=. Sasa linganisha gharama za matibabu kwa wakati tulionao na kulipa fidia kwa wafifa kwa shilingi ambazo hazizidi hata shilingi 200,000/=.

Hali kadhalika hata yule ambaye anaumia katika kile kiwango kinachoitwa katika ulemavu wa kudumu nayo ni vile vile sikumbuki ziko ngapi lakini hazizidi shilingi 200,000/=. Sasa masuala kama haya kwa wakati huu tulionao ni vizuri watu wetu tuwarahishie katika kiwango kama hicho. Hali kadhalika iko Sheria ile ya *Employment Ordinance*, nayo sijui ya tokea mwaka gani mpaka hii leo hizo zipo na zinaendelea. Kwa maana hiyo hizo haziwasaidii wafanyakazi katika wakati huu. Zaidi ya hayo sikuona katika hotuba hii wala katika yale mahesabu nimeangalia suaona kama kuna mwelekeo ndani ya mwaka huu kutakuwa na mabadiliko yoyote kwenye sheria hizo. Kwa hiyo, ningeliomba hili suala tuliangalie kwa kina na kwa undani sana kuona kwamba, mabadiliko hayo yanafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumekuwa na hili wimbi la migomo na migogoro mingi tu katika maeneo ya kazi. Hali hii haiashirii mwelekeo mzuri kiuchumi katika nchi na hiyo inachangiwa na hizi sheria ambazo zimepitwa na wakati kupita kiasi. Kwa hiyo, ni vema kukawa na utaratibu maalum, unaoleweka kwamba sasa tunaelekewa wapi katika mabadiliko haya kwa maslahi ya Watanzania wenyewe na kwa maslahi vile vile ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mizozo tuliyonayo hivi sasa hawa watendaji ambao tunategemea watanzue matatizo haya kutokana na utafiti mdogo niliofanya. Unajua ukiangalia hata hizi Ofisi zenyewe za kazi katika Mikoa kwa kweli haziridhishi hata kidogo, hayo majengo yao ni duni sana. Kwa hiyo, ni vema Serikali ifanye mabadiliko ya hali hiyo ili iendane sambamba na hili jukumu zito ambalo wanabeba watendaji hawa katika ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tu Wizara hii kwa kuwa imefikia hatua nzuri sana kwenye hii sera ya watu wenye ulemavu. Mwelekeo ni mzuri, ni vyema sasa ingeliharakisha kadri iwezekanavyo ili hii sera ikamilike na kutoka mapema iwezekanavyo. Pamoja na kuwa na Sera pia ni vyema tungeliangalia uwezekano wa kuingiza japo kwa kifupi sana ndani ya Katiba yetu kuonyesha haki za walemvu na kuwatambua kuwepo kwao na haki zao. Zipo nchi ambazo zimefanya hivyo nasi pia si vibaya tukafanya hivyo. Tukaonyesha japo kwa kifupi haki za walemvu, haki za watoto na mengine mengine kama hayo. Kufanya hivyo nadhani tutakuwa tumejenga mtiririko mzuri juu ya haki za hawa wenzetu. Kwa sababu huu ulemavu kuna aina nyingi sana. Kuna wengine ni walemvu lakini wenyewe hawajui kama wana ulemavu. Siku moja nilikuwa nasikiliza redio hivi karibuni, wakawa wanazungumzia

ulemau kama pengine alionao Mheshimiwa Professa Kapuya, kuwa na kipara hivi ambapo *group* hilo anaingia Mheshimiwa Magoba yumo, mimi simo ni panki tu yangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo pia nayo imezungumzwa kuwa ni ulemau. Sasa kuna hizi aina za ulemau ambazo nydingine hazionekani lakini nazo ni vizuri kwamba tutakapokuwa pamoja na sera ni kutambua katika Katiba itasaidia kwa kiwango kikubwa sana tutakapozungumzia juu ya haki nydingine ambazo zinawastahiki walemau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hifadhi ya jamii, nizungumzie hii *NSSF*. Ikiwa kama tunategemea iwe ni kioo kwa mwelekeo wa hifadhi ya jamii katika nchi yetu. Nasema kama ni kioo kwa sababu kwanza ipo chini ya Wizara ya Kazi. Wizara ya Kazi ndiyo yeny e jukumu la kuratibu mtiririko mzima wa masuala haya ya hifadhi za jamii. Nimeangalia hiki kitabu cha *Annual Report 2001/2002*, kinaonyesha mwelekeo au hatua ambayo imefikiwa na hifadhi ya jamii au *NSSF*. Wamepiga hatua nzuri na wanastahili pongezi. Nadhani Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hili anastahiki pongezi ya hali ya juu sana na ni vyema hizi juhud akazidi kuongeza. Kwanza katika hatua mbalimbali ambazo amefikia katika kuweka vitegauchumi sehemu mbalimbali katika nchi, kuonekana kwamba hii inakuwa badala ya kupunguka. Takwimu zinaonyesha kwamba, hata idadi ya wanachama inaonekana kuongezeka, idadi ya wanaoingia ni wengi ukilinganisha na wale wanaotoka kwa mwaka. Takwimu zinaonyesha kulikuwa kuna watu 55,655 waliongezeka wakati waliopungua ni 29,929.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wanachama kutoka 325,000 mpaka 351,000 hiyo inaonekana ni hali ya kukua. Kwa hiyo, mwelekeo ni mzuri lakini ni vyema mpaka hivi sasa kwa kuwa hatujawa na sera ya hifadhi ya jamii, lakini bado kuna zile nyininge ambazo ziko katika *provident fund* wakati ule mfumo wanaona ni mfumo ambaa umepitwa na wakati. Kwa hiyo, ni vizuri tutakapokuwa na sera zile itakuwa ni rahisi kuzibadilisha zielekee huko huko kwenye huu mfumo kamili wa hifadhi ya jamii. Hali kadhalika pia tutaweza kufika mahali pengine pa kuoanisha zile *statutory benefits* wanazostahili hao *members* wa hizo *scheme*. Lakini pia ningelimwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mkurugenzi wa hili Shirika, waangalie uwezekano wa kuwa na Ofisi au Wakala Zanzibar kwa sababu ninavyofahamu pia anao wanachama wake kule, kwa hiyo, ni vyema nako akawa na Ofisi ili kuwarahisishia wanachama wake waliokuwepo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niondoke hapo kutokana na muda sasa niende kwenye michezo. Wenzangu wameshazungumza kuonyesha, kukerwa kwao na hali ya michezo katika nchi yetu pamoja na ubovu wa uongozi uliokuwepo kwenye *FAT*. Katika Mkutano wa 10 tarehe 14 Februari, 2003, Mheshimiwa Richard Ndassa, aliuliza swali namba 110, ambapo ndani ya swali hilo alizungumzia kwamba, katika mwaka 1998 - 2002, *FIFA* ilitoa msaada kwa Tanzania zikiwemo Dola 1,000,000, Dola 250,000 na Dola 500,000. Hizi Dola 250,000 ni fedha ambazo zinatolewa kwa kila mwaka na Dola 500,000 zinatolewa kwa ajili ya shughuli za utawala na ukarabati wa Ofisi. Mheshimiwa Waziri, alipojibu swali hili alisema kwamba, fedha hizo zilitumika, akahuisha mpaka masuala ya utawala katika Ofisi, kulipia wafanyakazi katika hifadhi za jamii, kitu ambacho kwa mawazo yangu naona haya mambo ni mgongano mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu kila mchezo unochezwa ndani ya nchi, *FAT* kuna fedha wanazopokea. Sasa bado imefika mahali kwamba, inashindwa kuisafirisha timu kuipeleka nje kwa Michezo ya Kimataifa. Hali kadhalika, hata pale ilipokuwa kupeleka majina ya timu zetu, hiyo imeshindwa uongozi huu wa *FAT*. Kwa hiyo, nilichokuwa nataka kukizungumzia hapa ni kwamba, kwa uongozi huu tusitegemee mabadiliko. Badala ya ule mfano wa kuzungumzwa kichwa cha mwenda wazimu, nadhani kama lingekuwa kuna jina lingine duni zaidi ya hilo, tungelitegemea liwe zaidi ya hapo kuwa mwendawazimu. Kwa sababu pengine unawenza ukabahatika wazimu ukapona. Lakini kwa uongozi huu hakuna mwelekeo wa kupona. Juzi juzi tu kulikuwa kuna mkutano wa kusuluhisha. Leo asubuhi nasikia kwamba, Ndolanga anasema hakuna suluhu *FIFA*, ataamua sasa unategemea nini hapo. Kweli kuna uongozi hapo?

Zaidi ya hayo kuna taarifa hivi karibuni kwamba, *FAT* wamenunua vitanda. Sasa chama cha mchezo huu wa mpira wa miguu na kununua vitanda sijui kuna mchezo gani mwengine watakaouanzisha ambaa utatumia vitanda. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona na kunifanya mzungumzaji na mchangiaji wa mwisho katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, Bajeti ya Wizara ya Kazi, Vijana na Michezo.

Nimpungeze Mheshimiwa Waziri na watalamu wake, kwa hotuba nzuri na pia nimpungeze Waziri Kivuli, Mheshimiwa Khalifa, kwa hotuba nzuri ambayo mimi naamini kama Mheshimiwa Waziri, ataichukua jinsi ilivyo na akaifanyia kazi, naamini mwakani tunaweza tukaja tukiwa na sura tofauti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nikipita mitaani nikakuta vijiwe alivyovizungumza Mheshimiwa Waziri, nikakuta Maaskari Mgambo wanakimbizana na vijana Wamachinga, ukipita Ohio saa 6.00 usiku ukakuta jamaa wanakatiza mbuga na magari yanapiga *break* na pia ukiingia Uwanja wa Taifa mle ukakuta Timu ya Taifa inafungwa, mimi huwa namwonea sana huruma kabisa Mheshimiwa Profesa Kapuya. Kwa sababu ni kioo cha utendaji kwa Wizara yake. Sasa hali kama hiyo kwa Taifa ambalo linatafuta maendeleo yake si suala la kuliacha hivyo hivyo, ni suala ambalo linabidi kwa namna moja ama nyininge lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla sijachangia huko, zaidi mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, kwa msaada mkubwa walioutoa kwa Klabu ya Simba, wakati wa Mashindano ya Kimataifa ambayo mpaka hivi sasa Simba bado wako katika mashindano hayo na wataendelea kufanya vizuri na Mwenyezi Mungu akitujalia kombe lazima linakuja Tanzania. (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Poleni! (*Makofî/Kicheko*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali inathamini kazi ambayo Klabu ya Simba inafanya na kwa kiasi kikubwa, Serikali inaienzi Timu ya Simba, ndiyo maana ndani ya Bunge hili Simba tupu, *carpets* na kila kitu. Kwa hiyo, mambo yako katika msitari ule ule. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nielezee siri moja kubwa ambayo imechangia vile vile Simba kufanya vizuri, ni pamoja na viongozi wetu kujali timu zinapokuwa kwenye mashindano. Kitendo cha Mheshimiwa Waziri, kwenda mpaka Cairo akahudhuria ile mechî yeye mwenyewe bila ya kutuma wasaidizi wadogo wadogo ni kuongeza mori kwa wachezaji kujituma kuhakikisha hawamwaibishi Waziri wao akiwa pale uwanjani. Pia kitendo cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutembelea kambi na kuwapa moyo wachezaji ni kitendo ambacho kinawapa moyo wachezaji kujua Taifa zima liko nyuma yao. Kwa hiyo, mimi naamini kama Serikali kweli ikidhamiria kuweka nguvu japo hata *moral*, hata sio lazima fedha naamini wachezaji wetu watakuwa na moyo wa kufanya vizuri. Ndiyo maana nilikuwa naangalia kwenye *TV* mchezo wa wenzetu wa Rwanda wakati wanacheza na Ghana. Mheshimiwa Rais Kagame, alikuwa kati ya washabiki waliokuwa wanaruka ruka mpaka anaacha kiti anakwenda uwanjani kumshangilia mfungaji goli. Sasa hata mchezaji nafikiri akiona Rais wake yuko jukwaani yuko tayari kuacha mguu uwanjani kuhakikisha anatetea Taifa lake na Rais wake ambaye yuko pale uwanjani. Kwa hiyo, mimi naamini hata mechî zinazokuja Mheshimiwa Rais, tutamwona Uwanja wa Taifa akishangilia Timu ya Simba na kuhakikisha anaipa nguvu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kidogo suala la ajira. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia kwamba, kituo ambacho kinaunganisha watu wanaotafuta ajira na wale wanaotafuta kuajiri, kuanzia mwaka 2001 kati ya waombaji 7,067 waliofanikiwa kuunganishwa ni waombaji 182 ambao ni asilimia 7. Sasa mimi huwa nikipita pale kwenye lile jengo, wale Waheshimiwa wamepewa jengo kubwa lina maandishi makubwa na nafikiri ukiingia mle kuna *staff* wengi ambaeo sehemu ya malipo yao yanatokana na Bajeti tunayoipitisha. Sasa hii asilimia 7 kwa kweli ni *success* ndogo, lazima tukubali na kwa mwendo huu hiki kituo sidhani kama kinatoa msaada mkubwa wa kupatikana ajira au kwa malengo ambayo tulikuwa tumekusudia kifanye, kitabaki pale kama picha, kitabaki pale kupokea watu kwenye msululu tu na watu hao wasipate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nasema, suala la ajira tusiliangalie kwa upeo ambao ni finyu. Suala la ajira hivi sasa tutake tusitake, kama mwenzetu alivyozungumza katika Hotuba yake, Mheshimiwa Khalifa, Waziri wangu Kivuli, ni suala ambalo ni bomu ambalo tumelikalia na hatujui litalipuka siku gani. Wale watu ambao wameona hawana kazi si kwamba, hawataki kufanya kazi, ni kwa sababu utaratibu wa kinchi bado haujawekwa katika msitari kiasi cha ku-*accommodate* kufanya kazi. Lazima tukubali, *we are responsible* na ndio utawala wenyewe. Kuwaacha *idle* mtu yeote anaweza akawatumia vibaya.

Leo hii Bwana Mahita, anakimbizana na majambazi hawa wanaotokana na baadhi ya vijana ambao wanakosa ajira na hawa vijana wanaajiriwa na watu ambao wanakuwa na uwezo tu kwamba, wana mtaji wa silaha anamkuta kijiweni anamuajiri, wanakwenda kwenye misheni ili apate lishe ya kuishi siku hiyo jioni. Kwa hiyo, mimi nashukuru kwamba, katika Kamati tulizokaa katika majibu ya Serikali ambayo imekuwa inatoa ni kwamba, Serikali imeliona hilo na inataka kulifanyia kazi na si suala la Wizara moja, linapaswa liwe suala la Wizara zote za Serikali. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, hapa haiwezi kumaliza tatizo la ajira au hiki kituo hakiwezi kumaliza tatizo la ajira kama Serikali yenyewe, *department* zote hazikukaa kuangalia namna gani tunaweza tuka-*create* vyanzo vya ajira. Haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kutoa maoni kidogo ya namna ya ku-*create* ajira na *actually* ndio kazi ya Serikali. Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kutumia kanuni na taratibu ambazo amepewa uwezo huo wa kisheria, anaweza akaweka utaratibu leo hii tunapenda sana ku-*categorise* hoteli zile kubwa kubwa sijui *Five Stars*, *Two Stars* sijui na nini, lakini unaweza ukaka-*categorise* kutaka hoteli ya ngazi ya chini na mtu ukamwekea masharti ya ajira. Leo hii unakwenda kwenye *Hotel Fifty Six*, ni hoteli inayopokea Waheshimiwa Wabunge na wageni maalum. Yule bwana pamoja na huduma anayoitoa yeze pale ni kukata leseni na kumwajiri mtu yeote ambaye anajua mtoto wangu amemaliza darasa la saba mlethe bwana nitampa kazi. Lakini huwezi kukuta mtu ambaye amemaliza Forodhani na yeti vyake anahangaika yuko kwenye kituo kule Dar es Salaam anatafuta kazi. Lakini huyu mtu anapokwenda kukata leseni angekuwa ameelezwa kwamba, unapotaka kupewa leseni unapaswa uwe na wataalam wenye yeti vya aina fulani fulani. Kwa hiyo, angelazimika kuweza kuwa-*accommodate* watu waliomiliza kwenye vyuo mbalimbali badala ya kuokoteza tu na kuna watu wamesoma na wengine wanakatishwa tamaa wasiende kusoma kwa sababu hakuna ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *engineers* wengi wanakuwa hawana kazi lakini unakuta mtu ana Kampuni kubwa tu kwa sababu hakuna utaratibu unaomlazimisha kumwajiri *engineer*, yuko tayari anaweza akaajiri *engineers* wawili tena wenyewe hawafanyi kazi hata kwenye Kampuni yake wako kwenye Mashirika mengine anapewa kazi. Sasa mimi nilikuwa napendekeza kwa kweli kama tunataka kusaidia kituo hiki, ni lazima nguvu ambayo wamepewa ya kukianzisha kituo hiki ilindwe vile vile kitaratibu na kikanuni za sheria ili kuweza kuhakikisha nafasi za ajira zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kuweza kuongeza ajira ni Serikali pia kuheshimu kazi za watu na kuwa mstari wa mbele kuziheshimu na kuzifanyia kazi na kuziendeleza. Ukimkuta mtu ameanza mradi wa kuosha magari, wewe kama Serikali ukaona kitu cha kwanza cha kwenda kumpiga kirungu kwamba anaosha magari, anachafua mazingira humsaidii na wala humwendelezi kwenye kazi ile anayo fanya. Mimi nafikiri mtu kama huyu anahitaji kuelekezwa kwamba, bwana wewe *okay*, unaosha magari lakini unaweza ukaanzisha mradi wako wa kuosha magari sehemu fulani na tutaweza kukusaidia. Hivi ukiingia kumpiga virungu na kumfukuza pale haimsaidii. Ukimkuta mtu pale Bukoba Mjini ameanza biashara ya kuendesha balskeli, dawa, sio kumpiga virungu na kukamata balskeli yake kupeleka Polisi. Nafikiri kama huyu mtu atasaidiwa kuelezwia kwamba, hapa mjini kinachohitajika ni balskeli zenye gurudumu tatu na kiti cha sponji, mtu akakaa raha mustarehe kama ambavyo biashara ya balskeli inaendeshwa huko Bangkok. Yule mtu atanunua balskeli ya aina hiyo na atapata ajira badala ya kumfukuza asifanye kazi hiyo. Tunapaswa kuwa *creative* katika namna hiyo, Serikali inapaswa kuwa *sharp*. (*Makofî*)

Pia mimi nitumie fursa hii, dakika chache zilizobaki, niwapongeze dada zangu kutoka Bukoba, Saida, Levina Kasabila na Maua. *Since* dada zangu waliopoona kahawa imeshuka bei, wakaona afadhalii waimbe. Walivyooma Serikali hainunui kahawa, bei imeshuka kutoka shilingi 500 mpaka shilingi 90 wakaona bora waimbe tu. Kazi ambayo imewafanya sasa hivi ni kati ya watu wanaozungumzwa Dar es

Salaam, ambao wanaweza wakakununulia *crates* tatu za bia ukanya ukaacha. Wameajiri vijana wetu walikuwa huko vijijini tu wanalima magugu sasa hivi wako Dar es Salaam wanapiga piga manyanga, wenye kupiga ngoma wako Dar es Salaam, ni ajira. (*Makofsi*)

Kwa hiyo, mtu anapoanzisha shughuli akawa *creative*, aka-*initiate* vitu vyatufanywa ambavyo ni bora, Serikali ikamwendeleza na kwa kumwendeleza huyo itakuwa inawaendeleza wengine na kuwapa ajira wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimalizie kuhusu migogoro ya kikazi. Mimi nasema kwamba, Mheshimiwa Waziri, inabidi alivalie njuga. Baya zaidi ambalo nalichukia ni kuona Mashirika ambayo yanakabiliwa na migogoro ya wafanyakazi na hayawalipi wafanyakazi haki zao ndiyo yanayoongoza kuhudhuria *functions* za ku-*raise funds* kwa ajili ya dhifa mbalimbali.

Mimi kitu kinachoniudhi, unakuta mtu wa *NBC*, wafanyakazi hajawalipa, hajawapa marupurupu yao, anakaribishwa kwenye dhifa labda yuko mkubwa unakuta anamwaga sijui shilingi 50 milioni au shilingi 100 milioni wakati nyumbani kwake kumeoza na kunanuka na wafanyakazi wamegoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi suala hili sikubaliani nalo na nalilaani kwa nguvu zangu zote na naomba Mashirika hayo au Makampuni hayo yaweze kujirekebisha. Naiomba Serikali kwa sababu mojawapo ni Shirika ambalo wafanyakazi wake wanadai ni mali ya Serikali. Juzi nimeona wanalia mpaka mama anatoa machozi, watu wa *Tanzania Elimu Supplies* Serikali jamani tuonyeshe mfano mzuri wa kuwalipa watu vitu vyao. Tuwalipe haki zao tusizilalie.

Nashukuru Mheshimiwa Waziri, amezungumza kweli kwa unyonge na kwa hali ya kutia matumaini, awalipe wafanyakazi hawa jamani. Walipeni wengine tumesoma kwa msaada wa *TES*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja yako. Simba ooye!!!

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. BALOZI DR. PIUS Y. NG'WANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi hususan ufundi stadi ndiyo mkombozi wetu katika kujenga uwezo wa wananchi wetu hasa vijana kujiajiri wenywewe.

Ili tufanikishe malengo yetu ya kuwapa nafasi ya kujiajiri vijana wetu, inafaa kuainisha kwa ukaribu zaidi programu zetu katika sekta mbalimbali (*Intersectoral Coordination*). Kwa kuanzia mfumo wa elimu yetu nchini uwe wazi (*open*) na uweze kuingilika na kutoka (*Multiple Entry System*) kwa urahisi kwa nyakati na medani mbalimbali.

Ninapendekeza watoto waanze elimu ya ufundi katika elimu ya awali (miaka miwili ikiwezekana umri wa miaka 4 - 6). Katika elimu ya msingi *hand crafts, local crafts, typing* na *computer skills* zianzishwe. Mazoezi madogo madogo katika kutumia nyuzi kwa mfano, kufuma, kudarizi, yanawenza kuanzishwa. Baada ya kuboresha hali ya shule za msingi inawezezekana kuondoa *double session/half day schooling* katika madarasa ya kwanza na la pili na hivyo kuwa na mfumo wa miaka sita tu badala ya saba kwa elimu ya msingi.

Baada ya elimu ya msingi watoto wenye mvuto wa ufundi waendelee kwenye vituo vya ufundi vya Kata. Hapa wajifunze stadi mbalimbali zinazohitajika vijijini na mijini kwa mfano, *brick laying, hydrofoil block making, stone masonry, book keeping, commerce, cooperative-work*, ufundi wa baiskeli, matrekta na kadhalika. Wakae hapo miaka mitatu. Kila Wilaya kwa kuanzia kuwa na *Vocational Institute* au *Polytechnic*. Wanafunzi wachaguliwe kutoka vituo vya ufundi na wale waliomaliza *Form IV*. Mafunzo yaye ya miaka mitatu. Walimu wapewe *Trade Test Certificate* na wale waliofuzu vizuri kwa vitendo na nadharia wapewe *Ordinary Technicians Diploma* inayolingana na *FTC* au *City Guilds OTD of London*. Kila Mkoo uwe na *Technical College* ambayo itatoa *OTD* na *Higher National Diploma*. Uhusiano wa *VETA, NACTE, MOSTHE, MOEC* na Wizara ya Kazi uimarishwe.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Vyuo vya VETA hivi katika kuwatayarisha vijana kwa ajira binafsi au kuajiriwa, ni Sera ya Serikali kujenga Vituo vya VETA vingi zaidi ili kueneza kwa haraka taaluma mbalimbali kwa vijana. Kwa kuwa mpaka sasa kuna mikao ambayo bado haina Vyuo vya VETA, Lindi ikiwa ni mkoaa mmojawapo, ni lini Wizara itaanza mikakati ya kujenga chuo katika Mkoa wa Lindi? Awali chuo hiki kilipangwa kujengwa kati ya miaka ya 1996 - 99, lakini kwa sababu ambazo hazikutolewa maelezo, Wizara iliamua kutokujenga chuo hicho Lindi na badala yake kikajengwa Mkoani Mtwara. Ninatoa rai kwa Wizara kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga Chuo cha VETA Mkoani Lindi.

Sera ya nchi ni kutoa kipaumbele ajira kwa raia wa Tanzania hususan katika maeneo ambayo taaluma hiyo ipo. Hivi karibuni, katika zama za utandawazi na ubinafsishaji wa shughuli mbalimbali hapa nchini, kuna ukiukwaji ulio wazi wakati makampuni ya kigeni yanawaondoa Watanzania ambao wana *qualification* na uzoefu na badala yake kuwaweka wafanyakazi ambao siyo raia. Aidha, inaelekea mtindo huu unaendelea bila kuzingatia Sheria za nchi zinazowataka wafanyakazi hao wasio raia kupata kibali kwanzana na kukaa hapa kutoka uhamiaji na baadaye kibali cha kufanya kazi kwa muda uliokubaliwa. Haya yanaendelea *with impunity*. Ni utaratibu gani umewekwa na kufuatwa na Wizara katika kudhibiti tatizo hili ambalo linazidi kuongezeka siku hadi siku. Tanzania ni nchi pekee ambayo inaruhusu wageni wasio raia kuja kuanzisha hata biashara za migahawa ya mitaani, kazi ambazo wananchi wanazimudu kabisa.

Ninaitaka Wizara kuongeza *inspection* ya sehemu za kazi, mara kwa mara, ili kuondoa kero hii ya ajira isiyozingatia sheria za nchi na hivyo kuwanyima raia haki ya ajira hapa kwao.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote, kwa kuandaa hotuba nzuri yenyenye maelezo ya kina lakini pia kwa utekelezaji wa shughuli za mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunalo tatizo kubwa la watoto yatima hasa baada ya vifo vingi kutokana na Ugonjwa wa UKIMWI. Tunashukuru sana kwamba, yapo Mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamejitoa katika maeneo mbalimbali kuanzisha vituo/malazi kwa ajili ya kulea watoto hawa yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa ya kuhamasisha jamii ili wawe na moyo wa kuwasaidia watoto wanaoachwa yatima. Imezuka tabia ya kipeleka watoto kwenye makao ya yatima hata kama kuna baba mdogo, mama mdogo, shangazi, bibi, kaka au dada, ambao wanaweza kuwalea watoto hao na kuendelea kupata malezi na mapenzi ya kifamilia na kupata maadili mazuri. Ipo haja kubwa kuwa na sera kwa ajili ya malezi ya watoto yatima ili kuhamasisha jambo hili. Watu wenye ulemavu ni kundi maalumu katika jamii ya Watanzania, ambalo linahitaji kupata huduma wanayohitaji kulingana na hali zao.

Kutokuwapo kwa Sera ya Walemaru kunasababisha watu hawa kutopata huduma wanazostahili. Sasa je, ni lini Sera itakamilishwa? Ruzuku kwa ajili ya makao ya wasiojiweza na makao ya watoto yatima ni muhimu sana. Ni jukumu la Serikali kuyahudumia makundi hayo. Sasa ni muda mrefu sana Serikali imesitisha misaada kwa makao hayo. Je, Serikali imejivua jukumu lake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Profesa Kapuya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir na timu ya Watendaji wa Wizara nzima, kwa kazi nzuri na hotuba yenyenye dira na mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kwa njia ya kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Kapuya na uongozi mzima wa Michezo ngazi zote za Taifa, Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Arumeru, kwa ushirikiano na msaada wa hali na mali kwenye ajali ya trekti iliyotokea Sakila, Arumeru Mashariki, Juni, 2002. Wananchi wamenituma nifikishe hizi salamu kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara.

Shirika la Tija la Taifa (*NIP*), limezungumziwa ukurasa wa 40 wa Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Maoni yangu kuhusu *NIP* ni kwamba, dhana, mfumo, utendaji na mahitaji yake, yanahitaji kutazamwa upya. *It needs comprehensive review.* Vinginevyo tutakuja ku-regret muda na resources tulizowekeza au tunazoendelea kuwekeza kwenye *NIP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hisia kwamba, kuna masuala ya jamii ambayo yanaonekana kuwa na mwingiliano kati ya Wizara ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Wizara au Serikali inasemaje kuhusu hisia hizi? Je, ni lini suala hili litafanyiwa utafiti (*study*), kubainisha ukweli na kuweka mipaka ya majukumu inayolewaka na ambayo haileti utata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kipengele cha makazi ya maskini yanayosimamiwa na Serikali Kibirizi.

Makazi haya yanahitaji ukarabati na wakazi wake wanahitaji matunzo. Wameonekana kuwa kero kwani kila siku hasa siku ya Ijumaa huzagaa mjini kuomba. Zifanyiwe juhudzi za kukitembelea kituo na kujionea hali halisi ya kituo hiki. Kimegeuka kuwa kituo cha ombo ombo na kama fedha zinatolewa basi haziwafikii walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwenye makazi ya wazee wasiojiweza - Kituo cha Magugu - Wilayani Babati. Kituo hiki ambacho ni makazi ya wazee wasiojiweza kina matatizo mengi na sasa yamekuwa ya muda mrefu. Matatizo hayo ni:-

1. Huduma katika makazi haya hayaridhishi;
2. Utaratibu wa utoaji huduma hauzingatiwi ipasavyo;
3. Eneo la makazi ya kituo hiki linapaswa kujulikana vizuri zaidi kisheria hasa matumizi ya ardhi;
4. Majengo yanahitaji ukarabati mkubwa; na
5. Watumishi wanaohudumia kituo hiki wanapaswa kuangaliwa kwa karibu zaidi jinsi wanavyotekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa kuwa huduma za kituo hiki zimekuwa zikipitia Idara ya Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, sasa ni vema kuwe na Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Manyara, ambaye atawenza kuhudumia kituo hiki akiwa karibu zaidi na Babati. Pili, ni muhimu pia maelekezo yote yanayokwenda kwenye kituo hiki pia yafahamike na Viongozi wa Wilaya ya Babati kwani ni mara chache sana taarifa za Kituo hiki zinifikishwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Babati, kwa DC na kwa Mbunge. Huu ni upungufu katika kuboresha huduma za kituo hiki.

Pia nashauri Mheshimiwa Waziri, atembelee kituo hiki ili ajionee mwenyewe matatizo. Hivyo, nitapenda kupata kauli ya Mheshimiwa Waziri katika kuboresha kituo hiki cha Wazee wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchuua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kazi nzuri ambayo hatimaye imezaa hotuba nzuri. Ni hotuba ambayo italeta msisimko mkubwa katika jamii yetu hii ya Tanzania. Pia naomba kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja iliyio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu ziara ya Mheshimiwa Waziri, alipokuja Jimboni Kikwajuni, mnamo tarehe 11 Januari, 2003 wakati wa Sherehe ya Mapinduzi Matukufu. Alibahatika kuchaguliwa kuja kuweka Jiwe la Msingi katika Uwanja wa *Basketbal*, unaojengwa hivi sasa, uliopo kwenye Uwanja wa Michezo wa Mnazi-Mmoja kwenye Jimbo la Kikwajuni. Kwa kweli shughuli hiyo ilifana sana na Mheshimiwa Waziri, aliongelea mambo mengi yenye faida kubwa kwa vijana wetu, kwa jinsi wanavyowenza kujiepusha na mambo ya uasherati. Katika kuhamasisha kwake, Mheshimiwa Waziri pia aliahidi kutoa mchango wa Sh.500,000/= kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa uwanja huo wa *basketball*. Lakini ninaona ni muda mrefu hivi sasa umeshapita, fedha hizo zimeshindikana kupatikana na hivi sasa baadhi ya wananchi wanashindwa kuelewa ni kwa nini fedha hizo zimeshindikana kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakati ana-*wind-up* na ninasisitiza kwa heshima zote anieleze kinagaubaga ni lini fedha hizo zitapatikana na ni vizuri aniahidi lini niende nikazichukue.

Kwa hayo machache ninaomba kuishia hapo.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii muhimu ili nitoe mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Misungwi. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Waku wote wa Idara, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya hotuba hii, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inayo kazi ngumu sana katika suala la kulea wazee. Taarifa ya Wizara imeonyesha idadi ya watu kwenye makazi 17 ni 1,785, hii inaonyesha ukubwa wa kazi hii. Wazee ni sawa na watoto kwani huwa hawana uwezo wa kufanya kazi kutokana na umri pia magonjwa na ulemavu kwa baadhi yao. Watu hawa wanatakiwa kutunzwa na Serikali, kazi ambayo Serikai ya CCM inaifanya hadi leo katika maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makazi hayo 17, idadi kubwa ya watu iko Bukumbi Wilayani Misungwi Mkoa wa Mwanza. Naomba nipate majibu kwa maswali yafuatayo:-

Kwanza, Serikali imetenga kiasi gani kwa Kambi ya Wazee Bukumbi yenyne idadi ya watu 515, hii ikumbukwe kuwa mwaka huu chakula ni cha shida hasa katika Mkoa wa Mwanza?

Pili, katika Kambi hii vijana wanaoishi na wazazi wao waliopo hapo, wapo wanaosoma na pia wapo waliomaliza shule, Serikali ina mpango gani wa kuboresha shughuli zao za ufundi ili waweze kuijendeleza na baadaye kujajiri, kiasi gani kimetengwa kwa suala hilo?

Tatu, Kambi hii inapaswa kuwa na watumishi wa kutosha wakiwemo waganga kwa ajili ya kuwapatia matibabu, je, watumishi wangapi wapo na je, ikama ya kambi inatosheleza?

Nne, pamekuwepo na tatizo la maji siku za nyuma tatizo hilo sasa likoje?

Mwisho, naomba sana Waziri au Naibu Waziri, apate kutembelea Kambi hii ambayo majengo yake yanahitaji ukarabati. Pia ipo Kambi nyingine ndogo eneo la Igongwa sehemu ya Mwantambi ina idadi ndogo ya watu kati ya 30 hivi nayo ni vyema ikapangiwa mgao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametoa taarifa nzuri hivyo inanifanya niunge mkono kwa 100% ili pesa aliyoomba apitishiwe na afanye kazi alizokusudia. Niombe tu katika majumuisho anijibu maswali yangu. Ahsante.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara zote na watumishi, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba hii ya Bajeti. Nampongeza pia Waziri, kwa kuwasilisha hotuba yake kwa muda muafaka licha ya kasi kubwa ya kuisoma hotuba hiyo. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Yapo mengi yamefanywa na Wizara katika kipindi hiki cha mwaka mmoja. Naipongeza Wizara kwa kuliwekea uzito suala la kutekeleza uanzishaji wa Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (*OSHA*). Nimeona jinsi kaguzi zilivyoongezeka sana na kwa mara ya kwanza hata fedha zilizokusanywa kufikia Sh.127,000,000/= ni dalili nzuri ya awali. Hongera kwa hilo.

Suala la usajili wa Vyama vyta Wafanyakazi, linaonekana kuzidi kuendelea. Maana zaidi ya vyama 16 vipo sasa ukilinganisha na 10 vilivyoanza. Ni vizuri suala hili likatazamwa ili kuwashauri wafanyakazi wasiendelee kuwa na utitiri wa vyama. Huu unaweza kuwa ni mwanzo wa kudhoofika kwa umoja wa vyama. Linalotakiwa siyo uwingu wa vyama, bali ubora na umadhubuti wa vyama katika kutetea maslahi ya wafanyakazi popote pale walipo katika umoja wao. Kazi ya kuelimisha wafanyakazi iendelee kuwa ni ya Serikali pia. Sheria za nchi lazima zieleweke vizuri ili kupunguza vurugu zinazoweza kujitokeza, umuhimu wa kuendeleza Idara ya Elimu ya Wafanyakazi na kuipa watendaji wa kutosha wakati huu wa uchumi huru, ni *priority* kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaomaliza mafunzo ya *VETA* katika fani mbalimbali, ni budi wakaendelea kusaidiwa vifaa vyta kuanzia kazi. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kupata msaada wa vifaa kutoka China. Kwa kuwa bei yao ni nzuri na ni *affordable*, pia ni rahisi kuvitumia mahali popote. Lakini, vingine vinawenza kutengenezwa na baadhi ya vyuo vyta *VETA* hapa hapa. Naona hata vinavyotoka China, vinatengenezwa na vyuo vyao vidogo vidogo huko kwao, kwa nini tusifanye hivyo kwa sababu ya kuongeza ufundi, lakini pia kuongeza kipato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya *VETA* ni nzuri sana, lakini upo umuhimu wa kuangalia kwa undani matatizo ya watumishi wenyewe, ambao kwa sehemu nydingi huwa hawaelewani. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri ukawa unapata nafasi ya kukutana na watumishi wote wa *VETA*, ili kuelewa nini kinatokea ndani ya *VETA* na nini kinatokea nje ya *VETA*. Lipi linasababisha mikingamo ndani ya *VETA*?

Mikopo ya vijana sasa ingefaa ielekezwe kwenye Benki Kata ambapo ikitumwa Wilayani, maagizo yawe kuelekeza fedha hizo kwenye Benki kama hizo ili kuzisimamia vizuri, badala ya Wizara kuendelea kuzisimamia. Ila nashauri, Waziri abakie na fedha kidogo ofisini (*Political Vote*), ili anapotembelea vijana Wilayani, asikose kutoa chochote kile kutoptana na ziara hizo za Waziri na Naibu wake. Sera zilizobakia kama walemaru zikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wake kwa kuwasilisha hotuba nzuri na mipango yake kwa utekelezaji wa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Sheria ya Kazi (*Security of Employment Act Cap.212*), Sheria hii inahitaji kufanyiwa marekebisho, hivi sasa utekelezaji wake unachangia kuleta migogoro kati ya wafanyakazi na Waajiri ambao ni wawekezaji wageni kutoka nje. Wawekezaji wanaona sheria hii kama inamlinda zaidi mfanyakazi kuliko mwajiri na kumpa haki zaidi mfanyakazi kupata malipo hata kama atakuwa hakufika kazini kwa makusudi. Hatua za kumdhiliti mfanyakazi kwa kosa la kutouwepo kazini ni ndefu toka Karipio hadi kuweza kumfukuza kazi, ni zaidi ya ngazi tano na katika hatua tatu za mwanzo, bado atalipwa mshahara bila kufanya kazi. Kiuchumi Kanuni hizi zinawakera sana wawekezaji na hivyo kuwafanya wawe jeuri kuwatukana na kuwafukuza ovyo wafanyakazi. Ni vizuri sheria hii ikapitiwa upya kulingana na mazingira ya sasa.

Pili, Sheria ya Kiinua Mgongo (*Severence Allowance Act*), Sheria hii ni ya zamani sana na viwango vyta makadirio ya malipo ya kiinua mgongo ni ya chini sana na haimsaidii mfanyakazi anayeachishwa kazi au kustaaful. Sheria irekebishwe ili kuboresha kiwango cha malipo ya mwisho kwa mfanyakazi.

Tatu, migogoro kati ya Waajiri/Wawekezaji Wageni na Maafisa wa Kazi Mikoani/Wilayani. Kutokana na ugumu wa utekelezaji wa Sheria ya Usalama Kazini na pia tabia mbaya za baadhi ya wawekezaji toka nje katika kuwadharau wafanyakazi na kutaka kuwatumia kinyume na sheria, imeanza kuzuka migogoro mingi kuwadharau na kuwakaripia Maofisa wa kazi wanaposimamia Sheria za Kazi. Kwa mfano, Afisa wa Kazi wa Mkoa wa Tanga, ameandikiwa barua za vitisho na Mwekezaji wa Kiwanda cha Mifuko cha Tanga, kwa sababu alitumia taratibu za kisheria kumfikisha mwajiri huyo Mahakamani! Katika hali hii ni vizuri Wizara husika ikawa makini na kuchukua hatua za tahadhari kuwalinda watendaji wa Wizara wanaokandamizwa kwa makusudi wakati wakitimiza wajibu wao.

Nne, naomba kuchukua nafasi hii pia kumjulisha Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya ya Muheza haina Afisa wa Kazi sasa kwa zaidi ya miaka miwili tangu alipofariki Afisa wa Kazi wa Wilaya aliyeuwepo. Kutokana na hali hiyo, huduma muhimu za kisheria zinafanyika Tanga na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa waajiri na wafanyakazi kutokana na gharama za usafiri. Hali hiyo pia inasababisha baadhi ya Makarani waliopo Ofisini Muheza, kujichukulia madaraka na majukumu wasiyostahili kisheria kuyafanya na kutowatendea haki waajiri na hata wafanyakazi. Hawajui sheria na wanapotosha Sheria za Kazi na kuleta migongano isiyo ya lazima. Tunaomba Afisa wa Kazi Wilaya ya Muheza.

Mwisho, Wilaya ya Muheza ni moja ya Wilaya kubwa sana katika Mkoa wa Tanga na hata ukilinganisha na wilaya nydingi za nchi yetu (Tanzania Bara). Wapo vijana wengi waliokaza nafasi za masomo ya juu na hivyo wanahitaji kusaidiwa. Kutokana na Chuo cha *VETA* - Tanga na Pangani kuwa mbali na kufanya masomo kwa mfumo wa kutwa, inakuwa vigumu vijana wa Muheza kuhudhuria huko. Mwaka 2000/2001, niliomba kwa barua rasmi, Wizara yako ifikirie kuanzisha Chuo cha *VETA* - Muheza. Kwa bahati mbaya hadi sasa sijajibowi maombi hayo na hivyo sijui mwelekeo wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, itatekeleza lini ombi la wananchi wa Wilaya ya Muheza. Naomba kupewa mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote, kwa Hotuba nzuri yenye kuleta matumaini makubwa. Pamoja na hayo, naomba yafuatayo yaangaliwe:-

Kwanza, naipongeza Wizara kwa maendeleo ya *VETA* katika nchi. Kwa kuwa nchi inategemea sana mafundi watakaoelimishwa katika Vyuo vya *VETA*, nakuomba uongeze *intake* na uongeze nguvu ya ukarabati wa vyuo hivyo. Tendo la kuwapa wahitimu vifaa baada ya kuhitimu ni la kupongezwa sana na litiliwe mkazo mkubwa.

Pili, naipongeza Wizara kwa kuratibu *NGO*, zinazohudhumia watoto yatima. Hongera sana pamoja na nia yetu ya watoto walelewe katika jamii, lakini Mheshimiwa Waziri fikiria umaskini wa wananchi ulivyo siku hizi. Mtu akiwa na watoto wengi watalelewa kwa shida mno. Nashauri vituo viendelee kuenziwa na kusaidiwa. Serikali kwa kuitia shulenii, iendelee kuwasaidia watoto yatima wanaolelewa katika familia maskini. Watumishi wa Ustawi wa Jamii, waongezwe kuwafahamu watoto hao vizuri. Walezi wazee wasaidie zaidi kiuwezo na ushauri.

Mikopo ya vijana iweze kusaidia vijana kuondoa umaskini. Ikiwezekana vijana washauriwe kuunda vikundi vya kilimo, ujenzi, useremala na kadhalika. Wasaidiwe na kuanzisha viwanda vidogo vidogo mtaji ukiwa fedha hizo za mikopo. Kituo cha UVIKIUTA cha Dar es Salaam, kiwe mfano kwa maendeleo ya vijana. Kwa kuwa ajira ni ya shida, basi fedha hizo za mikopo zisimamiwe vizuri kuwa chanzo cha ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itafutwe njia nydinge ya kuwatafutia uwezekano wa vijana kushiriki katika uwekezaji, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuwapatia mikopo mikubwa waanzishe vitu vitakavyowawezesha kutoa umaskini. Lazima vijana wawezeshwe kushiriki katika uwekezaji katika nchi zao. Tuendako vijana wanaweza kuathiri amani ya nchi yetu kama hawatashiriki katika uwekezaji wa nchi zao. Saidia vijana sasa washiriki kikamilifu katika uwekezaji kwa kuwakopesha fedha za kutosha.

Nyumba zinazojengwa na NSSF zikopeshwe kwa Wanachama wake kila wanapojenga nyumba, hata hivyo, ninaipongeza NSSF kwa juhudzi zake nyingi wanazozifanya zenye matumaini makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Lakini vema Wanachama wake wafaidike kwa mapato yao.

Napongeza juhudzi za Kituo cha Ajira, kwa bidii kubwa ambayo imeonyeshwa katika hotuba yako. Kuunganisha wanaotafuta kazi na waajiri. Naomba Kituo hiki kitangazwe watu wakijue. Nadhani si watu wengi wanakijua Kituo hiki, tangaza ili watu wajiandikishe.

Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa usimamizi wa Wizara yake kwa kuendeleza michezo na kujitahidi bila kuchoka kusuluhisha migogoro ya michezo. Naomba kwa kushirikiana na Waziri wa Elimu na Michezo iimarishwe mashulen. Napongeza uamuzi wa kuifanya Makongo Shule ya Sekondari kuendeleza michezo. Lakini shule moja haitoshi, wasilianeni mkaongeze shule nyininge zenye kutilia mkazo michezo mashulen.

*Intake* katika Chuo cha Ustawi wa Jamii iongezwe. Wataalam hao wanahitajika sana katika nchi yetu kulinda maadili ya wananchi hasa vijana mitaani na mashulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia kuipongeza tena Wizara, Waziri mwenyewe na wataalam wote, kwa kazi njema. Naunga mkono hoja.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa kutayarisha hotuba hii ambayo ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo mimi mchango wangu naomba nijielekeze katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Wizara itembelee Vikundi vya Ushirika ambavyo vimeanzishwa na mikusanyiko ya vijana kama vile vikundi vya kilimo, uvuvi, useremala na kadhalika. Nasema hivyo kwa sababu endapo Wizara hii itavisimamia vizuri vikundi hivyo vijana wengi watapuekana na suala la uzururaji.

Pili, Wizara itoe kauli maalum kwa wale vijana wasio na kazi waelekezwe kujinga na Vikundi vya Ushirika au Wizara iwe na maeneo maalum ya kilimo (mashamba maalum) ambayo yatawafanya vijana waweze kujitegemea.

Tatu, kuhusu michezo, Wizara iwe na Maafisa wa Michezo wa Kata/Jimbo ili wanamichezo wapate maelekezo ya karibu zaidi badala ya kuwa na Maafisa wa Wilaya peke yake, jambo ambalo husababisha usumbufu kwa wanamichezo Vijijini.

Nne, Wizara iwe na ratiba ya kudumu ya kufanya ziara Vijijini au angalau katika Kata, kuzungumza na viongozi wa michezo wa timu za mpira na michezo ya aina mbalimbali, ziara hizo zikifanyika wanamichezo hao watapata moyo.

Tano, Wizara iwapatie mafunzo ya michezo yanayowahusu huko Vijijini kwa sababu michezo mingi inafanywa bila utaalam kwa mfano, Makocha wa Timu, wataalam wa kilimo wa Vikundi vya Ushirika vya vijana na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, kwamba Wizara ifanye/iandae Kongamano Maalum kwa Vijana Kitaifa ili kujadili mustakabali wa vijana dhidi ya mapambano ya madawa ya kulevyaa na athari zake.

Pili, kongamano hilo liwe ndio kiini cha kuipa nguvu sera ya kuwashirikisha vijana katika mapambano dhidi ya janga hili la madawa ya kulevya.

Tatu, Wizara iandae Kongamano la Kitaifa dhidi ya ajira mbaya ya watoto kwa kushirikiana na *ILO* na Asasi nyingine hapa nchini.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri, ninaunga mkono Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia yafuatayo:-

Fedha zinazotolewa kwa vikundi nya vijana ni ndogo sana, hazitoshii kuanzishia mradi wa kudumu. Ili tuwakomboe vijana wetu kiuchumi, napendekeza viwango nya mikopo/misaada viongezwe kwa vikundi. Kiwango cha chini kwa kila anayekopeshwa kiwe Sh. 500,000/= au kwa kikundi kiwe Sh. 1,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo nya *VETA* vinafanya kazi nzuri ambayo inastahili kupongezwa, ila tu baadhi ya Vyuo mfano Mtwara, hawapati wanafunzi wa kutosha. Kwa hali hiyo, ninapendekeza Wizara iwahamasithe Wabunge wa Majimbo husika, waweke jitihada za makusudi katika kuhimiza na kuwashawishi wazazi waweze kuwapeleka watoto kuijunga na Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na vitendo nya zinaa vinavyojitekeza wakati wa sherehe za usiku za kusherehekea Mwenge, ninapendekeza ya kwamba, sherehe zote za Mwenge zifanyike mchana tu. Usiku Mwenge uhifadhiwe sehemu nzuri ya ulinzi kwa ajili ya safari kwa siku ifuatayo. Sherehe za usiku zisifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nianze kwa kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya yenye dhamira ya kuinua maendeleo ya vijana na maendeleo ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuzungumzia juu ya suala la vijana wafanyabiashara ndogo ndogo waitwao Wamachinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira kubwa ya vijana hawa ni kujenga uwezo wa kujitegemea. Lakini tatizo ni kwamba, hawaajaandaliwa mazingira mazuri ya kuweza kuendesha shughuli zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi vijana hawa hufukuzwa katika maeneo wanayofanyia biashara bila ya kupewa maeneo mengine na inapotokea kupewa eneo basi hupewa eneo ambalo halifai kwa biashara. Lakini mbaya zaidi ni pale wanapofukuzwa, askari wanaofanya kazi hiyo huwapora vitu vyao bila huruma. Hivyo, ninaomba Serikali kuwaenzi vijana hao ili waweze kufanya shughuli zao kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mikopo ya vikundi nya vijana ya uzalishaji mali haikidhi haja. Kama makusudio ya mikopo hii ni kuwaendeleza vijana, basi ni vema viwango nya mikopo vingeongezwa angalau kufikia shilingi milioni 30 kwa kila Jimbo, ili kuwezesha kutoa angalau shilingi milioni moja kwa kila kikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuhusu hali ya Ukimwi. Vijana ni nguvu kazi ya Taifa letu, kwa bahati mbaya sana vijana wengi wanapoteza maisha kutokana na Ugonjwa wa UKIMWI. Ni vema elimu ya kupambana na UKIMWI sasa ifikishwe Vijijini kwa njia ya kuunda Kamati za UKIMWI kwa kila Kata na Kamati hizo washirikishwe watu wa makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuipongeza timu ya simba ambapo mara nyingi sana timu hii huitoa aibu nchi yetu kwa kufikia hatua nzuri katika michezo ya Kimataifa. Naomba timu zinazoshiriki mashindano ya Kimataifa ziandaliwe vizuri ili ziweze kutuletea ushindani. Michezo ni ajira kwa vijana hivyo ni vema ikapewa msukumo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *disco* ni kwamba, naomba Serikali ipige marufuku kuwachezesha vijana wa kike wakiwa uchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri, yenyenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ninapenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa migogoro inaongezeka katika maeneo ya kazi na hasa kwa sababu makampuni/viwanda vinabinafishwa; na kwa kuwa migogoro hiyo inasababishwa na wafanyakazi kutokulipwa mafao yao mapema; je, kwa nini Serikali isiweke mikakati ya kuwalipa wafanyakazi mafao yao mapema kiwanda kinapobinafishwa badala ya kukaa kwa muda mrefu bila kuwalipa na kusababisha migogoro kazini? Kwa mfano, mgogoro wa wafanyakazi wa Shirika la *Tanzania Elimu Supply*, kwa nini wasilipwe mafao yao?

Pili, migogoro katika vilabu vya mipira. Kwanza, napenda kuipongeza Timu ya Mji Mpwapwa kwa kutoshuka daraja msimu huu na kuendelea kushiriki ligi kuu ya *Vodacom*. Kwa kuwa Watanzania wanapenda sana mpira wa miguu lakini mchezo huo unaopendwa na watu wengi hauna maendeleo mazuri kwa kuwa migogoro ni mingi ya kugombea madaraka na matumizi mabaya ya fedha za vilabu hivyo; je, sasa Serikali imeweka mikakati gani ili kuhakikisha kwamba, migogoro hiyo inakwisha katika vilabu vya *FAT* kwa ujumla ili kuendeleza michezo hapa nchini?

Je, *Vodacom* ina mpango gani wa kuongeza fedha kwa vilabu vinavyoshiriki ligi kuu ya *Vodacom* ili vilabu hivyo vishiriki kikamilifu katika ligi hiyo, fedha inayotolewa ni kidogo timu zinahitaji kusafiri Mikoani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa siku za hivi karibuni kumetokea tofauti kubwa ya mishahara kati ya wafanyakazi wa Serikali wenye kwa wenye na kati ya wafanyakazi wa Serikali na Asasi zinazojitegemea mathalani *Executive Agencies*, jambo ambalo linahatarisha umoja na mshikamano wa Watanzania na kumomonyoa amani iliyojengeka kwa muda mrefu, je, Serikali inachukua hatua gani ya makusudi ili kuondoa tofauti hizi kubwa zilizojitekeza kwa lengo la kulinda umoja na mshikamano kwa nchi yetu?

Pili, kwa kuwa siku za hivi karibuni kumetokea migogoro kati ya wafanyakazi na waajiri wao aidha wa mashirika ya umma au mashirika yaliyobinafishwa, mgogoro ambao msingi wake ni Mikataba ya Hiari; je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria zinazohusu ajira hasa katika kipindi hiki ambapo kuna mabadiliko makubwa sana ya kisiasa, kijamii na kiuchumi; je, marekebisheso hayo yatakamilika lini na kuwasilishwa Bungeni?

Mheshimiwa Waziri, anasema nini kuhusu haja kubwa inayojitokeza sasa katika kulinda maslahi ya wafanyakazi wetu hasa katika mashirika yaliyobinafsishwa au kuuzwa kwa watu binafsi mathalani tatizo la wafanyakazi wa *Embassy Hotel*, wafanyakazi wa *TES, NBC (1997) Limited* na kadhalika.

Tatu, kwa vile Umoja wa Mataifa ultangaza *UN Decade for the Disabled*, zaidi ya miaka 30 iliyopita; na kwa vile Tanzania ni mwanachama mwaminifu wa Umoja wa Mataifa; na kwa vile ni zaidi ya miaka 10 sasa Tanzania imekuwa ikitengeneza sera kuhusu watu wenye ulemavu; ni lini sera hiyo itakamilika ili watu wenye ulemavu katika nchi yetu waweze pia kuelewa jinsi wanavyotakiwa kuhudumiwa na jamii na Serikali yao na au kupata haki zao mbalimbali ambazo hadi sasa imeshindikana kutekelezwa pamoja na uwepo wa Sheria kadhaa mathalani Sheria Na. 2 ya mwaka 1982 ambayo imeshindikana kutekelezeka?

Nne, miaka minne iliyopita Mheshimiwa Waziri, aliahidi ndani ya Bunge kusimamia matumizi ya fedha za Mwenge na kuhakikisha kuwa dhana ya chuki kwa Mwenge ambaa ndio chombo pekee, ukiacha lugha inayotunganisha Watanzania Mheshimiwa Waziri aliahidi yafuatayo:-

(a) Kuwa shughuli za Mwenge zitaondolewa chini ya zinayoitwa Kamati za Sherehe za Wilaya ambazo haziko Kisheria na wala haziwajibiki kwa yejote na wala fedha zake hazikaguliwi.

(b) Kuwa ataweka utaratibu wa kupokea fedha za Mwenge kupokelewa yaani risiti maalum na hivyo fedha hizo zifanyiwe ukaguzi kwani michango hiyo ni jasho la Watanzania wengi ambaa hata chakula chao cha siku siyo cha uhakika na wengi hupewa adhabu na faini mbalimbali na bado fedha hizo hazifanyiwi ukaguzi wa aina yejote ile. Sasa je:-

(i) Ni lini Mheshimiwa Waziri atatekeleza ahadi yake aliyoitoa Bungeni ili utaratibu mzuri ukiwekwa hata wale wanaoupinga Mwenge wasiwe tena na sababu ya kuuchukia na kuupinga Mwenge?

(ii) Njia ya uhakika ya *Accountability* ya fedha za Mwenge ni kuweka shughuli za Mwenge chini ya Mamlaka ya Halmaishi kuitia Vikao vya Kisheria na hatimaye mapato na matumizi ya michango ya Mwenge iwe *audited*. Ni lini Mheshimiwa Waziri, atatoa maelekezo au kuleta Sheria yenye lengo la aina hiyo badala ya mtindo wa sasa wa fedha za wananchi kukusanya na chombo kisicho cha Kisheria na ambacho hakitoi taarifa kwa yejote na wala kukaguliwa na yejote, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa Utawala wa Sheria na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya kina ama sivyo hasa kwa hili la Mwenge nina nia ya kutoa shilingi. *Thanks*.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri sana yenye mwelekeo na upeo wa kuleta maendeleo siku zijazo. Hongera sana. Pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote na Wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya Hotuba ya Bajeti ya mwaka huu wa 2003/2004. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni ya Kazi, kinachotakiwa ni kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi, si kazi ya ajira tu bali ni kazi yoyote ile halali. Hivi sasa Watanzania walio wengi wenye uwezo wa kufanya kazi hawafanyi kazi, ikumbukwe kuwa nchi yetu ni maskini, kamwe hatutaondokana na umaskini endapo watu walio wengi hawatashiriki kikamilifu katika kufanya kazi halali. Sheria ya nguvu kazi iliipa Wizara hii nguvu ya jinsi ya kumsimamia vizuri kila mtu afanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Watanzania tuko 35 milioni, idadi hii ni kubwa, Serikali isipokuwa na mpango kamambe wa kuwasimamia Watanzania, utakuwa mzigo mkubwa Kitaifa. Watu wengi ukiwatumia vizuri, mpango kamambe wa kuwashirikisha kufanya kazi utakuwa mzigo kwa Serikali. Nashauri Serikali iwe na mpango mahsus wa kusimamia na kuwafanya watu wote wenye uwezo wa kufanya kazi wafanye kazi. Iwepo Sera ya Taifa ya kuwalazimisha watu kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na jina jipya ni Ustadhi, nisimsahau Katibu Mkuu, Bwana Abubakar Rajabu, kwa kazi nzuri ya kusimamia maendeleo ya vijana, kazi na michezo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imetawanyika katika sehemu nyeti zinazohusisha vijana ambaao ndio Taifa la leo na kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunafahamu ajira hakuna lakini tuna mabonde mengi ambayo Serikali ikijiandaa vizuri, vijana wetu watashughulika na kilimo ambacho watajajiri wenyewe. Ili kuwepo na utaalalm, uandalive utaratibu wa kutoa mafunzo katika Vyuo vya Kilimo kwa kozi fupi ili vijana wetu wawe na utaalalm siyo kubabaisha lakini bado Serikali iwasaidie kuwatafutia soko mara wanapovuna mazao yao. Serikali isiwaache wakae na bidhaa zao bila kuzuza, tutawakatisha tamaa na watazidi kurudi tena Mijini kukaa na kucheza karata tatu na wizi utashamiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Wizara kwa kuanzisha Chuo cha Maendeleo ya Michezo katika Kijiji cha Malya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki sasa hivi ukarabati umekamilika na jenereta ya umeme inafanya kazi. Tunashukuru sana sisi wakazi wa Kijiji hicho kwa kutuletea umeme. Ili basi wakazi wa Malya wafurahishwe zaidi na Chuo hiki, tunaomba umeme wa uhakika upelekwe ukizingatia ni Chuo cha Afrika, jenereta haina hadhi na chuo kikubwa kama hicho. Hivyo, Wizara ya Nishati na Madini ilizingattie hili, wakazi wa eneo hilo wako tayari kuchangia gharama hususan ukizingatia Mji wa Malya umezungukwa na umeme Ngudu, Malampaka na Bukwimba, sasa kuna tatizo gani Malya umeme usiwekwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu kulaani malumbano ya Viongozi wa *FAT*, Serikali ilisimamie hili. Tunataka michezo Tanzania isikike Kimataifa siyo Viongozi kila siku kuongea katika *TV* tu bila kusemea ustadi wa michezo ukoje na mikakati ya kuendeleza michezo hakuna. Naiomba Serikali sasa iweke Sheria kwa Viongozi wanaojinufaisha na fedha za michezo (*FAT*) kwa manufaa yao, wavuliwe Uongozi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, awe karibu sana na wafanyakazi kwa mashirika ambayo sasa yana matatizo kama Shirika la Elimu. Kama Sheria zipo na mikataba ya ajira zao ipo, kwa nini watu walale nje ya jengo la kazi? Sisi Watanzania tusitumie *TV* kuiga mambo ya Mataifa yaliyozoea vurugu. Mheshimiwa Waziri, usikubali haya mambo yaendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kuwapa pole kwa matatizo wanayoyakibili na hasa vurugu katika Sekta ya Michezo ndani ya Klabu hasa ya Yanga na Simba, pamoja na baba yao *FAT* Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza *Simba Sports Club* kwa hatua waliyofikia ingawa hatua hii ilishafikiwa na Klabu ya *Dar es Salaam Young African's (YANGA)*. Wasilewe kufikia hatua hiyo kama inavyoijonyesha bali hatua hii iwe ni kichocheo kwa kufanya vizuri zaidi kwa faida yao na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya michezo nchini bado ni duni na imegubikwa na giza nene. Kama maamuzi ya kishujaa hayatafanywa na Wizara hii, hatuwezi kupata maendeleo katika sekta hii. Tulipofika sasa Mheshimiwa Waziri, anatakiwa achukue maamuzi ya kijasiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendeleza michezo kama vurugu na utovu wa nidhamu unaendelea kwa kasi iliyopo nchini na Wizara inabaki kusononeka na kukata tamaa. Inasikitisha kuona

kuwa Serikali imekata tamaa na kwamba haifikirii kuchukua hatua thabiti za kujikwamua kutoka hapa na hivyo kuridhika kuwa imezidiwa kete na *FAT* (T).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli Serikali imeridhika na kauli ya Mwenyekiti wa *FAT* (T) kuwa Mheshimiwa Waziri, asikaribie Ofisi za *FAT* (T) wala asiingilie uendeshaji wa shughuli za *FAT* (T)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sio kweli kuwa Mheshimiwa Waziri, anamuwalishaa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, katika shughuli za michezo ikiwa ni pamoja na mchezo wa mpira wa miguu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli busara ya Mheshimiwa Rais, ya kumkabidhi Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, dhamana au *portfolio* ya masuala ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo inakuwa *questioned* na mtu mmoja na Serikali inakubali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kitendo hiki kilichofanywa na Mwenyekiti wa *FAT* (T), sio *insubordination* kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais, aliyemchagua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali inataka kusema hajui kuwa kitendo hicho ni *insubordination* ya hali ya juu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hukumu ya mwenye kufanya *insubordination* kwa kiongozi wake Serikali hajui mpaka tuikumbushe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, ni lazima Mwenyekiti wa *FAT* (T), aombe radhi hadharani kama alivyotamka maelezo yake dhidi ya Mheshimiwa Waziri, hadharani katika vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna muafaka wa kusameheana kimya kimya bila tamko la kuomba radhi hadharani, vinginevyo Serikali itaonekana inapiga magoti na kujikomba kwa *FAT* (T) na itajidhalilisha.

Hakuna mantiki ya Serikali kutoa shilingi milioni nane ilizombwa na nyininge kama Uongozi wa *FAT* hautaomba radhi hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge hili tulipitisha Sheria Na. 5 ya mwaka 2003, ambayo ilianzisha Wakala wa Serikali wa *Occupational Safety and Health Authority (OSHA)*. Mheshimiwa Waziri, wakati anawasilisha Muswada huo alisitisiza umuhimu wa kuanzisha Uwakala huo kwa shabaha ya kuimarisha umuhimu wa afya na usalama mahali pa kazi baada ya kubaini kuwa kulikuwa na upungufu mkubwa katika usimamizi wa afya na usalama mahali pa kazi.

Nasikitika kusema kuwa, bado hali ya afya na usalama katika sehemu za kazi ni mbaya hasa viwandani. Wakati wa kupitisha Muswada uliozaa Sheria hii Na. 5 ya 2003, nilieleza umuhimu wa Uwakala huu na nilisisitiza suala la kuwawezesha watumishi husika hasa Wakaguzi kwa nyenzo mbalimbali pamoja na vyombo vya usafiri ili waweze kwenda kukagua na kuona kuwa Sheria, taratibu na viwango vya usalama vinavyotakiwa vinazingatiwa. Kutunga Sheria ni jambo moja na kutekeleza ni jambo lingine. Je, Uwakala huu umeshaanza kazi kikamilifu? Mbona katika Bajeti ya mwaka huu Uwakala haukutengewa fedha za *OC* au za maendeleo, kazi itafanyakaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati akijibu hoja anifafanulie kama fedha zipo na zipo wapi kwani mimi nimeangalia katika kitabu cha pili sikuona.

**MHE. FATMA SAID ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, kwa kusimamia suala la michezo hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo yafuatayo yafanyike tukitaka michezo iendelee hapa Tanzania:-

(i) Kurekebisha Sheria ya BMT, iliyopo imepitwa na wakati, lazima BMT iweze kuwa mahiri ili kukabiliana na Viongozi wanaovuruga michezo nchini.

(ii) Msajili wa Vyama vyaa Michezo havidhibiti vyama na vilabu vinavyokosa nidhamu. Ni vizuri apatikane Msajili ambaye ana taaluma ya Sheria za Michezo.

(iii) Uandaliwe Mkakati Maalum kwa maendeleo ya michezo kwa vijana wetu Tanzania.

(iv) Serikali iwapatie BMT fedha za kuendeleza shughuli za michezo hapa nchini kwani BMT peke yao hawawezi kupata mapato ya kuwawezesha kuandaan programu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kusaidiwa Timu ya Mlandege kwa vifaa vyaa mafunzo kwani hivi sasa imeathirika kisaikolojia.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, ili nami nitoe mchango wangu katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, hoja ambayo ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Awali ya yote, naomba uniruhusu nimshukuru na kumpungeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwanza, kwa kutambua shida ya usafiri inayotukabili watu wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani na pili, kwa kuchukua jitihada za makusudi za katuondoshea shida hiyo. Kesho Jumamosi tarehe 2 Agosti, 2003, Watanzania tutashuhudia tendo la kihistoria la ufunguzi wa daraja la aina yake katika Ukanda huu wa Afrika nalo ni Daraja la Mto Rufiji. Nasikitika sitakuwepo. (*Makofî*)

Nawapongeza sana Mheshimiwa John Joseph Magufuli na wasaidizi wake, kwa kusimamia barabara utekelezaji wa Mradi huu na sisi Wana-Lindi na Mtwara tunaamini kuwa Askari huyu wa Mwamvuli, hatopumzika hadi barabara ya Dar es Salaam, Mchinga, Mingonyo, ikamilike kwa kiwango cha lami. (*Makofî*)

Nawapongeza Wabunge waliotutangulia wakiwemo Waheshimiwa Maalim Sinani Nabahani, Masudi Chitende, Stephen Nandonde na wengine, ambao historia haitowasahau kwa kudai haki ya barabara kwa kiwango cha lami ya Dar es Salaam/Mchinga/Mingoyo. (*Makofî*)

Aidha, nawapongeza wenyeji wa mikoa hiyo ambao pamoja na tangu Uhuru, walijisikia kutengwa kwa sababu ya barabara hii, hawakuiacha CCM na kuijunga na Upinzani. Nitoe rai basi kwa wale wachache ambao walihama CCM kwa sababu hii, warejee maadam lililokuwa limefumba sasa limefumbuka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba kuchangia maeneo mawili tu ya *VETA* na Michezo. Katika *VETA* nianze na ule mchango mzuri wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Wao walizungumzia kwa kirefu sana juu ya bei za bidhaa zinazotengenezwa na *VETA* kuwa kubwa na hivyo watu wengi kushindwa kuzimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya Wananchi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wamewahi kulalamikia kuhusu bei kubwa ya bidhaa zinazotengenezwa na *VETA*. Tayari *VETA* imeanza kutoa mafunzo kwa Walimu wa Ufundii ili nao waweze kuwafundisha wanafunzi wanaojifunza ufundu waweze kufanya mahesabu sahihi kuhusu gharama za bidhaa wanazotengeneza na kuweka faida isiwe kubwa mno ili bei za kuuza ziweze kuwa nzuri na hivyo kuvutia wateja wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mafunzo haya yataanza kuonekana kwa Waheshimiwa Wabunge na wateja wengine katika Maonyesho ya Kibiashara yajulikanayo kama Saba Saba hapo mwaka 2004 au mapema kwa wale watakaovitembelea Vyuo vyetu vyaa *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Waziri Kivuli wa Wizara hii, amechangia mchango ambao kwetu ni changamoto kubwa na ninampongeza na kumuahidi kwamba, tutaufanyia kazi. Amechangia juu ya garama za vifaa kwa vijana kwamba ni mzigoto kwa wazazi, *VETA* iangalie upya juu ya bei za vifaa vyao na Serikali kupitia Wizara, ijenge Vyuo vya *VETA* kila Mkoo ili vijana wapate ujuzi stadi na kujitegemea. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutekeleza azma ya kununua vifaa kwa wahitimu katika Chuo cha *VETA* Mtwara, utaratibu wa kudumu unaandaliliwa ambao unatilia maanani gharama katika kila fani na jinsi ya kuboresha uchangiaji. Mafunzo yametolewa kwa wanafunzi pamoja na walimu wao kuhusu namna ya kukadiria gharama za uzalishaji katika karakana za mafunzo. Kuanzia mwaka 2004, bila shaka bei zitakuwa zimeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kujenga Chuo cha *VETA* kila Mkoo unaendelea kutekelezwa na baada ya kukamilisha ujenzi unaoendelea hivi sasa Kigoma, Mikoa mitatu iliyobaki itaanza kutekelezwa na hii ni pamoja na hoja ya Mheshimiwa Philip Magani. Mikoa hiyo ni Lindi, Pwani, pamoja na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Dr. Pius Ng'wandu, Mbunge wa Jimbo la Maswa, yeye ametaka *VETA* kwa kushirikiana na Shule za Msingi, tuanziszishe masuala ya kuingiza mafunzo ya ufundi katika Shule za Msingi, tuweke vituo kwenye Kata na tushirikiane na Taasisi nyingine.

Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Dr. Ng'wandu kwamba, mafunzo ya ufundi kuanzia katika Shule za Msingi inahitaji ushirikiano kati ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara nynginez. Lakini suala la kuwa na Vituo vya Ufundsi katika kila Wilaya na hatimaye katika kila Kata, haya ni malengo ya muda mrefu kwa sababu sasa tunamalizia kwanza Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ili kuhakikisha utekelezaji wa hoja hii, *VETA* imekwishaanza kushirikiana na Vyuo vya Watu Binafsi. Majukumu yetu ni mengi na makubwa na hivyo tunahitaji fedha nyingi. *VETA* inajitahidi sana kufanya mengi iwezekanavyo kwa kutumia pato lake kila mwaka. Vile vile, tunashirikiana na nchi za *SADC* ili kuhakikisha kwamba, sisi tunatoa uzoefu wetu, lakini tunapata na uzoefu wa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, ameulizia mipango ya *VETA* katika kukiendeleza Chuo cha *VETA* Tabora. Hatua ya kwanza katika kuendeleza Chuo hiki ilikuwa ni kuomba *SIDO* watupatie majengo ya Chuo cha Azimio cha Tabora. *SIDO* wametupatia. Hatua ya pili ni kukikarabati Chuo hicho na kukipanua ili uwezo wake wa kutoa mafunzo ya ufundi uongezekere. Tayari mipango hiyo imekamilika na ukarabati unategemewa kuanza Mei, 2004. Chuo hicho pia kitapatiwi mashine mpya na vifaa mbalimbali vya ufundi. Pia, walimu pamoja na mameneja wake watapatiwi mafunzo. Vyuo vya *VETA* vya Singida, Shinyanga, Mpanda na Ulyanhulu, navyo pia vitakarabatiwa katika mpango huu. (*Makofisi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Philip Marmo, ameshauri Mikoa iliyo nyuma ipewe kipaumbele katika kuongeza Vyuo vya Ufundsi Stadi. *VETA* imekuwa inahamasisha watu binafsi au Mashirika binafsi ili waweze kuanzisha Vyuo vya Ufundsi Stadi au wale wenye Vyuo visivyo bora waweze kuviboresha. Ili kuhimiza haya yafanyike, *VETA* imekuwa inatoa mchango wake kwa wale wanaoanzisha Vyuo na kwa wale wanaokuwa na mipango ya kuboresha Vyuo vya Ufundsi. Ofisi za *VETA* za kila Kanda zimekuwa zinapewa mafungu maalum ya fedha ambazo zinatolewa kwa utaratibu mzuri uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, anataka tujenge Chuo cha *VETA* pale Geita, ambapo kuna watu wengi mmo. Geita ni Wilaya katika Mkoo wa Mwanza, mipango ya kujenga vituo Wilayani itafuata baada ya kumaliza kujenga katika kila Mkoo. Waheshimiwa Wabunge, tuwamalizie kwanza wasio na viatu, halafu tuwatafutie wenye navyo soksi. Tunamwomba Mheshimiwa Rwilomba, avute subira, mipango hiyo ipo mara tutakapokamilisha Mikoa mitatu iliyobakia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Jimbo la Kiwani, anataka Vyuo vya *VETA* vienezwe katika Mikoa yote ya Tanzania. Mipango ya *VETA* kujenga Vyuo vya Ufundu katika kila Mikoa, kama nilivyoeleza ipo na hivi sasa tukimaliza Kigoma itafuata Mikoa iliyobakia ya Lindi, Pwani na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mbunge wa Jimbo la Kilolo, yeze amezungumzia mambo makubwa mawili katika sehemu hii ya *VETA*. Kwanza, ametaka wanaohitimu mafunzo wapewe *tool kit* na pili, *VETA* kujenga Chuo cha Ufundu katika Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa *tool kit* kwa wahitimu wa mafunzo ya ufundu katika Vyuo vilivyobakia utaanza Septemba, 2004 baada ya kufanikiwa Mtwara na Mbeya. Namwomba Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo, ahamasithe Wananchi wa Jimbo lake ili waanzishe Vyuo vya Ufundu wakati *VETA* inajiaandaa kutoka kwenye ngazi ya Mikoa na kuingia kwenye ngazi ya Wilaya, Majimbo na Kata. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, anataka tuanzishe Chuo cha *VETA* pale Wilayani Muheza. Sababu hizi nilizozito za kumalizia kwanza Mikoa, ningeomba Mheshimiwa Mntangi, naye azipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mzee Paul P. Kimiti, Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga, yeze kazungumzia mambo mawili. Kwanza, tujaribu kupata vifaa vya kutumika vyuoni kutoka China ambako ni rahisi na pili, kuangalia matatizo ya watumishi ndani ya *VETA* ili kujua ni nini kinaleta mkingano ndani na nje ya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile Vyuo vinavyotoa *tools* kwa wahitimu, tayari vimekuwa vinatengeneza baadhi ya *tools* katika Vyuo hivyo. Mfano, vifaa vya ujenzi tunatengeneza wenyeewe, vifaa vya *welding* na kadhalika. Vyuo vilivyobakia tayari vimeshaanza kuweka mipango ya kuiga kwa wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* kwa kushirikiana na Wizara yangu, tumekuwa tunajaribu kupata vifaa kutoka nchi mbalimbali na mwaka 2002 tulifanikiwa kupata vifaa vingi na vya thamani kubwa kutoka Japan. Juhudi hizo zinaendelea ikiwemo nchi ya China pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* ina mipango mizuri ya kumaliza matatizo kwa wafanyakazi wake na pale ambapo wamehitaji Wizara isaidie, wamekuwa wakiyaleta Wizardani. Utaratibu mpya umeandaliiwa unaotiliwa mkazo vikao vya wafanyakazi vya mara kwa mara kwa lengo la kuimarisha mawasiliano baina ya wafanyakazi katika ngazi zote. Wale wachache ambao wanapenda kutoa mambo ndani na kuyapeleka nje tunawasihi waige na wafuate taratibu zilizowekwa na *VETA*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mbunge wa Viti Maalum, ametolea mfano wa Vyuo kama vya Mtwara kuwa havipati wanafunzi wa kutosha, Wabunge wa Majimbo husika basi washawishi wazazi kupeleka watoto wao katika Vyuo hivyo. Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mwangunga kwamba, Chuo cha Mtwara kina wanafunzi wa kutosha na tulifanya utaratibu wa makusudi kwamba, *interview* zilipelekwa katika kila Wilaya, Makao Makuu ya Wilaya ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa hiyo, Chuo kile kimejaa. Naomba niwaondolee wasiwasii, lakini ni vyema vile vifaa tukapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu kwamba, Wabunge tuna jukumu la kuhamasisha vijana wetu kujiunga na Vyuo hivi ambavyo kwa ni ukombozi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mbunge wa Viti Maalum, ameshauri *VETA* iongeze idadi ya wanafunzi (*intake*), kwa kuongeza nguvu ya kukarabati Vyuo. Ukarabati na upanuzi wa Vyuo hivyo sasa unaendelea katika Vyuo vya Kagera, Musoma, Mikumi, Oljoro, Dakawa na hatimaye Tabora, Ulyankulu, Singida, Shinyanga, Mpanda na Arusha. Lengo kubwa ni kuongeza nafasi za mafunzo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mbunge wa Singida, anaulizia ahadi ya Waziri juu ya kujenga Chuo pale Singida kwani wamekwishatenga eka 20 tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Chuo cha Ufundı cha *VETA* Singida, kitajengwa upya kwa sababu ni kweli majengo yake hayafai kukarabatiwa. Ili *VETA* iweze kujenga majengo hayo mapya kwenye kiwanja hicho kikubwa kilichopatikana, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Uongozi wa Mjini Singida, ili kiwanja hicho kiweze kukabidhiwa kwa *VETA* mapema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi huo utafanywa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na mojawapo ya masharti ya mkopo huo ni kuwa ujenzi ufanyike kwenye viwanja vinavyomilikiwa na *VETA*, la sivyo fedha haitatolewa na benki hiyo. Mheshimiwa Nguli, kachangamke, nyoka yu aja huyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niingie kwenye nafasi ya michezo. Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, amezungumza mambo makubwa sana. Anauliza: "hivi Serikali imekata tamaa na imeridhika kuwa imezidiwa na *FAT*? Je, Serikali imeridhika na kauli ya *FAT* kwamba Waziri asikaribie *FAT* na asiingilie uendeshaji wa *FAT*? Ni kweli kwamba Waziri anamuwakilisha Rais katika shughuli za michezo ikiwa ni pamoja na soka? Ni kweli kuwa busara za Rais zimezidiwa na mtu mmoja na Serikali inakubali? Hii siyo *insubordination* kwa Waziri na Rais? Je, Serikali hajui kitendo hicho? Mwenyekiti wa *FAT* aombe radhi juu ya matamshi yake dhidi ya Waziri, hakuna muafaka bila kuomba radhi wala hakuna kutoa Shilingi milioni 8 kupeleka *FAT* bila kuomba radhi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hapana, Serikali hajakata tamaa katika kushughulikia matatizo ya *FAT* na Vyama vingine vyta michezo. Aidha, kauli za *FAT* za kumtaka Waziri, asiingilie shughuli za *FAT* hazina msingi kwa sababu Waziri anayo mamlaka ya kusimamia michezo yote ikiwemo *FAT* kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Wizara imepokea ushauri na maoni ya Mheshimiwa Missanga na itaendelea kuyafanya kazi ingawa suala la kuomba radhi ni utashi wa mtu binafsi. Kwa kawaida mwenye kuomba radhi ni yule anayetambua kuwa amemkosea anayewomba radhi, kama hajui hilo hukaa hivyo hivyo mpaka wakati inapofika hujuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema tukawakumbusha wenzetu kuwa Waziri Profesa Kapuya, aliteuliwa na Rais, akaapishwa kumsaidia katika Sekta hii ya Michezo, anapozuka raia wa nchi hii kwa jina lolote liwalo, kutilia shaka uamuzi wa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri, inatisha, kama anavyosema mdogo wangu Maulidi wa Kitenge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, amesema sheria zinazolinda michezo hasa *FAT* ni mbovu na ziangaliwe upya. Viongozi wabovu washughulikiwe na mengine mengi kuhusu *FAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inafahamu, katika Katiba za Vyama vyta Michezo na sheria inayosimamia michezo, kuna upungufu mkubwa na ndiyo sababu katika hotuba yangu nimeainisha kazi zitakazofanywa ili kurekebisha mapungufu hayo. Lakini ni vyema Watanzania tukafahamu kuwa, pamoja na upungufu huu wa Katiba ndani ya *FAT* na kanuni ngumu za *FIFA*, *FIFA* haipo Tanzania tu, ipo katika nchi nyingi za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tatizo si *FAT* wala tatizo si *FIFA*, tatizo ni Watanzania wachache walioamua kuweka maslahi yao mbele na kuwa tayari kusaliti furaha ya Watanzania milioni 34 na ushee. Kwa sababu kama watu wa mitaani, watu wa kwenye vyombo vyta habari na Wabunge, wote wanakupigia kelele wewe, halafu maskini ya Mungu husikii wala huoni, nafikiri huu hauwezi kuwa ubingwa hata kidogo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Waziri Kivuli, alinifundisha msemo wa Kipemba kwamba, kuna ng'ombe kule akitiwa wazimu huitwa kipole, yeze anachokuta njiani hukikumba tu! Basi mtu mmoja akawa anaswali na Waislam tunaposwali hatuzungumzi. Mpwa wake akamwambia: "Ami mtu akiswali hasemi, lakini akiambiwa husikia, kipole yu aja huyo." Aliacha sala akaondoka! Lakini hawa wa kwenye *FAT* hata wakiambiwa kwa gitaa bado hawasikii, lakini nasema siku inakuja na wala si muda mrefu

kuanzia sasa, Mwenyezi Mungu, atupe subira mambo yatanyooka na Watanzania watafurahi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, Mheshimiwa Estherina Kilasi, naye amezungumzia suala la *FAT*. Kwa kweli hatuna majibu mengine kuhusu *FAT* zaidi ya haya. Nafikiri tumejieleza vya kutosha juu ya *FAT*. Pia, Mheshimiwa Kilasi, amezungumzia tena uhakika wa kukamilika uwanja wa kisasa mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekeiti, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, itakapofika tarehe 15 Mei, 2005 uwanja wa kisasa wa michezo utafunguliwa pale Dar es Salaam. Naona Mheshimiwa Mbunge wa Temeke anafurahia sana kwa sababu mara nne alikuwa akipigia kelele uwanja usipelekwe Jangwani ubaki Temeke, uwanja uko Temeke mama. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, lakini Mheshimiwa Kilasi, alizungumzia vile vile juu ya mahesabu ya *FAT* hivi yanakaguliwa na nani? Pia, Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema hayajawahi kabisa kukaguliwa!

Mheshimiwa Mwenyekeiti, kweli kuna matatizo katika mahesabu ya *FAT*, lakini *FAT* wanao wakaguzi wa mahesabu ya fedha zao kama ilivyo kwenye Katiba yao na ambayo hutakiwa kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu wa *FAT* wa kila mwaka. Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria iliyopo, Msajili anaweza akavitaka Vyama kuwasilisha kwake taarifa za fedha za Vyama zilizokaguliwa. Aidha, anaweza akaagiza kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha kila inapobidi.

Mheshimiwa Mwenyekeiti, mara ya mwisho taarifa za fedha za *FAT* zilikaguliwa mwaka 2000, hatua iliyofanya Serikali kuwafikisha Mahakamani baadhi ya Viongozi, kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha. Kesi hiyo bado inaendelea mpaka hivi sasa. Nashindwa kuhoji kwa nini kama sauti ya chini inavyonitaka, kwa sababu Mheshimiwa Kapuya, alipouliza kule: "Mbona kesi nyingine za kushtakiwa Kapuya zimeamuliwa haraka haraka hii bado?" Ndio akaambiwa asikaribie *FAT*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, Mheshimiwa George M. Lubeleje, nae amezungumzia kwa uchungu juu ya maendeleo mabovu ya soka. Lakini Mheshimiwa Lubeleje, usije ukafikiria Viongozi wote wanapenda soka kama unavyopenda wewe. Umejikalifu takilifu kutumia pesa zako na wakati wako kuhakikisha Mji Mpwapwa inafanya vizuri hata kuifunga Simba. Umejitahidi mpaka Mji Mpwapwa imebakia kwenye nane bora. Kama Viongozi hawa tunaowazungumza hapa, wangekuwa na moyo huu wa kuthamini zaidi michezo kuliko ubinafs, nafikiri leo tusingekuwa tunazungumzia mambo haya hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, kwa niaba ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Lubeleje, kwa kazi hii nzuri anayoifanya. Tutaishauri *Vodacom* kwa maombi yako Mheshimiwa Lubeleje, kuona uwezekano wa kuongeza ufadhili kwa vilabu vinavyoshiriki ligi kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, Mheshimiwa Margaret A. Mkanga, ametoa pongozi kwa Wizara kuwashirikisha walemaru katika michezo, tunaipokea sana. Lakini ameagiza kwamba, uwanja mpya uhakikishe kwamba, unakidhi mahitaji ya walemaru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, tunamhakikishia Mheshimiwa Mkanga kwamba, uwanja huu wa kisasa au ujenzi wa eneo changamani (*Sport Complex*), unazingatia mahitaji yote ya walemaru, toka kwenye maliwato, maeneo yao ya kukaa na maeneo yao ya kupita. Pia, toka kwenye uwanja mpya, uwanja wa historia wa kisasa ambao unatumika sasa hivi, viwanja vya kuogelea, *theatre* na mpaka kwenye Chuo cha Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekeiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, ameshauri Utawala na Uongozi wa *FAT* ujiuzulu, kwani wanaidhalilisha michezo na kuendeleza migogoro. Eeh, *Wallahi* wamekusikia mama. Wamekusikia kama walivyowasikia Watanzania miaka nenda miaka rudi. Nami naamini kwamba, hawa ni watu wazima na waungwana, wakiwa hawana haya ya uso, hawakosi na zinduko la moyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya ngoma hii ya kwenye *FAT* tunaishabikia. Ngoma kama haina mashabiki haiwezi kukesha hata kidogo! Hata ngoma ya wachawi (mahepe), kama haina mshabiki ingawa inachezwa usiku gizani bado haiwezi kushabikiwa! Bahati mbaya wale wanakaa na maajuza na mashaibu ndio ngoma inaendelea kidogo. Hebu tuacheneni kushabikia haya makundi, tuyaache yenye we tu tuone kama watafika mbali. Tupo wengi tu tunashabikia, sijui kama na humu tumo, tunashabikia na sisi tumejigawa kwenye makundi haya! Hebu tuwaacheni wenye we tu, watajiuzulu kesho tu. Lakini kila mmoja akifikiria kwamba ana kundi lake, basi wanapata nguvu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, ameshauri michezo ya mitupo ya kuogelea nayo iendelezwe isiwe *football* tu. Kwa kweli napenda kumuunga mkono, bahati mbaya Watanzania sasa hivi ukizungumzia mchezo wanazungumzia mpira wa miguu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana hata Mheshimiwa mmoja amesema: "Hakuna chochote kilichofanyika kwenye michezo nchi hii." Yeye hana hata habari kwamba, tumeweka vijana pale Makongo katika mpango huu wa John Steven Akhwari, tunawasomesha na tumeshawapeleka na nje. Kwa mfano, wale vijana wakimbiasi wameshakwenda nje mara tatu kule Australia na mara zote mshindi wa kwanza na wa pili wanashika wao. Vijana hawa tunawaandaa mahsus kwa ajili ya mashindano ya *Olympic* mwakani kule Ugiriki, tunajitahidi. Hata mashindano haya ya mipira ya mikono bingwa wa Afrika ni Mtanzania, timu ya *handball* ya Tanzania. Kwa hiyo, si kweli kwamba tumedharau kila kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nguli, lakini najua huu ni mchango wa uchungu, kwamba kwa sababu *FAT* haifanyi vizuri, basi sasa hivi watu sote tumehamisha mawazo yetu yapo *FAT* tu na tumefikia mahali tunasahau vile vile mbaya ni nani katika zogo hili la mpira wa miguu. Watu wengine wamegawanyika wanassema Serikali mbaya, wengine *FIFA* mbaya, wengine *FAT* mbaya, tunawaacha wabaya wenye we na wenye we wanafurahia wamekaa kimya! Wabaya tunawajua ni hao hao ambao Mama Shamsa Mwangunga, anataka wajiuuzulu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa na uwezo ule wa kusema *out*, ningewaambia sasa hivi *out*, bahati mbaya sina. Lakini Mheshimiwa Nguli, hata *cricket* na ngumi sisi ndio tunaongoza hapa tunafanya vizuri. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, naye amezungumza kwa uchungu kweli kweli juu ya michezo. Masuala ya *FAT* nimeeleza, lakini ningependa nikujibu hili kwamba, Waziri Kapuya anahitajika na ile timu iliyotuletea medali 18 za wale vijana wetu akawaone kwa sababu hajawaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimthibitishie Mheshimiwa Mwamoto kwamba, Mheshimiwa Kapuya, ametuma nauli kwa vijana wote walioshiriki, ameandaa pesa za malazi na chakula kwa ajili ya vijana wale kuja kusalimiana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye amewahitaji Dar es Salaam tarehe 10 Agosti, 2003 kwa ajili ya kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Remidius E. Kissassi, ametoa ushauri mwingi sana. Tumeyapokea mawazo yake na ushauri mzuri na tutayazingatia kikamilifu. Yatakayowezekana sasa tutayaanza mara moja, yale ambayo yatahitaji kupata ushauri wa wenzetu zaidi tutafanya hivyo, lakini tunapenda tumthibitishie kwamba, hili suala la UMITASHUMTA na UMISETA Mheshimiwa Waziri, atazungumza na wenzake Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Philip S. Marmo, ameeleza kwamba, Kamati ya *John Steven Akhwari Foundation*, haijakutana hata siku moja toka ianzishwe. John angeweza kuunda Kampuni yake, lakini kwa uzalendo ameiachia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Marmo, kwa kusaidia kuainisha baadhi ya matatizo ya michezo, tumeyapokea na tunayazingatia kikamilifu. Lakini suala la *John Steven Akhwari Foundation*, Tawi la Tanzania limekwishakutana mara tatu tangu ilipoundwa. Aidha, Timu ya Taifa ya Vijana ya Riadha iliyoko chini ya Taasisi hiyo, inaendelea na mafunzo yake katika Sekondari ya

Makongo na vijana wawili, Patrick Marwa Joseph na Nyangerwa walishinda katika nafasi ya kwanza na ya pili katika *Sydney Marathon* na ikiwa ni mara ya tatu vijana wetu kuongoza mashindano hayo huko Australia. Kutokana na Mwenyekiti wa Kamati kuteuliwa kuwa Balozi huko Zimbabwe, Wizara yangu itateua Mwenyekiti mwingine na kuona uwezekano wa kuteua Wajumbe wengine ili kuimarisha Kamati hiyo. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunapenda kupokea ushauri wa Mheshimiwa Profesa Henry R. Mgombelo, juu ya masuala ya soka pale Tabora Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, ametoa maoni kuhusu Chuo cha Malya na Viongozi wa *FAT*. Tunayapokea maoni ya Mheshimiwa Nyawazwa na tunamwomba atusaidie kupitia vikao nya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, waone umuhimu wa kufikisha umeme wa gridi hadi Chuo cha Malya. Tumeweka jenereta pale kwa sababu umeme wa gridi haupo, suala la migogoro linaendelea kushughulikiwa mama. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, ameulizia kwamba, mbona Timu ya Simba wanafanya vizuri si Watanzania? Tunakubali wanafanya vizuri na nataka nikuthibitishie kwamba, maoni ya Mheshimiwa Salim Omar Ali, ya kesho kufanya mauaji katika Uwanja wa Jamhuri yatakamilika. Lakini napenda nikuthibitishie kwamba, kama Yanga watashinda, *FAT* hawataweza kuwapokonya *point* zao tatu kwa sababu *FAT* inaendeshwa kwa kanuni, lakini tunazingatia vile vile malalamiko yanayotolewa kwamba, wakati mwingine Viongozi wa Michezo basi watawaliwe zaidi na busara kuliko hamasa za mapenzi. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kivuli na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri na ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofsi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao mingi yenye manufaa, maelekezo na ushauri ambao kwa kweli hata kama tukijitahidi vipi, kwa muda tuliopewa haiwezekani tukayajibu yote au hoja zote ambazo zimejitokeza hapa. Lakini nataka nichukue nafasi hii kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hatuna tutakaloliacha, yote tutaya fanyia kazi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Haroud Said Masoud, ambaye ndiye aliwasilisha hoja kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Kama kawaida yetu, michango ya Kamati ile ni ya maana na tutaitilia maanani katika utekelezaji wetu. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Msemaji Mkuu wa Upinzani katika Wizara hii, naomba nami nikupongeze sana kwa hotuba yako ambayo kwa kweli imedhamiria kujenga kuliko yale matamshi ambayo tulikuwa tumeyazoea huko nyuma. Kwa hiyo, ninakupongeza sana. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba niwatambue wale wote ambao wamechangia hotuba hii nikianzia na wale ambao wamechangia kwa maandishi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme, Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu, Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Khamis Awesu Abood na Mheshimiwa Rhoda Kahatano. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Dr. Talala B. Mbise, Mheshimiwa Philip A. Magani, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Lekule M. Laizer, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi,

Mheshimiwa Hadija K. Kusaga, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri na Mheshimiwa Edson M. Halinga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo vile vile wapo ambao wamechangia kwa kuzungumza humu Bungeni nao ni Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, Mheshimiwa Remidius E. Kissassi, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine, Mheshimiwa Estherine Kilasi, Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri wote waliochangia wameunga mkono hoja, lakini wapo waliosema Shilingi wanaiweka kwanza mfukoni, watairudisha wakati tukijibu hoja. Nina hakika baada ya juhudzi za Mheshimiwa Naibu Waziri, Shilingi zote zimesharudi. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Khalifa Mohammed Issa, ulianza na tatizo kubwa la ajira, ukasema hili ni tatizo sugu nchini asilimia karibu 30 ya vijana hawana ajira na kwamba ukosefu wa ajira unawafanya Watanzania wasione hata umuhimu wa kupeleka watoto wao shulenii. Haya masuala mawili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inajua kwamba, lipo tatizo la ajira nchini. Kwa hiyo, siyo kwamba, sisi tumekaa kimya tukidhani kwamba *all is well* hapana!

Sasa katika kulitatu hilo na nataka nizingatie mchango wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, japo kwa ametoka amesema *it is cross cutting issue* ni kweli si *issue* ambayo inaweza ikashughulikiwa na Wizara moja tu. Ni *issue* ambayo Wizara zote kwa pamoja zinashirikiana katika Serikali nzima, kuhakikisha kwamba zinapanua ajira.

Katika kufanya hivyo Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, inakuwa ni mratibu, ndio chachu ya kuweza kuonyesha njia. Kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge katika miaka mitatu/minne ya nyuma tulikuwa katika mpango unaoitwa *Jobs for Africa*. Mpango wa *Jobs for Africa* ile ilikuwa ni kama hatua ya utafiti, baadaye umezaa *Country Action Programs* ambazo zilikuwa karibu 17. Katika *Country Action Programs* tumezigawa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linaitwa kundi A, miradi inayohusu kukuza uwezo wa uchambuzi wa sera na uratibu wa shughuli za kukuza ajira. Ajira hapa haitakuwa kubwa lakini itakuza uwezo wa wadau wengine kuweza kupanua ajira, miradi katika kundi hili itakuwa kama ifuatavyo:-

Kukuza uwezo, kuimarisha Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo hususan katika eneo la takwimu za ajira, kufanikisha utafiti wa sera isiyo rasmi na usimamizi wa sera ya ajira, kujenga uwezo wa ofisi za Wilaya na taasisi husika zinazoratibu ajira, kujenga uwezo wa taasisi zilizo katika ngazi ya chini (*Community Level Organization*), kujenga uwezo wa wadau wetu (*Social Partners*), kuanzisha kituo cha ajira *Centers for Employment Studies* na uhamasisaji na ushauri kuhusu masuala ya ajira. Kundi B, ni miradi inayohusu kujenga uwezo wa kuimarisha ukuaji wa ajira kwa kutoa nyenzo muhimu katika shughuli za ajira, miradi katika kundi hili ni kama ifuatavyo:-

Mipango ya ajira katika sekta ya ujenzi na mawasiliano karibu nafasi 9,000 katika awamu ya kwanza, huu ni mpango ambao Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, tumeshawasilisha *ILO* kwa pamoja tunaushughulikia. Vile vile kuanzishwa kwa kitengo cha kukuza na kusimamia taratibu nzuri katika Sekta ya *Macro-Finance* hii tunategemea itazaa ajira karibu mia tano kila mkoaa, kukuza mafunzo ya taaluma kwa ajili ya kuajiriwa kwenye ngazi za chini ya jamii, tunategemea itaongeza nafasi za ajira karibu 1200, kuimarisha Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, tunategemea kwamba, itaongeza nafasi za ajira karibu 20,000. Vile vile Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, alipokuwa akizungumza juzi hapa nadhani wenywewe mmesikia *demand* iliyopo, lakini na juhudzi ambazo Serikali inafanya kuendelea kukurabati Makambi haya.

Vile vile kukuza uwezo wa wanawake kujajiri katika eneo la kilimo cha bustani na shughuli nyingine karibu ajira 2,200, msaada wa wachimbaji wadogo wadogo karibu nafasi 400, ukuzaji wa kilimo cha uyoga karibu nafasi 10,000.

Miradi ya kundi B inahusu sekta mbalimbali kuhusiana na masuala ya jinsia katika maeneo yote ya ajira, kudhibiti Ukimwi sera na kazi, miradi kuhusu walemvu, miradi itapendekezwa kwa wahisani mbalimbali na hii tumeshaanza na karibuni tutakuwa na kikao cha pamoja kuangalia sasa tunaanzia wapi. Vile vile nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hata *ILO* bado iko pamoja na sisi hata katika *ku-lounge* hizi programu ili kuhakikisha kwamba, sasa tunaanza kupambana na tatizo la ajira kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lilizungumzwa ni lile la kusema kwamba, watoto wanaokwenda shule hawapati kazi. Kama tukilipigia debe hilo tutakuwa tumelifikisha Taifa mahali pagumu, kwa sababu lazima tutambue kwamba, elimu kazi yake ni kumpanua mtoto Mtanzania upeo wake wa kuweza kujitegemea. Kwa hiyo, asifike mahali anapokosa kazi ya ofisini akasema sasa mimi ni mtu wa jehanamu, hapana! Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge, hili kwa kweli tulipigie debe kwa pamoja kwamba, elimu kazi yake ni kufungua mapazia ili wawe sasa ama katika kazi za ofisi au kazi zingine zozote uweze kushika hatamu za kujitegemea mwenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile imezungumzwa kuhusu taratibu za kupata leseni zirahisishwe, hili nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, akasema kwamba, kutokana na hali hiyo basi tuna msemo wa kwamba watu wajajiri, hivi mtu aliyesomea Utawala anajari vipi? Hapa ndipo ambapo tunahitaji *Counselling*. *Counselling* inaanza kwanza kwa wazazi, *Counselling* inakuja katika shule, kuwe na *Counselling Officers* wa kutosha kuweza kuwaelekeza vijana katika vipaji vyao mbalimbali katika sehemu zao mbalimbali wakilinganisha na takwimu ambazo kituo cha *Centre for Employment Studies* kitakuwa kimekusanya kikitoa picha halisi ya ajira zilizopo nchini. Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo basi tunapounganisha nguvu hizi, mimi nina hakika tutakuwa na watu ambao kile wanachokisomea ama kipo kwa wakati ule ule au hakitachukua muda mrefu kupatikana.

Lakini kama tutakwenda kusoma kwa sababu ya kusoma tu hii ndiyo maana unaweza ukajikuta wakati mwininge unakuwa na watu ambao ni *redundant*, lakini kwa elimu ile ile wakigeuza basi na kuweza kutafuta vyanzo vingine vya kujitegemea, mimi nina hakika hata aliyesomea Utawala anaweza aka-*achieve*.

Vile vile imezungumzwa kwamba, watoto yatima wametengwa katika vyuo, vijana hawa wabaki katika jamii na familia. Kwa kweli huu ndiyo msimamo wa Wizara, tunasema kuwapeleka watoto katika vituo iwe ni *option* ya mwisho kabisa. Tungependa Watanzania turudi katika utamaduni wetu zamani za mababu hakukuwa na mtoto aliyejewa anazura mitaani. Mtoto alikuwa ni mtoto wa jamii, mtoto wa kijijij, huko ndiko tunatakiwa turudi ndugu zanguni. Kwa hiyo, tukishafanya hivyo na Serikali yenu hii kama jinsi ilivyo *humanitarian as it is*, mimi nina hakika nayo itajua namna ya kuweza kusaidiana na walezi wale jinsi ambavyo wataweza kusaidia watoto ambao wako katika familia hizo.

Vile vile imesemwa kwamba, watoto watukutu kesi zishe haraka, nakubaliana na wewe Mheshimiwa kama alivyokuwa akizungumza Mheshimiwa Niabu Waziri, hapa wakati mwininge vipaumbele vya sehemu mbalimbali huwezi ukazielewa kesi za michezo zinakwisha haraka, kesi za dhidi ya viongozi wa michezo haziishi haraka, kesi hata dhidi ya watoto zinachukua miaka sita unashangaa. Lakini hilo nalo tutaendelea kusukumana ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *VETA*, nadhani hilo limeshaelezwa. Zawadi kwa wafanyakazi, wafanyakazi wachaguane wenyewe. Mimi nakuhakikishia ndivyo ilivyo. Kama kuna mahali ambapo pametokea matatizo basi ni kwa bahati mbaya.

Vile vile imezungumzwa kwamba ajira inapendelea wageni. Hili la ajira kupendelea wageni, Waheshimiwa Wabunge, si sahihi, kinachotokea ni kwamba, wale wageni wanapokuja wanakuwa na *study* fulani fulani ambazo wanahitaji kuajiri wageni. Sasa kinachopishana hapo ni jinsi mafao yalivyo, hilo naweza nikalikubali tatizo hilo tunalo. Lakini huwezi ukaniwa kampuni hapa Tanzania ambayo utaniambia kwamba, ukichukua takwimu za wafanyakazi walio pale ukute *majority* ni wageni na Watanzania ni wachache, hilo si kweli. Kwa hiyo, hilo tatizo la mafao tunalo.

Lakini tunalo tatizo vile vile la kupuuza sheria zetu za nchi, hilo nakubali ndiyo maana Wizara hii inajitahidi kuwarudisha katika mkondo wale waajiri wakorofsi wachache ambao wanajaribu kudharau Sheria za Nchi yetu, kupuuza Vyama vya Wafanyakazi, kunyanyasa wafanyakazi, hayo matatizo yapo. Lakini kusema kwamba, waajiriwe wengi wawe ni wageni, hilo nadhani siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumziwa ni kuhusu masuala ya Mwenge. Imesemwa kwamba, Mwenge unachochea watu kulewa pombe, ngono. Hili nadhani ningeliunganisha na Mheshimiwa Salim Omar Ali, naye alikuwa akizungumza kwamba, yanayozungumzwa pale ni ya CCM na sare zinazovaliwa ni za CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kukurejesha Mheshimiwa Mbunge, kwenye mchango wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alisema kuna mambo fulani fulani lazima tuwe juu ya siasa (*We have to be above Politics*), mambo ambayo yanatu jenjea utambulisho katika dunia hii, tukianza kufanya nayo mchezo, tutakuwa tunajimaliza sisi wenye we kwa sababu tutafika mahali tutakuwa hatuna utambulisho. (*Makofsi*)

Unapokuwa na mazungumzo ya kuukejeli Mwenge, ukidhani Mwenge ni lazima Mwenge ufile mahali ndiyo watu wagundue kwamba kumbe kunawezekana kufanya ngono, hivi kweli? Kama hiyo ingekuwa ndiyo sababu ya Ukimwi kuenea nchi hii, vijiji vya Watanzania viko karibu 20,000 Mwenge unalala kwa mwaka katika vijiji 365 hivi kasi ya Ukimwi tulio nayo ingekuwa kubwa kiasi hiki kweli kama chanzo kingekuwa ni Mwenge? Haiwezekani! Halafu vile vile ni kuwafanya Watanzania hawa kwamba, akili yao kila wanapokutana wanachojua wao ni mambo ya ngono tu basi, hakuna mengine ambayo yanaweza kufanya, lazima tuwaheshimu Watanzania kwamba, wana akili, wanajiheshimu, wanaweza wakakutana, wakazungumza bila kugusia mambo hayo. (*Makofsi*)

Vile vile kwamba zinavaliwa sare za CCM. Mimi sijui Mwenge gani ulikwenda kuushangilia. Kwa sababu Miende yote ambayo mimi nimehudhuria kama Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, *uniform* zao ama ni *maroon* au kama za mwaka huu ni kaki, sijui chama gani kina *uniform* za kaki, siyo CCM *for sure*. Hata zile *slogan* wanazotumia hata uchaguzi wao wanavyoteuliwa wengi utakuta wanatoka katika vyombo vyetu vya dola kama Majeshi, Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa, JWTZ. Huu U-CCM unatoka wapi? Kama rafiki yako mmoja alizungumza akasema CCM oyee! Nadhani alipokuona tu pale akajua ndiyo matunda yetu yale yale, kwa hiyo, nadhani alikuwa anakuburudisha. (*Makofsi*)

Labda niende moja kwa moja kwenye suala lingine vile vile lilojitekeza la Mheshimiwa Mariam Mfaki. Nilimwomba Mheshimiwa Naibu Waziri, aliache hili japokuwa lilikuwa linahusu michezo. Mavazi mabaya na kumomonyoka kwa maadili. Mheshimiwa Mariam Mfaki, tunalo tatizo, tatizo hili ili tuweze kulitatta tunahitaji nguvu za pamoja. Chanzo kikubwa cha maadili haya, chanzo kikubwa cha mavazi haya ni sisi wazazi. Kama wote sisi wazazi tungejua kwamba, hili ni baya, kwa kweli yasingetokea. Mimi nakuhakikishia Mheshimiwa Mariam Mfaki, hili nimelijibu kwa sababu najua historia yake, *otherwise* hili ni suala la Elimu na Utamaduni. (*Makofsi*)

Wakati nilipokuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, tulijaribu kutilia mkazo sheria inayosema watoto wa chini ya umri wa miaka 18 wasiende kwenye mabaa, adha tuliyopambana nayo kwa watu wazito ilikuwa ngumu sana. Mtu anakuambia unakujaje kuminiliki katika familia yangu, kunichagulia hata mahali ambapo naweza nikaenda na mtoto? Kwa wenzetu Ulaya inahemishika hapa kwetu ni tatizo. Kwa hiyo, kasheshe kubwa ni kwa wazazi, kama wazazi mngeamua isingewezeekana. (*Makofsi*)

Lakini la pili wanaonyanyasika katika mavazi kweli ni wanawake na wasichana. Lakini na sisi akina mama tuna vyombo ambavyo navyo vinaona kwamba, kumwambia msichana avae nguo za staha ni kumyanyasa kijinsia, ninyi mnafahamu, TAMWA inakampeni hili kwamba usimwambie hata mtu namna ya kuvaan unamnyanyasa kijinsia.

Sasa unaiambia Serikali, Serikali inafanyaje katika mazingira kama haya? Vyombo vya Habari navyo vitusaidie. Mimi nadhani mmeshaona *television* za Ulaya utakuta watu wanapocheza kama wamevaa ovyo ovyo kamera, hailengi pale. Lakini kamera za Waandishi wa Habari wa hapa wako tayari hata kupiga magoti chini ili wampige mama kwa hivi. Sijui *why?* Sijui wapi na wapi! (*Makofsi/Kicheko*)

Kwa hiyo, tusaidiane haya. Ninyi wenyewe mtaona angalieni vyombo vya habari, hawa wenye Vyombo vya Habari kuna mmoja nilizungumza naye nikamuuliza hivi wewe huoni hata miziki mizuri ya Tanzania? Huoni mambo mazuri ya Tanzania kuonyesha? Wakati niko Wizara ya Elimu na Utamaduni, akasema Mheshimiwa Waziri, *lets face it there is nothing present to show about Tanzania. Really!* Hii ndiyo *mentality* ya baadhi ya waanzilishi wa Vyombo vya Habari katika nchi hii. Sasa ndiyo nasema tusaidiane kwa pamoja, kama jinsi ambavyo tunacho Chama cha Kupambana na Ukimwi cha Wabunge, hebu basi tuanzishe na chama kingine cha kuhamasisha jamii juu ya mavazi. (*Makofsi*)

Vile vile Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Makamu Mwenyekiti, amezungumzia upungufu wa watumishi katika Mahakama ya Kazi, Mheshimiwa Mbunge, hilo tumeanza kulisahihisha kwa mifano, sasa hivi tunaye Msajili wa Mahakama ameshaajiriwa, Manaibu Wenyevitit wawili wameshaajiriwa, bado tuna upungufu lakini katika kasma ya mwaka huu tutaendelea kuziba mapengo hayo.

Labda la Ma-miss ambalo nilikuwa nimelisau hapa, Mheshimiwa mmoja anaitwa Mheshimiwa Lekule Laizer, anasema upendeleo wa ma-miss kwanza kuna wasichana wafupi warembo eti wanaambiwa siyo warembo kwa sababu ya ufupi, hii ni kuwanyima haki baadhi ya watu. Akasema nakataa urefu siyo urembo, wafupi wakidai haki Mahakamani mtashindwa. (*Makofsi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mchezo una kanuni zake. Sasa mimi sijui ni kama wakati ule wa Mkoloni Askari ilikuwa mpaka uwe mrefu kama mimi au Cheyo hapo, wafupi wafupi walikuwa hawachukuliwi. Baadaye nadhani hata wafupi watakuja kutiliwa maanani. Vinginevyo wewe na Mheshimiwa Benedict Losurutia, labda na Mheshimiwa Parseko Kone pale, mnaweza mkatengeneza mashindano mengine mkaja mkapata kibali mkahusisha wanawake wafupi nao wakapata haki yao. Hakuna matatizo. (*Makofsi/Kicheko*)

Vile vile Mheshimiwa George Lubeleje, amezungumzia juu ya migogoro kazini. Suala la migogoro kazini limezungumzwa na Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa George Lubeleje. Waheshimiwa Wabunge, tuko katika kipindi cha mpito hivi sasa. Tulikuwa na taratibu zetu za uchumi, tumebadilika tumeingia katika mazingira ya *Free Market Economy*. Hii ina kanuni zake.

Sasa katika mazingira haya ya mpito wafanyakazi wanajaribu kujipanga upya na waajiri nao kujipanga upya. Ndani yake bado kunahitajika elimu kubwa. Sasa wakati bado hajajizatiti katika kupanua elimu ile ndiyo unakuta kunatokea vurugu hizi tulizo nazo. Lakini nataka niwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali iko *on top of this situation*. Katika mazingira ya *Free Market Economy*, suala la Utatu tunaliheshimu sana, lakini mazungumzo yanapoanza huendi wewe Serikali moja kwa moja kusimamia, ndiyo maana huwa mnaona tunasubiri kwanza waendeele na mazungumzo, kama kila mmoja atasimama katika mstari wa sheria inavyopatikana, Serikali huhitajika pale. Hii ni *Two Free Parties* ambayo wanapaswa kujadiliana mpaka kufikia muafaka. Inapofika sasa ukiukaji wa sheria ndipo ambapo Serikali inapokuja kuingilia kati, inapokuja kudharau kanuni ndipo Serikali inapokuja kuingilia kati. Kwa hiyo, msitegemee katika mazingira ya *Free Market Economy*, *Free Enterprise* kwamba, tutakuwa tena sisi Serikali moja kwa moja ni wasimamizi wa moja kwa moja, wewe mwajiri njoo hapa na wewe mfanyakazi njoo hapa anzeni mazungumzo si kweli. Lazima wazungumze wao kwa wao kwa sababu mfanyakazi ndiye anayejua anazalisha kiasi gani na huyu tajiri anajua *value* ya huyu mfanyakazi, lazima wazungumze. (*Makofsi*)

Kwa hiyo, migogoro hii ni suala la mpito lakini Serikali inapobidi nawahakikishieni (*we shall put this situation under control*), tutadhibiti hali na uchumi wetu hautayumba.

Kwa hiyo, ndiyo yaliyojiteza *NBC*. *NBC* kilichotokea ni kwamba, walikuwa na mkatuba wa hiari ukaisha, wakataka kujadiliana mkatuba wa hiari mpya lakini mwajiri akadhani anaweza akakata kona kwa kuacha kuzungumza na Chama Kikuu cha Wafanyakazi, bali azungumze na wafanyakazi wa pale pale, chama cha wafanyakazi kikataa, ndiyo kikataka kuitisha mgomo. Tulipoingilia Serikali tumerejesha hali nzuri, kwa hiyo, hii ndiyo mambo yanavyokwenda. Hivi sasa *management* wanajua kwamba la kwanza lazima waheshimu Uongozi wa *TUICO* Taifa, la pili, wasiwapangie wafanyakazi namna ya kupata viongozi wao watakaokwenda kujadiliana nao na la tatu kwa sababu hali hii ilijitokeza katika hali ya

vurugu, hakuna kufukuza mfanyakazi yeote wala kuwakata mishahara kwa siku tatu ambazo wamekaa nje. (*Makofî*)

Vile vile imezungumzwa tofauti kubwa ya mishahara kati ya Serikali na wafanyakazi, hilo lilichangiwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Wafanyakazi wa Serikali na *Executive Agencies*. Ushauri huu tumeupokea tunaufanya kazi. Migogoro ya kazi nimeshajibu.

Vile vile Mheshimiwa Herbert Mntangi, amesema Sheria za Kazi zifanyiwe marekebisho. Hii tayari tumeshaanza awamu ya kwanza tumesha kamilisha na sheria hizo zitakuja Bungeni Oktoba, 2003. Awamu inayofuata itakuwa ni awamu ya pili. Wakati tunatayarisha Muswada wa kuleta hapa, wakati huo huo tutakuwa tunakwenda na awamu ya pili kumalizia zile sheria zilizobaki. (*Makofî*)

Pia Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, amesema ushauri umetolewa kwa Wizara iandae kongomano la Kitaifa dhidi ya ajira mbaya ya watoto kushiriki na *ILO* na asasi nyingine. Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, nataka nikuhahakishie kwamba, hili tunalifanya kazi jinsi ambavyo tunaweza kulitekeleza hili kwa sababu kwa kweli ajira mbaya ya watoto ni moja ya kumnyang'anya haki mtoto, unamwachisha kucheza, unamkosesha elimu na mabaya mengine kadha wa kadha. Kwa hiyo, unakuwa uzaa mtu ambaye ni mpumbavu au mijinga wa baadaye katika Taifa hili na hatimaye kwa sababu hana stadi zingine zozote atakuja kuishia katika mahali pabaya.

Pia Mheshimiwa Rhoda Kahatano, amezungumza kuhusu kutangazwa kwa Kituo cha Ajiri. Mheshimiwa Rhoda Kahatano, tunatangaza katika magazeti, redio, *television* mara kadhaa na pia tumeshiriki katika Maonyesho ya Ajiri (*Job Fair*) Apili, 2002 na Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Sabasaba mwaka 2002/2003. Lakini nakubaliana na wewe kwamba, bado tunalazimika kufanya juhudu kubwa zaidi. Vile vile mtafute kazi. Jinsi kituo kile kinavyofanya, mtafuta kazi anakwenda pale anajiorodhesha na sifa zake na tunamruhusu achagua kazi kama tano, wakati huo huo tunapokea waajiri, nao wanaleza nafasi za kazi walizo nazo na *qualifications* wanazohitaji, uzoefu wanaohitaji, halafu sisi tunafanya *job matching*, tukiona mfanyakazi tuliyie naye anaweza akafanana na kazi hii tunamwita, tunamfundisha hata namna ya kuandika *CV*, tunamfundisha hata baadhi ya maswali ambayo tunategemea anaweza aaulizwa katika kazi ile ili aweze kupata nafasi. Kwa hiyo, tunajitahidi Mheshimiwa Rhoda Kahatano. (*Makofî*)

Vile vile Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, amesema Serikali iwe na mpango mahususi wa kusimamia watu kufanya kazi, amesema ni kwamba kila mtu mwenye uwezo lazima afanye kazi. Nakubaliana na wewe Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, lazima wafanye kazi wote lakini hatuwezi kurudisha sheria ya nguvu kazi kwa sababu hiyo tutapambana na *ILO* kwamba, tunalazimisha watu kufanya kazi (*Force Labour*) na hiyo nayo sasa hivi imepitwa na wakati, tujitahidi basi sisi viongozi wa kisiasa kuwashamasisha vijana kwamba, wasichague kazi, kazi ni kazi, upimo wa mtu uwe ni kazi. (*Makofî*)

La kuhusu vijana kujifunza kilimo nadhani nimejibu. Mheshimiwa Mohamed Missanga, ameuliza je, Wakala ameanza kazi kikamilifu baada ya Sheria Na. 5 ya 2003. Mheshimiwa Mohamed Missanga, napenda kukumbusha kwamba, Sheria ya Afya na Usalama sehemu za Kazi Na. 5 ya 2003 haikuanzisha *OSHA*, Wakala wa *OSHA* umeanzishwa chini Sheria ya *Executive Agency Act No. 30* ya 1997, ambayo inaaniszisha Wakala zote za Serikali. Sheria na Afya ya Usalama mahali pa kazi Na. 5 ya 2003 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu katika kikao chake cha 10 kwa ajili ya kuboresha usalama wa wafanyakazi sehemu zote za kazi. Lakini nakubaliana na wewe kwamba, iko haja ya ku-double juhudu katika kutekeleza majukumu yake ili ianze kuonekana kwamba, sasa yale meno ambayo tumewapa kwa kuititia sheria hii, ambayo inaongeza usalama mahali pa kazi na afya mahali pa kazi, basi kweli wafanyakazi wafaidike nayo. (*Makofî*)

Vile vile Mheshimiwa Paul Kimiti, amesema pongezi kwa Wizara kuanzisha Wakala wa Usalama Sumbawanga, hizo pongezi tunazipokea Mheshimiwa Mbunge na kukusanya hela zilizokusanywa. Nataka hela tulizokusanya na nataka kuwashakikishia kwamba, mwaka huu wa fedha *OSHA* itafanya bidii kuongeza ufanisi zaidi.

Kumezungumzwa Idara ya Ajira, Mheshimiwa Salim Mohamed Ali, nadhani nimejibu yale masuala ya Mwenge na CCM. Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ameuliza miaka minne iliyopita Waziri

aliahidi kusimamia michango ya Mwenge. Ili kukidhi masuala ya Mbunge, Wizara imetua mwongozo wa mbio za Mwenge wa Uhuru unaotoa utaratibu wa usimamizi wa shughuli za Mwenge katika ngazi zote. Nadhani kama umesoma Kitabu changu nimesema vile vile tumefanya tathmini kamili kuhusu mbio za mwenge. Kutokana na tathmini hiyo ndiyo tutatoa taratibu zetu mpya. (*Makofit*)

Vile vile imezungumzwa Idara ya Ustawi wa jamii, *VETA Colleges*, nadhani Mheshimiwa Margarth Mkanga, umeshajibiwa. Idara ya Ustawi wa jamii kutotajwa kwenye jina la Wizara ya Kazi, Vijana na Michezo. Nadhani jina la Wizara pamoja na kwamba halitaji walemavu lakini imepewa umuhimu wa hali ya juu kabisa kwamba, Sekta zingine ni kurugenzi wakati Sekta ya Walemavu ni kamisheni. Kwa hiyo, ina kamishna, sekta zinazoongozwa na walemavu na hata Kibajeti ukiangalia Bajeti yetu wao wanashika nafasi ya pili baada ya Idara ya Kazi. Kwa hiyo, kwa huu umuhimu kwa kweli tumejitahidi kuwapa. (*Makofit*)

Vile vile imeelezwa kwamba, kitengo hiki kihamishiwe Ofisi ya Waziri Mkuu. Serikali ndiyo inayoamua. Lakini nataka niwahakikishie kwamba, hata hii Wizara ya Kazi ni Ofisi ya Waziri Mkuu, yeze si ndiyo Wizara zake zote hizi. Kwa hiyo, yeze ndiyo anayetu-*direct* sisi namna ya kuendelea na shughuli hizi. Kwa hiyo, hata mimi nataka kuwahakikishia kwamba, hata hapa haiathiriki sana.

Pia imeulizwa kwamba, baada ya sera kupita kinafuata nini? Mikakati ya utekelezaji inaanaliwa, majibu ya *NSSF* Mheshimiwa Peter Kabisa, ameuliza Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha Sheria ya *NSSF* kwa mfanyakazi anayeacha kazi kabla ya kufikisha umri wa kustaifu alipwe. Hii tutaizingatia katika Sera ambayo tumeshaipitisha wakati tunatengeneza sheria, hilo kwa kweli tatalizingatia.

Pia imeulizwa kwamba je, wanachama wa *East Africa* wakistaafu tu wawe wanapata malipo yao kwa mkupuo. *Otherwise* mengine ni pongezi tu. Mheshimiwa Venance Mwamoto, anataka ajengewe soko hili watu wa *NSSF* watakwendwa kumtembelea, wafanye tathmini kama inawezekana watajitalidi. (*Makofit*)

Pia imeulizwa kuhusu Shirika la Tija la *NIP*, Shirika hili lilianzishwa kwa chombo cha kusaidia sehemu za kazi kuongeza tija, linafanya hivi kwa njia ya utafiti mafunzo ya utekelezaji. Lakini ni kweli mbinu zake zimepitwa na wakati, mazingira yake yamebadilika, hivi sasa Bodi imeanza kulifanyia kazi ili libadilike liende na wakati. (*Makofit*)

Vile vile imeulizwa kwamba, Shule ya Buigiri, Mheshimiwa Mfaki, shule hii iko chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, tutawafikishia habari hizo. Sheria Kongwe tumeshazungumza, Mheshimiwa Ruth Msafiri amesema kuna huyu Mama Adwele, ambaye analea watoto angependa Serikali imfikirie namna ambavyo inaweza ikamsaidia. Hili tunalipokea tutaaingalia ambavyo tunaweza tukasaidia. (*Makofit*)

Pia Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, ameuliza haki za watu wenye ulemavu kuingizwa katika Katiba, hili tutaaingalia jinsi ambavyo tunaweza tukasaidiana na Watanzania wengine, kama linawezekana wazo hili likapokelewa katika mabadiliko ya Katiba ambayo Serikali inategemea kuyaleta.

Pia Mheshimiwa Edward Nziriyi Ndeka, amesema namwomba Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ambaye Jimbo lake linapakana na langu, la Kigoma Kusini, awapelekee shukrani zangu wapiga kura wake wa vijiji vyta Kaliua, Usinge na kadhalika, kwa kuendeleza ujirani mwema kama walivyofanya baada ya ushindi wangu wa kishindo katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kigoma Kusini na kujumuika na wenzi wao katika kata za Mwenegoha, Maganzo na kadhalika. Hizo salamu zimefika Mheshimiwa Mbunge. (*Makofit*)

Vile vile Dr. James Wanyancha, kwamba shule zetu zimejaa walimu wa Kingereza kutoka nje. Mheshimiwa Mbunge, hilo tatizo tunalo lakini ni lazima Wizara ya Elimu na Utamaduni ikarabati Idara yake ya Mafunzo ya Kingereza.

Kuhusu Taasisi ya Ustawi wa Jamii ameuliza Mheshimiwa Mariam Mfaki. Chuo cha Ustawi wa Jamii kipandishwe cheo kuwa Chuo Kikuu. Mazungumzo tumeshaanza ya kuzungumza na Mjumbe na Chuo Kikuu cha Dar es Saalam. Katika ku-*operate plan* ile inavyokwenda ndiyo tutakopofanya utathmini kama tunaweza tukapandisha daraja kuwa Chuo Kikuu.

Pia Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, ameuliza taasisi imeanza kutoa mafunzo ya *diploma, fine*, lakini majengo yake yanatia homa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, kama ungetembelea sasa hivi ungekuta kuna maghorofa makubwa ya hosteli za wanafunzi, sasa hivi tumeanza ujenzi wa *administration block* na fedha bado tunaendelea kutafuta lakini kazi imeshaanza. Kwa hiyo, hilo tumeshatambua. (*Makofi*)

Vile vile kuhusu sera ya watu wenye ulemavu, limezungumzwa na Mheshimiwa Margaret Mkanga. Nakuhakikishia kwamba, *by* Oktoba sera hiyo itakuwa imeshakamilika kuitishwa kwenye Baraza la Mawaziri, tutakutana. Kwa hiyo, naomba ile shilingi uliyokuwa unataka kutoa Mheshimiwa Margaret Agnes Mkanga, uniachie kwa sababu nina watoto saba watakosa chakula. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo

##### Fungu 60 - Mahakama ya Kazi

Kif. 1001 - <i>Administration and General</i> .....	.....	Sh. 293,482,200/=
Kif. 2001 - <i>Arusha Zone</i> .....	.....	Sh. 85,583,000/=
Kif. 2002 - <i>Dar es Salaam</i> .....	.....	Sh. 72,588,500/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

##### Fungu 65 - Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo

Kif. 1001 - *Administration and General* .... ... Sh. 711,492,247/=

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Vote 65*, programu ya 10, Utawala. Mimi sina sababu ya kutoa shilingi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini nimeona nizungumze haya niliyonayo kwa sababu sikupata nafasi ya kuongea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, huwezi kutumia nafasi hii kuzungumza yale uliyotaka kuchangia. Kwa hiyo, utauliza swali au namna nyiningine.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali kwa sababu sikupata nafasi ya kuliuliza. Kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, kwa msada alionipa kuhakikisha uwanja unajengwa Temeke. Kwa hiyo, naomba Wana-Temeke wamenituma ili apeleke salama hizi kwa Mheshimiwa Rais.

Uwanja huu utaanza kujengwa mwezi Novemba, sasa ombi langu nilikuwa naomba watakapoanza kujenga, yule Mkandarasi asaidie kutoa ajira kwa vijana wa Temeke hususan akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anasemaje kuhusiana na hili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutazingatia maoni ya Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nataka maelezo.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** *Program ten, sub-vote 1001*, nilitaka kupata ufanuzi, sisi ni washabiki kabisa wa mpira, lakini michezo siku hizi imezorota kwa sababu ya mtu mmoja na ningependa kupata maelekezo kwamba, huyu mtu ambaye amevuruga timu za Tanzania mpaka tukawa washabiki wa timu za Ulaya, mimi na Mheshimiwa Kapuya ni washabiki wa *Manchester*, tumerema Simba tumekwenda *Manchester* kwa ajili ya mtu mmoja, atachukuliwa hatua gani? (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mtaje.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Ndolanga na timu yake. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hili halitajibwa kwa sababu Ndolanga hawezi kujibu hapa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... Sh. 123,919,177/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1003 - *Policy Information Development* ... ... Sh. 219,040,309/=

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia, nilieleza kwamba, sehemu hii ya *Policy and Planning*, nina matatizo nayo kuhusu sera. Hiyo ya juu na hiyo *sub-vote* yote. Lakini kwa sababu maelezo yamekuwa kwamba Oktoba sera itakuwa tayari, basi sina ugomvi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 - *Macro - Economy* ... ... ... ... Sh. 902,797,217/=

Kif. 2002 - *External Sector* ... ... ... ... Sh. 456,172,620/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 4001 - *Social Welfare* ... ... ... ... Sh. 1,794,134,970/=

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika programu ya 40 *Sub-Vote 4001*, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa ni kipindi kirefu sana hajatoa ruzuku kwenye Makao ya Watoto Yatima ya Rulenge na Nyamahanga, Ntoma na vituo vinginevyo Mkoani Kagera; Je, mwaka huu atatoa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikuwa tumesimama kutoa ruzuku sio katika Kituo cha Rulenge tu, katika Vituo vingi. Hii ilikuwa inatokana na uwezo mdogo wa Serikali. Lakini hivi sasa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshaanza na tunategemea kufika Rulenge mwaka huu. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 5001 - *Youth Development* ... ... ... ... Sh. 819,311,082/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 6004 - *Sports Development* ... ... ... ... Sh. 412,520,678/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu hii programu Na. 60, kifungu 6004. Kwanza, nataka tu niipongeze Wizara kwa kujitahidi kuendeleza baadhi ya michezo. Lakini inaonekana sasa tunaingia kwenye ujenzi wa *facilities* za michezo na katika kuendeleza michezo wakati tunakubali Katiba za baadhi ya Vyama vya Michezo vya nje na vya ndani, kuzuua jitihada zetu za kuongeza ufanisi katika michezo, hususan mchezo wa mpira ambao naweza nikasema kwamba, ni mchezo wa Kitaifa hapa kwetu, sasa hivi tuko kwenye jitihada za kujenga *Stadium* mpya, lakini hatujaweza kufanya vizuri katika mchezo wa mpira kwenye nyanja yoyote isipokuwa Simba wakati huu katika mazingira magumu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Waziri aliambie Bunge lako hii *impotence* ambayo Wizara inayo, tumeshuhudia ugomvi kati ya Wizara na Bwana Ndolanga, Bwana Ndolanga akashinda kwa *intervention* ya vyombo vya nje na tunashuhudia sasa ugomvi, mpaka jana kuna wengine walisema tumefikia muafaka, Ndolanga akaja akasema hatujafikia muafaka. Mheshimiwa Waziri, atakuwa *held ransom* mpaka lini? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufanuzi juu ya swali alilouliza Mheshimiwa Lamwai, kama ifuatavyo:-

Tungependa kurekebisha kwamba, ugomvi haukuwa kati ya *FAT* na Wizara, ilikuwa tu ni Bwana Ndolanga, kumuelewa vibaya Mheshimiwa Waziri na ndio maana juzi wakati najibu swali hapa nilisema, namshukuru Waziri, kwa kutokuendeleza mpambano na matokeo yake akaamua kuua kwa kutumia asali badala ya sumu, ambayo ni uungwana mkubwa sana.

Lakini suala la kwamba, Bwana Ndolanga alishinda katika kesi ile, Ndolanga hakushinda. Sisi tulifkiria maslahi ya Watanzania, hivyo kweli wakati ule kulikuwa na Simba Mkubwa na Yangu zinawakilisha Taifa hili. Lakini kulikuwa na suala la Serikali ya *Zanzibar Football Association (ZFA)*, hao wote walikuwa na *interest* ya kwenda kucheza. Hivyo, tuwazuie kwa sababu ya mtu mmoja? Kama tungekubali kufungiwa, pale Ndolanga angekuwa ameshinda. Lakini kwa sababu sisi tuliamua kumuacha ye ye ili hawa waendelee kucheza kuiwakilisha nchi yetu, sisi tunahisi kwamba ndio tulishinda.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Lamwai na Wabunge wengine wote kwamba, hatua tunazozichukua sisi, zitatufikisha mahali kumalizana na Mwenyekiti huyu wa *FAT*, kwa usalama na amani bila kuacha matatizo mengine pembedi kuliko kama tutachukua *shortcut*. Naomba tustahimiliane. (*Makofî*)

**MHE. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yasiyordhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, *concern* yangu ni kwamba, pamoja na ile *intervention* ya *FIFA* ya wakati ule ilifanya Bwana Ndolanga arudi kazini na tukakaa kimya, sasa hivi tumeona tena *intervention* nyininge ya *FIFA*, ambayo baada ya maamuzi ya Mahakama yetu ambayo tumeiunda Kikatiba na Kisheria tunaambiwa kwamba, *FIFA* ina-dictate juu ya sheria zetu. Pia tuna *weakness phenomenon* ambayo Bwana Ndolanga, pamoja na kilio cha wananchi kwamba jiuzulu, hususan Mheshimiwa Makamba Dar es Salaam amemwambia waziwazi ajiuzulu, ye ye hajakubali kuijuzulu. Je, Mheshimiwa Waziri, kwa busara zake hawezi kujadiliana na Bwana Ndolanga akatuachia mpira wetu tukauendeleza? (*Makofî*)

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, aliposema kwamba, tunatafuta njia za kuweza kulimaliza tatizo hili bila kuzusha matatizo mengine pembedi, ni kwa kuzingatia mikakati ambayo imekwishaanza katika kuondokana na tatizo hili. Moja ambalo lilitaka kutokea sasa hivi, Bwana Ndolanga, ameshaandikiwa barua, anaitwa na Kamati ya Maendeleo ya Jamii ya ya Bunge hili na anakuja ye ye na Kamati yake yote ya Utendaji, waje wajieleze na kwa sababu hii ni sauti ya wananchi watajua kwamba, sasa nchi imeamua kuwa *serious* kupambana na tatizo hili. (*Makofî*)

Kuna siku tulijibu swalii la nyongeza hapa kwamba, hivi inawezekanaje fundi cherehani akawa Katibu Mkuu? Tatizo tulilonalo ndugu zanguni, ni kwamba, baadhi ya viongozi wetu wa vyombo vya michezo ni watu ambao walikuwa matajiri zamani, wamefilisika, hawana kazi, sasa namna ya kumtoa

mahali pa kazi anapopatia riziki ni kazi kweli kweli! Ndio tatizo lingine tulilonalo hilo. Ndio maana ni vyema ukawa na mtu ambaye ana kazi yake yoyote ile hata kama ni msukuma kwama lakini inampa riziki kuliko kwenda kugombea uongozi wa michezo halafu ukaona hapo ndio pa kupata riziki. Ndiyo tatizo kubwa tulilonalo nchi hii. (*Makofî/Kicheko*)

Kwa hiyo, mimi nakuhakikisha Mheshimiwa Lamwai kwamba, Wizara itashirikiana kwa ukamilifu kabisa na Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, ili kuhakikisha kwamba, tatizo hili linafikia mwisho. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wanyancha, mradi isiwe suala la *FAT* kwa sababu huwezi kusema suala lile lile katika kifungu kile kile. (*Kicheko*)

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sizungumzii *FAT*, mimi katika kuchangia nilisema kila Mtanzania ana haki yake Kikatiba na hivyo mtu anapokuwa ana haki yake Kikatiba ni lazima mwingine asimbughudhi na nikasema kwamba, ndugu yetu Wambura hatendewi haki na Ndolanga na nikamwomba Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba Ndolanga anamtendea haki Mheshimiwa Wambura. Je, Mheshimiwa Waziri, atashughulikia hilo suala? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona sasa tunajadili watu, kifungu kinaafikiwa?

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

##### **Fungu 65 - Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... Sh. 3,649,577,300/=

Kif. 6004 - *Sports Development* ... ... ... ... Sh. 5,000,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

#### **T A A R I F A**

**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima, imeyapitia Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa mwaka 2003/2004, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Hivyo, kwa heshima naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha makisio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

*(Hoja iliamuliwa na na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa Mwaka 2003/2004  
yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo. Kwanza kabisa, kuna tangazo linalotoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Anasema kwamba, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kesho tarehe 2 Agosti, 2003 saa tano asubuhi katika Chumba Na. 81 nadhani kuna Mkutano.

Tangazo la pili, sasa msinishangilie hapa. Mimi timu yangu ni Nazareth. Kesho kuna mpira tarehe kati ya Yanga na Palson ya Arusha saa 9.30 jioni. Wabunge wanakaribishwa. *(Makofi)*

Halafu tarehe 3 Agosti, 2003, *Bunge Sports Club* inatakiwa kwenda Kongwa kwenye Mechi na *Kongwa Veteran*. Mabasi yataondoka hapa saa 4.30. Kwa hiyo, kwa wale wote wanaofikiri wanataka kwenda kule na kushangilia timu yetu ya *Bunge Sports Club*, mabasi yatakuwepo hapo nje saa 4.30. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naahirisha kikao hadi Jumatatu, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.16 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 4 Agosti, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*

